**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 9 Agosti, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. ZAYNAB MATITU VULU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE):** Maoni ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY - (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:** Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 366

**Kuigawa Wilaya ya Geita**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, vigezo vya kugawa Wilaya ni pamoja na ukubwa wa eneo na idadi ya watu na kwa kuwa, Wilaya ya Geita inakidhi vigezo hivyo:-

Je, ni lini Serikali itaigawa Wilaya ya Geita?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uundaji na ugawaji wa wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 kwa (Mamlaka za Wilaya) na sheria Na. 8 kwa (Mamlaka za Miji) za mwaka 1982 na Sheria za Uanzishaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994. Sambamba na Sheria hizo vigezo muhimu vilivyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, kwenye Waraka wa Mwaka 1995 ni pamoja na:-

1. Eneo la Wilaya moja lisilopungue kilomita za mraba 5,000;
2. Idadi ya Tarafa zisizopungua 5;
3. Idadi ya Kata zisizopungua 15;
4. Idadi ya Vijiji visivyopungua 50;
5. Idadi ya wakazi wasiopungua 100,000; na
6. Jiografia ambayo inafanya huduma kwa wananchi kuwa ngumu kwa sabau ya milima, mito, misitu, maziwa, mabonde au visiwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vigezo hivi wananchi wa eneo husika wanatakiwa kuwa na nia ya kugawa Wilaya yao kuwa zaidi ya moja na waombe rasmi. Maombi yanatakiwa kuambatanishwa na baraka za Vikao husika katika Ngazi za Wilaya na Mikoa na yaeleze bayana sababu za kutaka Mkoa au Wilaya igawanywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Geita, ina vigezo vinavyostahili kuifanya igawanywe kwani ina kilometa za mraba 7,825, Majimbo 3 ya Uchaguzi Kata 33, Vijiji 187, idadi ya watu 782,782 kwa mujibu wa sensa ya 2002.

Aidha, kwa kuzingatia vigezo hivyo, zipo Wilaya nyingi sana zinahitaji kugawanywa kwa kuwa ni kubwa kieneo na zina idadi kubwa ya watu kwa mfano Wilaya ya Kasulu ina watu 628,667 na Wilaya ya Mbozi ina watu 515,270. Kwa kutumia vigezo vilivyopo kigezo cha watu pekee kinafanya Wilaya 27 zihitaji kugawanywa na kuzingatia ukubwa wa eneo Wilaya 32 zinahitaji kugawanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa Wilaya au maeneo mapya huwa muafaka endapo Serikali inalo fungu la kuyajenga Makao Makuu ya Wilaya, gharama za uendeshaji na uwekazi miundombinu muhimu pamoja na watumishi katika Wilaya husika. Ugawaji wa Mkoa au Wilaya huigharimu Serikali takriban shilingi bilioni 1 kwa

Wilaya na bilioni 4 hadi 6 kwa Mkoa. Hivyo, Serikali hugawa maeneo kwa awamu kulingana na uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali itaendelea kugawa maeneo mapya ya kuitawala ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Geita kadri uwezo wa kifedha utakavyokuwa unaruhusu ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa urahisi na kutimiza ahadi ya Serikali ya awamu ya nne ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. (*Makofi*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Geita inavyo vigezo vya kufanywa igawanya na kwa kuwa iko namba moja kwa zile Wilaya kwa maana idadi ya watu lakini pia hata nataka awe *specific*.

(a) Je, Serikali iko tayari kuigawa Wilaya hiyo kwa mwaka huu wa Fedha kwa kuanzia tuanzie Geita mwaka huu na kama sivyo ni lini?

(b) Kwa kuwa wananchi wa Geita kupitia Baraza lao la Madiwani wameshakaa na kupendekezo kuhusu kugawanywa kwa Wilaya je, Serikali iko tayari kuheshimu maamuzi na kuyabariki kwamba Wilaya mpya sasa iitwe Nyang'hwale na na Makao Makuu ya Wilaya hiyo iwe mji mdogo wa Karumwa? (*Makofi*) (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi kwamba Wilaya ya Geita ina vigezo ambavyo vinatakiwa igawanywa na zipo Wilaya nyingi ambazo zina vigezo muhimu ambavyo vinatakiwa vigawanywe. Masuala yote hayo yameshawasilishwa katika ofisi yetu na ofisi yangu inayachambua hayo maeneo ili kubainisha ni lipi lipewe kipaumbele katika kugawa katika mwaka huu wa fedha na mwaka ujao wa fedha.

Kuhusu suala la kupitisha kwenye vikao husika ni kweli Wilaya ya Geita imeshapitisha suala la kuigawa hiyo, Wilaya katika vikao vyote vinavyohusika na imeshawasilishwa katika ofisi yetu. Kama nilivyosema kwamba tuko katika mchakato wa kuchambua Wilaya hizo zote kwamba ni Wilaya ipi ambayo tuipe kipaumbele kulingana na uzito na vigezo husika. Pia tunaangalia na uwezo wa kiuchumi kama nilivyosema kwenye suala langu la msingi.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba iko haja ya kuweza kugawa hizi Wilaya na kwa hesabu yake amesema ziko 37. Je, atakubaliana nami kwamba inahitaji watulie ili uamuzi huu ufanyike bila kuchelewa kwa sababu ya kuleta maendeleo ya nchi kwa haraka? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Waziri Mkuu niseme yafuatayo kuhusiana na eneo hili la ugawaji wa maeneo mapya.

Tulishawahi kulieleza jambo hili hapa Bungeni kwako tukatoa idadi ya Wilaya ambazo tunadhani zinastahili kugawanywa. Lakini tukaeleza vile vile Wilaya hizi zitakuwa zinatolewa kidogo kidogo kwa sababu kuna gharama kubwa sana wakati wa kuanzisha Wilaya hizi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, bado mimi nafikiri nitoe rai kwa Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla kwamba jitihada za Serikali zitaendelea lakini itakuwa ni vigumu sana kufikiria kwamba tunaweza tukaanzisha Wilaya Mpya kwa mara moja karibu 30 na zaidi si rahisi mzigo utakuwa mkubwa kuliko tunavyofikiria. Lakini tunatoa ahadi kwamba kila itakavyowezekana tutawasilisha mapendekezo haya kwa viongozi wa kitaifa na yale yatakayoonekana yanabadalika basi tutakuwa tunatoa kidogo kidogo. (*Makofi*)

Na. 367

**Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025**

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI (k.n.y. MHE. COSMAS M. MASOLWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumbukumbu zinaonyesha kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ilishaingia katika mpango wa muda mrefu wa Maendeleo ya Taifa, mpango wa kwanza, mwaka 1964 – 1980, mipango wa pili mwaka 1981 – 2000 na sasa mpango wa tatu unaohusu Tanzania yote ujulikanao kama kama Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 unaohusu Tanzania Bara tu:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha kutokuwa na mpango mmoja wa muda mrefu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyokuwa katika mpango wa pili wa taifa wa maendeleo?

(b) Je, Serikali haioni vema kuwa na mpango wa pamoja wa maendeleo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuondoa utata kwa wafadhili kuliko ilivyo sasa ambao dira ya Taifa ya Maendeleo Tanzania Zanzibar 2020 inatofautiana na ile ya Tanzania Bara?

(c) Je, Serikali imepanga vipi kwenye mipango yake ya maendeleo suala la ahadi za Mheshimiwa Rais, kwenye hotuba yake ya tarehe 30.12.2005 juu ya kuchangia maendeleo ya uchumi wa wananchi wa Tanzania, Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** atajibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa si sahihi kwamba Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, inahusu upande mmoja tu wa Jamhuri ya Muungano, yaani Tanzania

Bara. Tukumbuke kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, katika maandalizi yake ilishirikisha wadau mbalimbali Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Miongoni mwa walioshirikishwa ni Wabunge wa Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar. Aidha, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ilijadiliwa na makundi mbalimbali Bara na Visiwani vikiwemo vyama vya siasa, viongozi wa madhehebu mbalimbali ya dini, Jumuiya za Wanawake na Vijana, Vyama vya Wafanyabiashara na wenye viwanda, wakulima, wasomi watu mashuhuri katika histori ya nchi yetu na wananchi wa kawaida. Hivyo kwa kuzingatia muktadha huu utaona kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inajumuisha Watanzania wote Bara na Visiwani na ni yenye malengo shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwapo kwa Dira ya maendeleo 2025 kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 ni makubaliano ya mwelekeo kiuchumi na kijamii uliopata ridhaa ya wananchi wote. Kinyume na ilivyokuwa katika mpango wa pili wa muda mrefu (1980 – 2000), ambapo kulikuwapo na mipango ya pamoja na maendeleo ya miaka mitano, utekelezaji wa Dira ya Taifa ya maendeleo 2025 unazingatia zaidi mazingira na muundo wa sehemu husika.

Kwa upande wa Tanzania Bara, Dira hutekelezwa kupitia Mpango wa muda wa kati *(MTP)* wa miaka mitatu mitatu. Mikakati na programu mbalimbali zimeandaliwa ili kutekeleza dira kama vile MKUKUTA, Mpango wa Kuhakikisha maendeleo (*Tanzania mini – tiger plan 2020),* n.k. Aidha, kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 iliandaliwa ili kufikia malengo na dhamira kuu ya kulikomboa taifa kutoka nchi maskini kwenda nchi za kati kimapato pamoja na kuwa na maisha bora. Mkakati wa kupunguza umaskini Zanzibar (MKUZA), miradi ya *SELF, TASAF, EPZ, SEZ* na programu nyingine mbalimbali ni nyenzo zinazohakikisha kuwa malengo hayo yanafikiwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni vyema kuwepo kwa mipango ya muda wa kati ya pamoja na maendeleo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani Bara na Zanzibar kama ilivyokuwa awali kwa kuzingatia muundo wa kiuchumi na kijamii wa sehemu mbili hizi.

Kuhusu suala la utata kwa wahisani, naomba ieleweke kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina ushirikiano na maelewano ya karibu na wahisani na hivyo hakuna utata uliopo kwani wahisani wanayo miradi mbalimbali ya kimaendeleo katika Tanzania Zanzibar na hakuna utata wowote uliojitokeza.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya maendeleo katika nchi hii ina taratibu zake zinazofuatwa. Hivyo ahadi za Mheshimiwa Rais, alizozitoa katika hotuba yake ya tarehe 30/12/2005 juu ya kuchangia maendeleo ya uchumi wa wananchi wa Tanzania Zanzibar zitatekelezwa kupitia Bajeti za sekta mbalimbali ambazo ahadi hizo zinahusu.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kama hii ndiyo hali halisi ilivyo kwamba hakuna utata ambayo kweli tunakubaliana kwamba hakuna na tunayaona. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuniambia kwamba kwa

maana hii inaweza kuwa Tanzania iko tayari kuifanya Zanzibar kuwa sehemu moja ya *very special economic zone* kwa ajili ya Tanzania nzima?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya *SEZ* ni maeneo yanayoibuliwa katika Mikoa mbalimbali kufuatana na mazingira na hali ilivyo katika maeneo hayo. Lakini vile vile yanaibuliwa kushirikiana na uongozi wa sehemu au Mikoa mbalimbali pamoja na taasisi kwa mfano *TCCIA, TNBC* na kadhalika.

Vile vile wakishirikiana na kituo chetu cha uwekezaji. Kwa hiyo, namsihi Mheshimiwa Mbunge, achangamkie suala hili katika maeneo yake na kushirikisha taasisi ambazo nimezitaja hapa kama wanataka kuibua maeneo ya *SEZ*. (*Makofi*)

Na. 368

**Mpango wa Mkoa wa Ruvuma**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa akina mama wa Mkoa wa Ruvuma wana hisia kuwa, rasilimali za taifa zimewekezwa kwa upendeleo na hasa walipoona kuwa Mkoa wa Ruvuma haumo katika mpango wa maeneo maalumu ya uwekezaji (*special economic zones*) ambao vigezo vya utendaji wake viko wazi (*measurable indicators of performance evaluation):-*

(a) Je, ili kuondoa dhana hiyo ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, Serikali haioni umuhimu wa kuwaeleza bayana juu ya mipango muhimu iliyotayarishwa kwa ajili ya Mkoa wa Ruvuma ili waweze kuifuatilia na kufaidika na mipango hiyo?

(b) Je, wananchi wa Ruvuma wanaweza kupata mikakati ya uendelezaji wa Bonde la Ziwa Nyasa hatua kwa awamu hii ya nne ili kupima mafanikio?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO NA UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Awali ya yote naomba kutoa ufafanuzi kuhusu hisia ya akina mama Mkoa wa Ruvuma kuona kwamba Mkoa wa Ruvuma haumo katika Mpango wa Maeneo Maalum ya uwekezaji rasilimali *(special economic zones).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipowasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya kuanzisha maeneo maalum ya Uwekezaji Rasilimali, *(Special Economic Zones Act)* tarehe 15 Februari, 2006, nilieleza kuwa wakati wa kutayarisha mpango maalum wa kuhakikisha maendeleo ya Tanzania *(Tanzania mini- tiger plan 2020)* watalaam wetu wakishirikiana na watalaamu kutoka (*Japan Development institute*) walitembelea baadhi

ya Mikoa na Zanzibar ili kubaini fursa ambazo zinaweza kuvutia wawekezaji.

Kwa ujumla Mikoa ilionyesha utayarisha mkubwa na fursa nyingi zilidhihirika katika sekta za kilimo, ufugaji, misitu, uvuvi, madini, viwanda, utalii na teknolojia ya habari na mawasiliano. Kutokana na maelezo haya ni wazi kwamba Mikoa yote ukiwemo Ruvuma inazo fursa zilinabainishwa katika kuanzisha *SEZs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilielekeza pia kwamba ni muhimu Mikoa, Wizara na Taasisi mbalimbali zibainishe fursa na aina ya maeneo maalum yanayofaa kuendelezwa na kuyatenga ili kuvutia wawekezaji hususan kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Rasilimali (*TIC*) kupitia *Regional Investors Forum* kama ambavyo baadhi ya Mikoa imekwishafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa ufafanuzi huo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mbunge wa Viti Maalumu, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mkoa wa Ruvuma kimeandaa na kutenga maeneo maalum ya kuvutia wawekezaji katika sekta mbalimbali Mkoani Ruvuma.

Maeneo hayo yamewekwa katika hazina ya ardhi *(Land Bank)* kwa ajili ya kuvutia wawekezaji. Kwa hivi sasa fursa katika maeneo hayo imewekwa katika matangazo mbalimbali ya kituo ikiwemo majarida na tovuti. Aidha, *TIC* imeanza mazungumzo na uongozi wa Mkoa wa Ruvuma ili kufanikisha Kongomano la Uwekezaji Mkoani Ruvuma baadaye mwakani ambapo mpango kabambe wa kuvutia wawekezaji pamoja na fursa za uwekezaji zitaainishwa. Tayari kituo kimeanza matayarisho ya kumpata mtaalamu wa kuandaa mchanganuo wa vivutio katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati niliyoitaja hapo juu, pia upo Mpango wa Maendeleo wa Ukanda wa Mtwara (*Mtwara Development Corridor*) ambao unashirikisha miradi ya ujenzi wa barabara kutoka Mtwara hadi *Mbamba Bay,* Peramiho – Mbinga, Daraja la Umoja (mitimoni) na Kivuko katika Ziwa Nyasa kati ya *Mbamba Bay* (Tanzania) na *Nkhata Bay* (Malawi). Mpango huu una lengo la kuchochea maendeleo ya haraka ya kiuchumi kwa ukanda wa Kusini ambao unajumuisha pia Mkoa wa Ruvuma. (*Makofi*)

Katika Mkoa wa Ruvuma, Bonde la Ziwa Nyasa linajumuisha Wilaya ya Mbinga na Songea. Mikakati ya uendelezaji wa bonde hilo katika Wilaya hizi unajumuisha kilimo kikiwemo cha umwagiliaji miundombinu, utunzaji wa mazingira kwa kuhifadhi misitu na vyanzo vya maji na kadhalika. (*Makofi*)

Aidha, miradi mingi ya kilimo inatekelezwa kwa kupitia mipango ya Wilaya ya Kuendeleza Kilimo (*District Agricultural Development Plans (DADP).* Katika Mkoa wa Ruvuma maeneo yaliyoendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji ni Lundo, Litumbadyosi na Nakahuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika kuendeleza teknolojia za umwagiliaji maeneo ya Ngindo, Mkalachi na Ngingama katika Wilaya ya Mbinga yanaendelezwa. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma umedhihirisha kuwa kuna fursa katika kuzalisha mazao ya kilimo na chakula kwanza kuna mvua za kutosha zisizochenga, pili, kuna mabonde na mito inayofaa katika kilimo cha umwagiliaji na tatu kuna Mbuga kubwa ya hifadhi za wanyama *Selous* na mapito ya wanyama kutoka katika Mbuga za Msumbiji.

Je, Serikali inaweza kufikiria uamuzi wake wa kutouweka Mkoa wa Ruvuma katika mpango huu wa *SEZ*? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mkoa wa Ruvuma ni Mkoa ambao unachangia kwa hali ya juu sana uchumi wa Taifa hili na tunajua kwamba uko katika *The big five*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *SEZ* kama nilivyojibu swali lililotangulia ni kwamba ni lazima kwanza wana Mkoa mchakarike katika kuainisha maeneo haya na hata kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba *TIC* walishatuma timu na zilipita katika mikoa mbalimbali na kuainisha maeneo ambayo yanaweza kuanzishwa *SEZ*. Kama nilivyojibu katika jibu langu kwamba tayari wako katika mchakato wa kuanzisha *investors forum* baadaye mwaka huu ili maeneo hayo yaweze kuainishwa na kujua waanze vipi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nina mshauri Mheshimiwa Mbunge Vita Kawawa pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma waweze kuchangamkia utayarishaji wa kongamano hili la *investors forum* ili maeneo hayo yaweze kuainishwa na baadaye kuweza kuanzisha *SEZ* kama ambavyo wameshaanza Mikoa mingine na ili waweze kuchangia uchumi wa Ruvuma pamoja na uchumi wa nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnaona tunakwenda haraka kidogo leo tuna maswali mengi kuliko idadi ya siku zingine.

Na. 369

**Management ya Fukwe za Bahari**

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, sehemu kubwa ya Jimbo la Kigamboni, limefunikwa na Ufukwe wa Bahari ya Hindi na watu wake kwa kiwango kikubwa wanategemea uvuvi, lakini Jimbo hilo limekabiliwa na uanzishwaji wa Hoteli za Kitalii.

Je, Serikali inasimamia vipi maeneo hayo ili kuona kwamba Sheria na Kanuni za kumiliki fukwe zinafuatwa?

(a) Je, Serikali inawachukulia hatua gani wamiliki wa hoteli na wengine ambao wameweka uzio hadi baharini au karibu na bahari na kufanya wananchi washindwe kupita hasa maji yanapojaa ikizingatiwa kuwa ufukwe ni matumizi ya wote?

(b) Je, ni umbali gani unaotakiwa uachwe wazi baina ya eneo la juu na bahari?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** ajilibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Msomi Mbunge wa Kigamboni lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inazo Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia mazingira ya maeneo ya fukwe za Maziwa na Bahari. Sheria zinazosimamia uendelezaji wa maeneo ya Fukwe ni pamoja na Sheria ya Ardhi Sura Na. 113, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004; Sheria ya Usimamizi wa Maeneo ya Wazi Sura Na. 320 na Sheria ya Mipango Miji na Vijiji Sura Na. 378 ya mwaka 1956.

Kwa kuzingatia Sheria hizo, viwanja vya Hoteli na matumzi mengine vilivyoko kwenye fukwe vinapimwa, vinamilikishwa kwa waombaji, vinaandaliwa vibali vya ujenzi na kuendelezwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Sheria. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji wa michoro ya mipango Miji huzingatia maelekezo yaliyomo kwenye Tangazo la Serikali Na. 76 la tarehe 22 Mei, 1992. Tangazo hilo linaelekeza kuwa, kila mara inapoandaliwa mipango ya kuendeleza ardhi inayopakana na ufukwe wa bahari, hapana budi ukanda wa mita 60 unatakiwa uachwe wazi.

Aidha, inapotokea wamilikiwa wa Hoteli na majengo wanajenga bila kufuata Sheria, kanuni na taratibu, Serikali iwachukulie hatua za kisheria kwa ukiukwaji huo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji na Vijiji Sura Na. 378 na Tangazo la Serikali Na. 76 la tarehe 22 Mei, 1992 na kwa kuzingatia sehemu ya maelezo ya jibu la sehemu (b) hapo juu, uendelezaji wa maeneo yanayopakana na ufukwe wa bahari unatakiwa utekelezwe kwa kuacha wazi eneo la mita 60 kwa fukwe za bahari na mita 30 kwa fukwe za Maziwa.

Hata hivyo, uendelezaji katika fukwe unaweza kufanywa jirani kabisa na maji endapo uendelezaji huo ni kwa ajili ya shughuli zinazoendana na maji *(water related activities).*

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Ahsante Mwenyekiti. Kwa kuwa hivi sasa kuna unyanyasi mkubwa katika fukwe hizi zilizopo Tarafa ya Kigamboni, wananchi wanashindwa kupita baadhi ya maeneo kwa ajili ya shughuli zao za uvuvi, pamoja na

shughuli za kwenda kupumzika katika fukwe hizo. Je, Serikali itachukua hatua gani za haraka na kama alivyokiri kwamba kuna mita 60 ambazo zinahitajika kuachwa kwa ajili ya matumizi ya jamii. Je, kutokana na unyanyasaji huo Serikali itachukua hatua gani?

Swali la pili, katika Kata ya Mji Mwema kuna barabara ya asili imefungwa, ambayo ilikuwa ikiwezesha wananchi wenye uwezo wa magari kwenda kwenye fukwe kwa kutumia magari yao. Barabara hiyo ya asili imefungwa na matajiri wenye maeneo hayo wameanzisha barabara nyingine zinaangukia kwenye vyao kufunga ruhusa ya wananchi kupita hadi kwenye fukwe kwa kutumia gari. Je, tatizo hilo pia Serikali inasemaje. Hatua gani za haraka zitachukuliwa ili wananchi wapate fursa hiyo ya kutumia fukwe kwa mujibu wa Sheria zilizopo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza hapa kwamba kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya mwaka 99 kifungu Na. 113 na kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na kwa mujibu wa Sheria nyingine inayohusiana na usimamizi wa maeneo yaliyo wazi Kifungu Na. 320 na kwa mujibu wa Sheria nyingine tena ambayo inahusu makazi na vijiji ambayo iko kwenye Sura Na. 378 ya mwaka 56 zinasisitiza kwamba maeneo ya fukwe ni lazima yawe na umbali wa mita 60 kabla ya majengo yanayohusika. Lakini pia inasisitiza kwamba katika maeneo ya fukwe yaliyo kando kando ya maziwa huwa ni mita 30. Lakini msisitizo huu ulifafanuliwa vizuri katika *Government Notice No.76* ambayo ilitangazwa tarehe 22 Mei, 1992. Kwa hiyo, kwa sababu Sheria zipo ni lazima Serikali na wananchi wote kwa mujibu wa Sheria tuzifuate hizo sheria. Sasa kwa hao wakazi ambao wamezuiwa kupita kwenye maeneo hayo ambayo ni haki yao na ni urithi wao, Sheria ni lazima zifuate mkondo wake.

Lakini katika kipengele No. 101 cha maendeleo ya viwanja na vijiji Halmashauri za Miji wamepewa mamlaka ya kusimamia Sheria hizi. Kwa hiyo, kwa jibu hili ambalo nitampa Mheshimiwa Mbunge alipeleke kwenye Halmashauri yake ya Temeke wahakikishe wanazingatia Sheria ambazo zimewekwa na nchi. Kuhusu suala la barabara ambalo limefungwa. Sasa kwa sababu sijui kamili kwamba hii barabara imefungwa kwa vipi. Lakini ninachotaka kusema wawekezaji au hata mmiliki yoyote wa viwanja vinavyoenda mpaka baharini au hata ni kiwanja cha mtu yoyote. Ni lazima Sheria za nchi zizingatiwe na Halmashauri zote nchini zikiwepo Halmashauri za Temeke, Kinondoni na zote zilizoko Dar es Salaam zina wajibu wa kuzingatia Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5 ya mwaka 69 inayofafanua kuhusu usimamizi bora wa Sheria.

**MWENYEKITI:** Nadhani matatizo haya yanafanana na tatizo la Mheshimiwa Rished kule Pangani.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Ahsante Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliagiza kila Wilaya iunde Kamati kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo yao. Na muda huo sasa umekwisha lakini migogoro bado haijakamilika. Na kwa kuwa fukwe za bahari zimepimwa na kutolewa hati miliki kwa kuingilia ile mita 60 katika maeneo ya Pangani. Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kuongeza muda ili Kamati hizi ziendelee kutatua

migogoro hii na ili upate taarifa na vipi Wizara ya Ardhi imetoa hati miliki katika maeneo haya?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kumweleza Mheshimiwa Rished kwamba sina mamlaka ya kuongeza muda wa Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Rais. Mwenye Mamlaka ya kuongeza muda ni Mheshimiwa Rais mwenyewe aliyeunda zile Tume.

Sehemu ya pili ya swali lake kwa yale maeneo ambayo yako yamepimwa katika hifadhi za bahari za fukwe bila kuzingatia sheria ambazo nimezitaja hapa. Nimeeleza wazi kwamba Sheria zinasema wazi kwamba kwenye fukwe za bahari maeneo ya mita 60 hayaruhusiwi kuingizwa kwenye shughuli zozote. Na ilifanywa kwa makusudi ili kulinda maeneo yale na urithi kwa wananchi wote, ili wananchi wanaohusika katika maeneo hayo wasije wakawa watumwa kwa kutokwenda hata kuvua au kukosa mahali popote pa kwenda ziwani au baharini kwa ajili ya shughuli zao. Sheria ndivyo inazungumza hivyo na sisi tuko hapa kwa mujibu wa kusimamia sheria. Kuhusu matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza ni kweli kuna Mabaraza ya Ardhi ambayo yanatakiwa kushughulikia hizo kesi na mpaka sasa hivi katika kipindi cha mwaka uliyopita zaidi ya maamuzi 4,043 yalipelekwa kwenye Mahama za Ardhi ambazo ziko 23. Kwa hiyo, migogoro haiwezi ikaisha siku moja lakini napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya kazi kuhakikisha migogoro hii inapungua na tutahakikisha kwamba haki tunazilinda hasa za wanyonge, ili kuhakikisha kwamba wasije wakawa watumwa katika nchi ambayo wamepewa na Bwana Mungu wao. *(Makofi)*

Na. 370

**Tatizo la Maji Maji wa Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mji wa Chunya ambao ni Makao Makuu ya Wilaya kwa muda mrefu sasa unakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa maji na kwa kuwa tatizo hili limesababisha maisha ya wakazi wa mji huu hususan wanawake kuwa magumu sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulitatua tatizo hilo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba ni vyema kutafuta vyanzo vingine vya maji vinavyoaminika badala ya kutegemea maji kutoka katika kisima kimoja kilichochimbwa mwaka 1938 wakati ambapo wakazi wa mji huu walikuwa 2000 tu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mji wa Chunya una Kata mbili za Itewe na Chokaa zenye jumla ya wakazi wapatao 11,714 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002. Kwa sasa mji una visima virefu vinne lakini vinavyofanya kazi ni viwili tu ambavyo huzalisha jumla ya meta za ujazo 410 kwa siku ukilinganisha na mahitaji halisi ya meta za ujazo 780 kwa siku. Hii ni sawa na asilimia 52 ya mahitaji. Visima viwili vilivyobaki vina uwezo wa kutoa meta za ujao 260 kwa siku lakini havitumiki kwa sababu vinahitaji kusafishwa na kufungwa mitambo ya kusukuma maji. Mtandao wa bomba za kusambaza maji uliopo unaweza kuhudumia wakazi 6,850 tu sawa na asilimia 53. Huduma ya maji mjini Chunya inaendeshwa na Mamlaka ya Maji iliyoanzishwa kisheria chini ya usimamizi wa Bodi ya Maji iliyoteuliwa na Mheshimiwa Waziri wa Maji tarehe 1 Juni, 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ina mpango wa kuongeza upatikanaji wa maji mjini Chunya kutoka meta za ujazo 410 kwa siku mpaka meta za ujazo 670 kwa siku na kukidhi asilimia 85 ya mahitaji ya sasa. Mpango huu utatekelezwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007 na utahusisha kusafisha visima na kununua mitambo ya kusukumia maji katika visima viwili vilivyopo na ambavyo havitumiki kwa sasa mjini Chunya. Halmashauri kwa kupitia Bajeti yake ya maendeleo ya mwaka 2006/2007 imetenga shilingi 7,000,000/= kwa ajili ya kununua mtambo wa kusukumia maji, na kwa kupitia mfuko wa *Local Government Development Grant* imetenga shilingi 40,000,000/= kama ruzuku kwa Mamlaka ya Maji Mjini Chunya ambayo itatumika katika kukamilisha kazi zilizobaki ili visima vyote viwili viweze kutumika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wa Chunya umeingizwa katika Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini itakayoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2006/2007. Mojawapo ya kazi zitakazofanyika ni utafiti wa vyanzo vya maji kwa matumizi ya wakazi wa mji wa Chunya na kupendekeza hatua sahihi za kuchukuliwa katika kuboresha huduma ya maji mjini Chunya.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii Mheshimiwa Mwenyekiti na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na fasaha. Nina swali moja dogo sana la nyongeza. Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema Serikali ina mpango wa kuboresha huduma ya maji mjini Chunya kwa kutumia *Local Government Grant.* Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imeshindwa kupata ruzuku hiyo kwa sababu ya utendaji mbaya wa mwaka jana. Je, Mheshimiwa Waziri atafikiria njia zingine za kuisaidia Wilaya hiyo badala ya hiyo *Local Government Grant?*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja pia na wananchi wa Wilaya ya Chunya, wafahamu kwamba Wizara ya Maji tuko makini katika kuwapa huduma ya maji. Napenda kumfahamisha ya kwamba kwa kipindi cha awamu hii katika Wilaya ya Chunya ambayo ina majimbo mawili la Lupa na Songwe. Kwa upande wa Lupa kuna vijiji vifuatavyo ambavyo vyote vitahudumiwa vitapata maji kikiwemo kijiji cha Kiwanja, Chunya Mjini, Makongorosi, Lupa, Lualage na Sangawama. Hali kadhalika na Songwe pia vijiji vinne na vyenyewe vitapata huduma ya maji ambapo miradi hiyo itagharimu karibu takriban shilingi bilioni 2 kwa kipindi cha awamu hii ya mwaka 2006/2007 na miradi hiyo tunategemea ikamilike mwaka 2008/2009.

Na. 371

**Miundombinu ya Maji Taka**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Jiji la Dar es Salaam hasa katika mitaa ya Kariakoo kunafanyika ukarabati mkubwa wa miundombinu ya maji taka ili kuliweka Jiji katika hali ya usafi na kudhibiti maradhi ya mlipuko na kwa kuwa, Mkandarasi hulazimika kuchimba barabara ambazo tayari zimeshajengwa kwa lami, na baada ya kukamilisha kazi katika eneo moja, Mkandarasi hujaza kifusi peke yake katika eneo lililochimbwa na hivyo kuharibu mtandao wa barabara za Jiji:-

(a) Je, ni nani anayepaswa kurejesha lami katika barabara hizo baada ya kazi kwisha?

(b) Je, kwa nini hadi sasa utaratibu wa kurudisha lami katika barabara hizo haujaanza, na ni lini kazi hiyo itaanza ili kuondoa usumbufu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Kazi ya ukarabati wa miundombinu ya majitaka inayotekelezwa na Mkandarasi *M/S China Electric Power and Technology Import and Export Corporation (CETIC)* ni sehemu ya mradi wa kukarabati miundombinu ya majisafi na majitaka Dar es Salaam. Urejeshaji wa lami katika barabara zilizochimbwa wakati wa ulazaji wa mabomba ya majitaka unafanywa na Mkandarasi kwa mujibu wa mkataba na kugharamiwa na mradi wenyewe.

(b) Kazi hiyo ya kurejesha barabara katika hali ya kawaida ilianza mapema mwezi Juni, 2006 katika mitaa ya Mkwepu, Samora na Makunganya. Kazi ilichelewa kuanza kwa sababu ya mvua iliyokuwa ikinyesha. Kazi hii inaendelea katika maeneo mengine mwezi huu. Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo ya Kariakoo ambako kutakuwa

na kazi mpya ya kulaza mabomba na kujenga chemba kwa ajili ya kuunganisha wateja wapya kwenye mtandao wa majitaka. Kazi hiyo itakapokamilika barabara za maeneo husika nazo zitarejeshwa katika hali yake ya kawaida.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba nimwulize swali la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa sababu kazi hii inayofanywa ni ya muhimu sana. Lakini ukizingatia mazingira yanakuwepo wakati zoezi linaendelea kwa sehemu ya majitaka basi muda mrefu kumekuwa kuna mashimo yako wazi na wakati wa kutengeneza basi yanatengenezwa bila ya lami. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kazi hii huchukua muda mrefu kwa kisingizio cha mvua haoni kwamba ni usumbufu kwa watumiaji wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye jibu la awali kwamba ucheleweshwaji huo ulitokana na mvua lakini hata hivyo ili kazi iwe mzuri na kazi iwe ya kudumu inabidi kwamba wamalize kwanza mtandao mzima wa barabara hizo na baada ya hapo ndiyo waanze kufukia na katika kufukia huko kutafukiwa kwa aina mbili. Kufukia kwa kwanza watafukia kwa kushindilia changarawe na udongo halafu baadaye ndiyo watakuja kurudishia lami. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira baadaye kazi hiyo itakuwa imara na barabara zitarudi katika hali yake ya kawaida.

Na. 372

**Mabaharia wa Kizanzibar**

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa mabaharia wa Kizanzibar wenye vitambulisho vya kibaharia kutoka Zanzibar *(Seamen's Discharge Book issued in Zanzibar)* hulazimika kubadilisha vitambulisho vyao na kupatiwa vile vya Jamhuri ya Mungano, ambayo ni mwanachama wake huruhusiwa kufanya kazi katika meli za kimataifa *(Foreign going vessles)* kwa sababu Tanzania imekamilisha masharti yote na kuwa katika *IMO White list.*

Je, ni masharti gani nchini hulazimika ili kuingizwa katika *IMO White list* na nini faida na hasara zake?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, naomba kwanza kutoa maelezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaharia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanapokuwa wanafanya kazi kwenye meli za kimataifa *(foreign going vessesls)*

hutambulika kwa utaifa wao. Utaifa wa baharia hutambuliwa kwa kuonyesha *Seaman's Records Book and Identity Document.* Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia mkataba ulioanzisha *IMO* na mikataba mingine iliyowekwa na jumuia hiyo ya kimataifa ikiwemo ile iliyowekewa viwango vya mafunzo ya mabaharia *(Standards of Training Certifications and Watch keeping for Seafarers-STCW 1978 as amended).* Nchi wanachama wa *IMO* ambazo zinakidhi matakwa ya mkataba wa viwango vya ubora wa mafunzo huorodheshwa katika orodha ijulikanayo kama *IMO White List.* Nchi mwanachama wa mkataba huu haina budi kutekeleza viwango vya kiufundi, kiutawala ukaguzi na wataalam wa masuala ya bahari kama vilivyoelekezwa kwenye mikataba hiyo. Tanzania iliingizwa kwenye *IMO White List* tarehe 29/5/2003 baada ya kukidhi kikamilifu matakwa niliyoyaeleza hapo juu. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kama ifuatavyo:-

Masharti ambayo nchi inatakiwa kukamilisha kabla ya kuingia katika *IMO White List* ni pamoja na nchi husika kuwa:-

Mwanachama wa *IMO*

Kuwa imeridhia mkataba wa *STCW 78* kama ulivyorejewa 1995 na kuutekeleza ipasavyo. Kuwa na Sheria inayosimamia usafiri wa majini na

Kuwa na Mamlaka (*Administration)* inayosimamia viwango vya kifundi, kiutawala, ukaguzi na wataalamu wa masuala ya bahari.

Faida za nchi kuwepo kwenye *IMO White List* ni kama ifuatavyo:-

Mabaharia wanaohitimu kwenye Chuo chetu wanakubaliwa kufanya kazi kwenye meli za kimataifa *(Foreign going vessels)* hivyo kupanua wigo wa ajira kwa Watanzania na

Pili, elimu inayotolewa na Chuo chetu cha Bahari *(DMI)* inatambuliwa kimataifa na hivyo vyeti vinavyotolewa kwa wahitimu wa Chuo hicho kukubalika mahali popote katika sekta ya usafiri wa majini duniani kote na hivyo kuvutia wanafunzi kutoka nchi mbalimbali kusajiliwa kusoma katika chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio rahisi kubaini hasara ya moja kwa moja inayotokana na Tanzania kuingizwa kwenye *IMO White List* kwa kuzingatia faida kuu zilizotajwa katika jibu la sehemu ya kwanza ya swali hili.

**MHE. MOHAMED H.J. MNYAA:** Ahsante sana, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Zanzibar sasa hivi ina sheria yake, na kwa kuwa sheria hiyo inakidhi masharti yote ya *IMO* na kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa *IMO.* Je, atakubaliana na mimi Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa Zanzibar *discharge book* zinazotolewa zikubalike kwa vile Tanzania ni mwanachama wa *IMO* ili kuondoa hii sitafahamu kwamba upande mmoja unakandamizwa na upande mwingine wa Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Zanzibar ina sheria hiyo aliyoitaja lakini kama nilivyosema ili uweze kuingizwa katika *list* ya *IMO White List* inabidi nchi husika izingatie vigezo ambavyo nilivyoviweka. Mojawapo ambavyo nilivisema ni kwamba lazima nchi iwe na mamlaka au *administration* inayosimamia viwango vya kiufundi, kiutawala, ukaguzi wa wataalam wa masuala ya bahari. Sasa hilo halijafanyika kwa upande wa Zanzibar na sasa hivi ndiyo kuna huo mvutano kwamba *SUMATRA* waanze kumaliza shughuli zao Zanzibar ili Zanzibar iweke utaratibu wa kuanzisha mamlaka hayo.

Kwa hiyo, ni sharti mojawapo. Kwa hiyo, kuwa na Sheria haitoshi hadi mamlaka hayo yatakapowekwa. Kwa hiyo, nadhani baada ya utaratibu huo wa Zanzibar kuwa na mamlaka yake hilo ulilolisema linaweza likafanyika.

Na. 377

**Barabara ya Kyaka – Karagwe – Benaco**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Kyaka-Karagwe-Benaco ndiyo barabara pekee inayotumika kwa usafiri wa abiria na mizigo na hasa mazao ya chakula na kwa kuwa, barabara hiyo ni korofi sana kwa miaka mingi na Serikali ya Awamu ya Nne iliahidi kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kujenga barabara hiyo?

(b) Je, ni hatua zipi ambazo zimechukuliwa ili kuhakikisha barabara hiyo inajengwa katika mwaka wa fedha 2005/2006?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Barabara ya kutoka Kyaka – Bugene (Karagwe) hadi Kasulo (eneo la Benaco) ni barabara ya Mkoa na ina jumla ya urefu wa kilometa 178 ambapo kati ya hizo, kilometa 10 kutoka Nyakahanga hospitalini hadi Omugakorongo ni za lami nyepesi *(Otta Seal)* na kilometa 168 ni za kiwango cha changarawe.Wizara yangu inatambua umuhimu wa barabara hiyo na imekuwa ikiifanyia matengenezo ili kuhakikisha kuwa inakuwa katika hali nzuri muda wote kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha wa 1996/1997 barabara hii ilifanyiwa matengenezo makubwa kupitia mradi wa *Core Rural Roads Rehabilitation Project (CRRRP).* Matengenezo hayo yaligharimu jumla ya shilingi milioni 791.639. Baada ya matengenezo hayo makubwa barabara hiyo imeendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida na ya sehemu korofi kuanzia 2002/2003 hadi 2004/2005 kwa jumla ya shilingi 253.34

milioni. Aidha, katika mwaka wa fedha 2004/2005 na 2005/2006 jumla ya shilingi milioni 834.9 zilitumika kukamilisha mradi wa lami nyepesi *(Otta Seal)* kwenye sehemu ya Nyakahanga-Omugakorongo (Kilometa 10).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hiyo ili iweze kupitika katika muda wote wa mwaka. Wizara yangu kwa mwaka huu wa fedha 2006/2007 imetenga jumla ya shilingi milioni 152.76 ili kuendelea kuifanyia matengenezo ya kawaida na ya sehemu korofi barabara hii.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi wa Karagwe kwamba barabara hii ya Kyaka-Karagwe Mjini itajengwa kwa kiwango cha lami. Je, Serikali ina mkakati gani kuijenga barabara hiyo katika kiwango cha lami ndani ya miaka mitano ya Awamu ya Nne? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA);** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne imejizatiti sana kutekeleza ahadi zote ambazo alizitoa Mheshimiwa Rais na hivi sasa tunachambua ahadi zote hizo na zinaanza kutekelezwa kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha. Kwa sasa wakati ambapo Bajeti haijatosheleza kutengeneza barabara zote alizoahidi Mheshimiwa Rais kujengwa kwa lami tutaendelea kuziimarisha kwa kiwango cha changarawe kama ambavyo tunafanya kwa barabara hii.

Na. 374

**Barabara ya Tabora – Rungwa**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Tabora – Sikonge – Ipole - Rungwa ilitengewa fedha na mkandarasi *Badr East Africa* alianza kufanya kazi mwaka 2005 na kuvunjiwa mkataba baada ya kukiuka masharti kwa kufanya kazi kwa kasi ndogo:-

(a) Je, Serikali itamaliza lini kilio cha wananchi wa Tarafa ya Kiwere kwa kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba eneo lililotengenezwa kuanzia Rungwa halina maana kwa sababu eneo kubwa halikuunganishwa na kuifanya barabara hiyo kutopitika hasa nyakati za mvua za masika?

(c) Je, ni mkandarasi gani mbadala ameteuliwa kumalizia kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said

Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Ipole – Rungwa yenye urefu wa kilometa 172 ipo katika hali mbaya kiasi kwamba kila ifikapo wakati wa masika huwa inajifunga.

Kutokana na hali hiyo barabara hii ilikuwa miongoni mwa barabara zilizokuwa kwenye mpango wa matengenezo ya barabara kuu zilizoathirika sana na mvua za *El-Nino* za mwaka 1997/1998. Barabara hii ilikuwa itengenezwe kiasi cha kilometa 80 kati ya Ipole na Rungwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.12 kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).*

Kwa bahati mbaya utekelezaji wa mradi huu haukuwa mzuri kwani ni kiasi cha kilometa 15 tu kutoka Rungwa kilitengenezwa kutokana na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* kufunga ufadhili wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya *ADB* kufunga ufadhili wa mradi huu, juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanyika ili kuzifanyia matengenezo kilometa zilizobaki ili barabara hii iweze kupitika kwa wakati wote bila shida pamoja na ufinyu uliopo wa fedha za matengenezo kutoka Mfuko wa Barabara. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 kiasi cha kilometa 15 kilifanyiwa ukarabati kwa gharama ya shilingi 110 milioni.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2005/2006 daraja la Kululu lenye urefu wa mita 12 lilijengwa upya kwa gharama ya shilingi 65.2 milioni. Pia kilometa nyingine 8 zimekarabatiwa kwa gharama ya shilingi 97 milioni. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali imetenga kiasi cha shilingi 65.17 milioni kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Mlolwa lenye urefu wa mita 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inayo nia thabiti ya kuwaondolea kero ya usafiri wananchi wa Tarafa ya Kiwele kwa kuifanyia matengenezo barabara ya Ipole – Rungwa ili iweze kupitika nyakati zote. *(Makofi)*

Tatizo lililopo ni ufinyu wa Bajeti ya matengenezo ya barabara. Wizara yangu inaendelea kutafuta fedha za kutengeneza barabara husika na mwaka ujao wa fedha wa 2007/2008 tutatenga fedha za maendeleo kukidhi mahitaji ya matengenezo kama tulivyofanya mwaka huu wa fedha kwa kutenga shilingi milioni 600 kwa barabara nyingine ya Ipole – Koga ambayo nayo haikukamilishwa na Mkandarasi *Badr East Africa.*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, si kweli kwamba eneo lililotengenezwa kuanzia Rungwa halina maana kwani eneo hili lililofanyiwa matengenezo tayari

limeshapunguza gharama ya kuifanyia matengenezo barabara yote yenye urefu wa kilometa 172 na hivi sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya sehemu iliyobaki.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi wa kumalizia matengenezo ya barabara hii atateuliwa mara baada ya kupata fedha za kukamilisha matengenezo ya barabara hiyo.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Kanuni hairuhusu kuondoa shilingi katika kipindi cha maswali. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-
Kwa kuwa mgao wa fedha za barabara kuu kwenye Bajeti hauna uwiano, jambo linalosababisha baadhi ya barabara kuu nchini kupata mabilioni ya fedha na nyingine kupata fedha za matengenezo zisizokidhi kabisa kabisa matengenezo ya baadhi ya barabara nchini ikiwemo ile barabara ya Ipole-Rungwa.

Je, sasa Serikali iko tayari kutoa tamko hapa Bungeni kwamba itahakikisha barabara kuu zote nchini zinapitika kwa muda wote hata kwa kiwango cha changarawe ikiwemo barabara ya Ipole-Rungwa? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa adha kwa wananchi wa Tarafa ya Kiwele inayosababishwa na kutokupita kwa barabara hii hasa nyakati za masika na kiangazi kupita mbugani kuiacha barabara kwa sababu ina mahandaki na siyo mashimo?

Je, Waziri yuko tayari kufika na kuwa kiongozi wa kwanza wa Awamu ya Nne ukiwaacha Mheshimiwa Mzee Jumbe, Mzee Malecela na Mheshimiwa Dr. Salum Ahmed Salum, waliowahi kufika na kupita kwenye barabara hii, ukiwaacha hao uko tayari kufika na kuona maeneo korofi na kuyabaini na kuelekeza maeneo ya matengenezo makubwa ili barabara hii iweze kupitika masika na kiangazi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umaskini wa nchi yetu na ukosefu wa fedha hatuwezi kutegemea kwamba barabara zote kuu tutazitengeneza kwa wakati mmoja.

Lakini ni kweli kwamba ili tuweze kutekeleza miradi hii itabidi tuende mradi mmoja mmoja na barabara hizi kuu ambazo zinajengwa kwa lami zina gharama kubwa. Kwa hiyo, kwa mwaka mmoja utaona kwamba barabara moja imechukua fedha nyingi sana lakini muda utakapofika wa kujenga barabara nyingine kwa lami, mabilioni vile vile yatakwenda kule, na itaonekana kule pamependelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa hili ni kutokana na umaskini wetu. Nataka nimhakikishie kwamba kama alivyosema, sisi tutahakikisha kwamba barabara zote ambazo hatujaweza kupata fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Dar es Salaam tunazikarabati ili ziweze kupitika. Naelewa barabara anayozungumzia ina hali mbaya na sisi ahadi yetu ni hiyo hiyo kuhakikisha kwamba inapitika kwa mwaka wote. (*Makofi*)

Kuhusu kufika, kama nilivyomwahidi nje ya Bunge, tutakwenda pamoja na yeye tukiandamana na watalaam wa *TANROADS* pamoja na *TANROADS* Meneja Mkoa wa Tabora, ili kuangalia barabara hiyo na kuweka msisitizo wa papo kwa papo.

Na. 375

**Mradi wa Kuendeleza Gesi ya Mnazi Bay kwa Kuzalisha Umeme.**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kazi ya upatikanaji wa gesi kutoka *Mnazi Bay* kwa ajili ya kuzalisha umeme inaendelea kwa sasa na kwa kuwa umeme utakaopatikana kwa mradi huo ndio tegemeo kuu la kuondoa tatizo la upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

(a) Je, Serikali inaweza kuwaarifu wananchi ni lini mradi huo utafikisha umeme mjini Masasi?

(b) Je, kuna mpango gani wa kusambaza umeme huu katika vijiji ambavyo njia za kusambaza umeme (*transmission line)* zitapita?

(c) Je, kampuni gani kati ya *TANESCO* na *ARTUMAS* itakayofanya kazi ya kusambaza umeme huo na kwa vigezo gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Lindi na Masasi watapata umeme wa gesi ya *Mnazi Bay* mara kazi ya kupanua na kukarabati miundombinu itakapokamilika ambapo makisio ya Mkandarasi ni miezi kumi na miwili baada ya kusaini mikataba.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kumalizika kwa kazi ya kupanua na kukarabati njia za usafirishaji umeme wananchi wengi wataweza kusambaziwa uememe kwa utaratibu sawa na ule uliokuwa unafanywa na *TANESCO.*

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *ARTUMAS*, itaendesha mfumo wote wa umeme kuanzia uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme kwa wateja.

Kwa maana hiyo *TANESCO* haitahusika tena na utoaji wa h uduma ya umeme katika eneo la mradi yaani Mtwara, Lindi na Masasi. Kampuni ya *ARTUMAS* wataingia mkataba wa *Franchise* kwa muda wa miaka ishirini kwa ajili ya kuendesha usafirishaji na usambazaji umeme kwa wateja katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Katika kipindi hicho

*ARTUMAS* watakodi miundombinu ya *TANESCO* na kulipa ada kila mwaka kama watavyokubaliana katika majadiliano.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tarehe 15 Julai, 2006 Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifanya ziara ya ghafla kutembelea mradi huu, na kwa kweli tumetiwa moyo sana sana kwa kasi yake ambayo imewezesha mpaka hivi leo, Waziri wa Nishati na Madini kutangaza humu Bungeni kwamba Mheshimiwa Rais, ameshakubali na kuridhia maendeleo ya mkataba huu.

Sasa swali, Je, ni kwanini Wizara mpaka sasa inachezeshwa danadana na *TANESCO* na *TPDC* ambao mpaka leo hawajakamilisha na hawajatiliana mkataba na *ARTUMAS,* kuna nini?

Pili ni kwamba Je, Wizara hii inatoa kauli gani kuhusu kukamilika kwa mkataba huo na lini utatiwa saini, ilikuwezesha kupata *development licence* na mambo mengine yanayofuata, kama *generation licence*, ama wanasubiri Waziri Mkuu, arudi tena awakabe koo ili waweze kukamilisha mambo haya na wananchi wa Mtwara waweze kupata umeme mwezi ujao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kumhakikishia kwamba hatutakuwa na haja ya Mheshimiwa Waziri kurudi kule tena ili kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumfahamisha kwamba *TANESCO* tayari imeshafikia hatua ya kukubaliana na *terms* za *interim power points agreement* na Wizara yetu imeshakubali kwamba *interim power points agreement* inaweza ikasajiliwa na ningependa kumhakikishia kwamba tunakamilisha taratibu zote ambazo zinatakiwa kuhakikisha kwamba mradi huu utaendelea kama alivyoagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, na ninayo matangazo mengi sana. Kwa hiyo, nitaomba mnisamehe, nitayatangaza haya matangazo kwa *blocks,* sitaweza kutambulisha kama Waheshimiwa Wabunge mlivyoniomba, vinginevyo itatumia karibu nusu saa nzima.

Sasa naomba kwanza niwahataarifu wajumbe wa Kamati ile ya Kanuni kwamba nimeagizwa na Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao cha leo kitafanyika saa saba na nusu na vilevile naomba niwahataarifu wajumbe wa Kamati ya Uongozi, Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Kamati ya Uongozi kutakuwa na kikao cha dharura leo saa nane, mchana kwenye ukumbi wa Spika.

Kwa hiyo, naomba hilo tangazo la kwanza lizingatiwe, lakini naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kwamba kutakuwa na

kikao cha Kamati ya Chama, leo saa saba baada ya kuahirisha Bunge kwenye ukumbi wa zamani.

Naomba niwatangizie Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Shellukindo, anaomba wajumbe hao wakutane leo Jumatano, tarehe 9 saa saba mchana katika ukumbi Na. 432 nafikiri mtashauriana mnakutana saa ngapi, labda baada ya kikao cha chama.

Ninaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Mgana Msindai, anaomba kuwatangazia wajumbe wake kwamba kutakuwa na kikao wao watakifanya leo saa tano hii asubuhi chumba Na. 133, wajumbe wote naomba muhudhurie kikao hicho.

Ninaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo Jumatano tarehe 9 saa nne na nusu na wao wanafanya asubuhi hii, saa nne na nusu, Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati hiyo anaomba wajumbe muhudhurie bila kukosa kikao hicho cha Kamati.

Ninaomba nitambue wageni wa Mheshimiwa Diodorus Kamala, Naibu Waziri ambaye leo na Waziri wake watawasilisha hotuba yao ya Bajeti, leo hapa mbele yetu, Mheshimiwa Naibu Waziri amemleta Mama yake Mzazi Mama Rose Kamala, lakini Mama huyo mzazi ameambatana na Mke wake na watoto wake na mdogo wake. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niendelee kwamba tunao wageni kutoka *Rotary Club*, tawi la hapa Dodoma, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Madeje, lakini wameongozwa na Mwenyekiti, wao Mheshimiwa Francis Mazanda na pia ni Mstahiki Meya wa Mji huu wa Dodoma, lakini wako pia na Mheshimiwa Balozi Job Lusinde na wamekaa kwenye *Speaker Gallaery.* (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge naomba pia mtambue wageni wa Mheshimiwa Shellukindo, hawa ni Wakurugenzi wa *General Tire,* Meneja Mkuu wa *General Tire*, na Mameneja watano wa Kanda wa *General Tire* nao wamekuja kwa ajili ya shughuli rasmi ya ufunguzi wa tawi la *general tire,* naomba na wao pia wasimame kwa umoja wao. (*Makofi*)

Naomba tuwatambue wanafunzi ambao wako mkono wangu wa kushoto pale, wamependeza vizuri watoto wetu wa shule, hao ni wanafunzi wa shule ya sekondari ya Huruma, wakiwa pamoja na walimu wao, naomba tu wasimame tuweze kuwatambua. (*Makofi*)

Naomba pia vilevile nitambue uwepo wa Mheshimiwa Mafudhi, yeye ni Mwenyekiti wa Wabunge wa Afrika Mashariki lakini wanaotokea katika nchi yetu ya Tanzania. Tunao Madiwani 30 kutoka Hanang, ni Waheshimiwa wageni maalum kabisa wa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri na wanaongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. Hivyo, naomba hao Waheshimiwa Madiwani pia wasimame. (*Makofi*)

Ninaomba niwatambue wageni wa Mheshimiwa Stella Manyanya, ambao ni wakurugenzi wa *Peninsula English Medium School*, naomba nao wasimame kwa umoja wao. (*Makofi*)

Naomba pia niwatambue Waheshimiwa Madiwani wa wilaya ya Kati Unguja ambao ni wageni maalum kabisa wa Mheshimiwa Haroub Masoud, na hao wameongozana na Mwenyekiti Diwani Abdallah Makame na Madiwani wengine kwa umoja wao naomba wasimame tuweze kuwatambua. (*Makofi*)

Vilevile naomba niwatambue vijana ambao wako hapa wakihudhuria semina maalum ya MKUKUTA, nayo imeandaliwa na *Youth Partnership something* ambao wako pale *CBE* wakiendelea na mafunzo yao maalum ya MKUKUTA, lakini wageni wa Mheshimiwa Killimbah, Gosbert Blandes, William Ngeleja, Amina Chifupa, Faida Bakari na Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu, naomba vijana hao ambao wamekuja kwenye masuala ya MKUKUTA, naomba tuwatambue karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Zainab Vulu, ambaye atawasilisha leo hotuba ya Kamati ya Wizara husika kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, yeye ameniomba sana nimtambue mume wake, kwa agizo la Spika, ameona atekeleze agizo hilo kwa kumleta mume wake, naomba Mr. Vulu asimame na yeye tuweze kumtambua. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kwenye *Speakers Gallery* tuna wageni wengine ambao wametoka nje ya nchi yetu, baada ya muda tu nikishapata majina yao na utaratibu wao nitawatambulisha rasmi mbele yenu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ikiwa ni hotuba yangu ya kwanza Bungeni baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, awali ya yote napenda kuungana na Mawaziri walionitangulia kutoa pongezi na shukrani zangu kama ifuatavyo:

Kwanza nampongeza kwa dhati, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Makamu wa Rais, Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi huo wa kishindo ni ishara ya imani waliyonayo wananchi kwa Rais na kwa sera sahihi za Chama cha Mapinduzi (CCM). Aidha, nampongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa hivi karibuni kwa kura

karibu zote kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kwake kwa kipindi cha pili kuwa Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge hili kwa kura nyingi kuwa Waziri Mkuu. Pia nawapongeza Mawaziri, Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu pia niwapongeze wabunge wenzangu kwa ushindi walioupata katika majimbo yao na wale wa kuteuliwa, kwa wote kuingia katika Bunge hili Tukufu. Aidha, nakupongeza wewe Mwenyekiti, pamoja na Mwenyekiti mwenzako Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyekiti wetu. Nampongeza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliongoza Bunge hili la Awamu ya Nne. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza Mheshimiwa Johnson Mwanyika kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nafasi ambayo nilibahatika kuishikilia kwa takriban miaka kumi na miwili na nusu hadi mwaka jana. Ninamtakia kila lililo jema na mafanikio katika wadhifa huo kama na mimi ninavyoamini kuwa na yeye ananitakia mema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bariadi Magharibi kwa heshima waliyonipa kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao. Nina deni kubwa la kuwalipa kwa imani walioonyesha kwangu na ninawaahidi kuwatumikia kwa uwezo wangu wote. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu kwa kuniteua kuwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kuanzishwa kwa Wizara hii mpya na nyeti ni ushahidi tosha wa jinsi Rais wetu anavyolipatia uzito unaostahili suala zima la Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anna Magareth Abdalah, Mbunge wa Viti Maalum, kwa ushauri, maoni na mapendekezo yaliyowezesha kuboresha Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, napenda pia kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri wote waliotangulia kuwasilisha hoja zao hususan, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Mbunge wa Jimbo la Ulanga Magharibi, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Mbunge wa Kuteuliwa pamoja na Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa sera za jumla za uchumi, fedha na utendaji wa Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi na shukrani sasa nizungumzie masuala yanayohusu Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Shughuli za kujenga Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea vizuri. Ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 24 Aprili, 2006 Tanzania imetoa Katibu Mkuu mpya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki naye si mwingine bali ni Mheshimiwa Balozi Juma Volter Mwapachu. Mheshimiwa Balozi Juma Mwapachu amechukua nafasi hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Nuwe Mushega wa Uganda ambaye amemaliza kipindi cha utumishi wake. Kabla ya uteuzi huo Mheshimiwa Juma Mwapachu alikuwa Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi Juma Mwapachu ni mtu mwenye uwezo mkubwa wa kiutendaji, kibiashara na kidiplomasia**.** Mheshimiwa Balozi Mwapachu ni mtu hodari na makini wa kutetea maslahi ya Afrika Mashariki. Tunaamini chini ya uongozi wake Jumuiya ya Afrika Mashariki itaboreka kiutendaji na hadhi yake kimataifa itaongezeka. Naomba, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Juma Volter Mwapachu, kwa kuteuliwa katika wadhifa huo. Tunamtakia kheri na mafanikio katika kazi zake na tunamhakikishia kila aina ya ushirikiano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kama itakavyokumbukwa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliundwa kwa Tamko la Rais tarehe 4 Januari, 2006 ikiwa ni azma ya Serikali katika kutekeleza na kuimarisha usimamizi wa karibu wa majukumu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo Wizara hii ni daraja muhimu katika kuunganisha Serikali na sekta binafsi, wananchi na wadau wengine kwa ujumla kuhusu masuala ya Afrika Mashariki. Aidha, Wizara hii ni mwezeshaji na mratibu mkuu wa Nchi katika usimamizi na utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Treaty*) na Itifaki zake (*Protocols*). Pia Wizara inaratibu na kusimamia ushiriki wa Watanzania katika kutumia fursa ya masoko na uwekezaji inayotolewa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ili wananchi waweze kujiimarisha kiushindani na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kuu la Wizara ya yangu ni kuhakikisha Tanzania inanufaika kwa ukamilifu kutokana na ushiriki wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Dira ya mtangamano (*integration***)** wa Afrika Mashariki ni pamoja na kukuza utajiri, kuinua hali ya maisha ya wananchi wa Afrika Mashariki, kukuza uchumi, na kujenga ushindani wa kanda katika ngazi ya kimataifa. *(Makofi)*

Dira hiyo itafikiwa kwa kuongeza tija na uzalishaji, kwa kuzalisha bidhaa nyingi na bora na kwa kutoa huduma za viwango vya juu kwa ajili ya kuuza katika soko kubwa la ndani na la nje pamoja na kuvutia uwekezaji. Katika kuhakikisha ushiriki madhubuti wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara imepewa kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake;

(ii) Kuratibu na kusimamia Majadiliano yahusuyo ushirikiano wa Afrika Mashariki hususan Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Umoja wa Sarafu na hatimaye Shirikisho;

(iii) Kusimamia na kuratibu shughuli za Idara zinazojitegemea na miradi itakayokuwa chini ya Wizara;

(iv) Kusimamia na kuratibu shughuli za Wakala za Serikali zitakazokuwa chini ya Wizara; na

(v) Kuimarisha utendaji na ujuzi wa wafanyakazi wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Mikakati, ushirikiano wa kikanda ni miongoni mwa nyenzo muhimu katika kukuza na kuendeleza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Hata hivyo faida itokanayo na matumizi ya nyenzo hii inategemea kuwepo kwa sera safi pamoja na mipango madhubuti ya utekelezaji na usimamizi. Kwa hiyo, kisera Wizara yangu inazingatia yafuatayo:

(i) Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Umoja wa Forodha unakuwa chachu na nguzo muhimu katika kujenga uwezo na imani ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kuelekea katika ushirikiano mpana na wa kina zaidi katika siku za usoni;

(ii) Ushiriki wa sekta ya umma na sekta binafsi, taasisi zisizo za kiserikali na wadau wengine katika maamuzi yahusuyo mustakabali wa ushirikiano wetu wa kiuchumi, kijamii na kisiasa;

(iii) Matumizi kamilifu ya fursa za soko kubwa la watu takriban milioni 90 zilizojitokeza katika Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha ili kukuza na kuendeleza mauzo ya ndani ya Afrika Mashariki na nje; (*Makofi*)

(iv) Mikataba na Itifaki kuhusu hatua yoyote ya mtangamano wa Afrika Mashariki itakubaliwa pale tu itakapothibitika kwamba ina maslahi kwa nchi;

(v) Kuhimiza ukamilishaji wa mikataba itakayoimarisha ushirikiano baina ya *EAC* na kanda nyingine za kiuchumi hususan *SADC* na *COMESA* kama ilivyoainishwa katika Itifaki ya Umoja wa Forodha na Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya mwaka 2004;

(vi) Kuhakikisha ushirikishwaji wa Wizara na taasisi nyingine katika kutekeleza masuala mtambuka yahusuyo Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(vii) Uimarishaji uwezo wa Wizara kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, mikakati itakayotumika katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara itazingatia Mkakati wa tatu wa Maendeleo wa Afrika Mashariki (2006 - 2010) ambao ubora wa misingi yake unatokana na utekelezaji wa mkakati wa kwanza (1997 - 2000) na Mkakati wa pili (2001 – 2005) wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu itajielekeza katika mambo yafuatayo:

(a) Kutangaza fursa za masoko zilizoko Kenya na Uganda na kwingineko kwa kutumia vyombo mbalimbali vya habari yakiwemo magazeti, radio na televisheni.

(b) Kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge kutumia mikutano yao na wapiga kura kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kukuza uzalishaji mali nchini ili Tanzania iweze kunufaika na fursa inayotolewa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(c) Kufanya utafiti kuhusu nyanja za ushirikiano kwa lengo la kubaini vikwazo na kubuni mikakati ya kukabiliana navyo.
(d) Kutumia Balozi zetu nchini Kenya na Uganda katika kuwawezesha Watanzania kuendeleza biashara.

(e) Kuwasiliana na Wizara, sekta binafsi na wadau wengine katika kubuni sera, mikakati na programu za utekelezaji katika kukuza na kuendeleza uzalishaji mali na biashara.

(f) Kufanya maandalizi ya kutosha katika majadiliano na Nchi Wanachama.

(g) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake kwa lengo la kubaini mafanikio au mapungufu ya utekelezaji na kuchukua hatua zinazostahili.

(h) Kujifunza kutoka kanda au nchi nyingine jinsi ya kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na ukuaji wa Jumuiya yenyewe.

(i) Kuratibu kwa karibu utekelezaji wa maamuzi mbali mbali ya vyombo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki ukiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge na Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(j) Kuendelea kushawishi Nchi wanachama kuweka mkazo katika masuala yahusuyo maendeleo badala ya biashara pekee, na

(k) Kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya yaAfrika Mashariki, Ushirikiano wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki una historia ndefu iliyoanza hata kabla ya uhuru wa nchi zetu. Nchi za Kenya, Tanzania na Uganda zimekuwa na uhusiano wa karibu wa miaka mingi katika nyanja mbalimbali. Kwa miaka mingi Nchi hizi zimekuwa zikishirikiana kwa sababu Nchi hizi ni majirani; na zinafanya biashara baina yao na watu wake wamekuwa wakisafiri na kutembeleana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuvunjika kwa ile iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, juhudi mpya zilianza kuchukuliwa na Viongozi Wakuu wa nchi

za Tanzania Kenya, na Uganda za kufufua ushirikiano. Juhudi hizo zilipata msukumo mpya pale Viongozi Wakuu wa Nchi za Tanzania Kenya, na Uganda walipokubaliana kufufua ushirikiano wa nchi zetu tatu kwa kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Kamisheni ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Itakumbukwa kwamba Sekretarieti hiyo ilizinduliwa na Marais wa nchi za Kenya, Uganda na Tanzania mjini Arusha tarehe 14 Machi, 1996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makubaliano ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki yalipandishwa hadhi kutoka Makubaliano ya kawaida ***(**Agreement*) na kuwa Mkataba kamili (*Treaty)*. Baada ya mchakato mrefu uliowahusisha wananchi wengi wa Afrika Mashariki wakiwemo, wananchi wa kawaida, makundi maalum kama Wabunge, Wawakilishi, Wanataaluma, Wafanyabiashara n.k, rasimu ya Mkataba huo ilitiwa saini na Wakuu wa Nchi Wanachama, yaani Tanzania, Kenya na Uganda tarehe 30 Novemba, mwaka 1999 mjini Arusha. Itakumbukwa kwamba Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Treaty*) uliridhiwa na Bunge lako tarehe 13 Juni, 2000 kwa kauli moja. Baada ya kuridhiwa na Mabunge ya nchi zetu tatu, Mkataba huo ulianza kutumika rasmi tarehe 7 Julai 2000. Aidha, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilizinduliwa rasmi mjini Arusha tarehe 15 Januari, 2001. *(Makofi)*

Chini ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki Nchi zetu tatu zimekubaliana kushirikiana katika mambo ya siasa, uchumi, huduma za jamii, utafiti, ulinzi, usalama na sheria. Katika ushirikiano huo, kipaumbele kinatolewa katika maendeleo maeneo ya kiuchumi, uchukuzi, mawasiliano, biashara, viwanda, fedha, vitega uchumi, kilimo, mifugo, uvuvi, maliasili, utalii, nishati, mazingira, uhamiaji na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki tunayokusudia kuijenga inatokana na kutambua ukweli kwamba nchi changa kama zetu zenye uchumi dhaifu zinapaswa kuunganisha nguvu ili kukabiliana kikamilifu na hali halisi katika dunia ya leo ya utandawazi. Katika kufanya hivyo siyo tu tunaunganisha uchumi wa nchi zetu lakini pia tunataka kurejesha na kuimarisha historia na sifa yetu mbele ya mataifa mengine kama wana wa Afrika Mashariki. Wahenga walisema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kuunganisha kwa uchumi wa nchi zetu kutatusukuma kuongeza uwezo wa uchumi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kushindana wenyewe kwa wenyewe, na Afrika Mashariki kushindana na dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Customs Union*), baada ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuzinduliwa rasmi tarehe 15 Januari, 2001 hatua mbalimbali za kutekeleza Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki zilianza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoa mchango mkubwa ambao ulitolewa na nchi yetu katika kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ilishiriki kwa karibu sana katika kuanzisha Umoja wa Forodha, ambao kwa mujibu wa Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni hatua muhimu ya kwanza katika kujenga ushirikiano wa Nchi wanachama. Zoezi la kuanzisha Umoja wa Forodha ambalo majadiliano yake yalichukua takriban miaka minne lilifikia kilele tarehe 2 Machi, 2004 pale Viongozi Wakuu wa Nchi zetu tatu walipoweka saini Itifaki ya Umoja huo wa Forodha mjini

Arusha. Itifaki hiyo ya Umoja wa Forodha ilianza kutekelezwa rasmi tangu tarehe 1 Januari, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la msingi la Umoja wa Forodha ni kulifanya eneo la Afrika Mashariki kuwa eneo moja la kibiashara kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki ni miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyokwishafikiwa katika hatua ya awali ya mtangamano ya nchi zetu tatu. Utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha unazingatia mambo yafuatayo:-

(i) Kuwa na mpango wa kuondoleana Ushuru wa Forodha kwa bidhaa zinazozalishwa au kutengenezwa ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuwa na wigo wa pamoja wa Ushuru wa Forodha (*common external tariff*) kwa bidhaa zinazotoka nje ya Jumuiya. Chini ya mpango huu hakutakuwa na ushuru wa forodha kwa bidhaa zitokazo Tanzania na Uganda zinapoingia katika soko la Kenya. Hata hivyo baadhi ya bidhaa kutoka Kenya zitatozwa ushuru wa Forodha zinapoingia katika soko la Tanzania na zinapoingia katika soko la Uganda kwa kipindi cha miaka mitano. Lengo likiwa ni kulinda bidhaa za viwanda vichanga vya Tanzania na Uganda katika kipindi hicho cha mpito. Hata hivyo, ushuru huo utakuwa unapungua taratibu hadi kufikia kiwango cha sifuri (0) ifikapo tarehe 1 Januari 2010. (*Makofi*)

(ii) Kutoza ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bidhaa hizo zimewekewa viwango vitatu ambavyo ni asilimia sifuri (0) kwa malighafi na bidhaa za uzalishaji (*Capital Goods);* asilimia kumi (10) kwa bidhaa za kati *Intermediate Goods*); na asilimia (25) kwa bidhaa zilizokamilika kabisa (*Finished Goods*) tayari kwa kutumika.

(iii) Kuwapo na bidhaa ambazo hazitafutiwa ushuru na kiwango cha ushuru kitakachotozwa kwa bidhaa hizo.

(iv) Kuwapo na kundi la bidhaa kutoka Kenya ambazo hazitatozwa ushuru wowote wa forodha zinapoingia Tanzania au Uganda tangu tarehe ambayo Itifaki ya Umoja wa Forodha ilianza kutumika, yaani tarehe 1 Janauari, 2005.

(v) Kuwapo na kundi la bidhaa nyeti (*Sensitive Products)* Kundi hili linajumuisha bidhaa ambazo kutokana na umuhimu wake kwa uchumi na nchi zinastahili kulindwa dhidi ya ushindani na bidhaa za aina hiyo kutoka nje. Kwa ajili hiyo bidhaa za namna hiyo zitakapoingizwa

(vi) Katika soko la Afrika Mashariki zitatozwa ushuru mkubwa kuliko kiwango cha juu cha asilimia 25.

(vii) Kuwa na kanuni za kutambulisha uasili wa bidhaa (*Rules of Origin*) kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa motisha katika matumizi ya malighafi ipatikanayo katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo kukuza na kuendeleza teknolojia na kuvutia wawekezaji. Madhumuni ya kuwa na kanuni hizi za kutambulisha uasili wa bidhaa ni kuhakikisha kuwa bidhaa zinazopatiwa unafuu wa ushuru ziwe kweli za Afrika Mashariki na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeanza na unaendelea vizuri. Ingawa yamekuwepo matatizo ya hapa na pale ya kisera na kiutendaji hilo siyo jambo la ajabu hasa tukizingatia mapana na marefu ya suala lenyewe na ukweli kwamba Umoja huu wa Forodha bado ni mchanga sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, jambo la kutia moyo ni kwamba pale yalipojitokeza matatizo ya utekelezaji wa Mkataba huo matatizo hayo yamepatiwa ufumbuzi wa haraka na nchi wanachama kupitia vikao halali vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa majadiliano ya kuelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ilikuwa makini sana wakati wa majadiliano ya kuanzisha Umoja wa Forodha. Lengo la Serikali wakati wa mazungumzo kuhusu Umoja wa Forodha lilikuwa ni kuhakikisha kuwa nchi yetu inanufaika na uwanachama wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba hakuna nchi mwanachama wa Jumuiya hiyo ambayo itaumizwa kwa upande wa mapato ya Serikali wala kuathiri viwanda vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuratibu kwa karibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itachukua hatua mahsusi za kufidia pengo katika mapato yake pale itakapoonekana kwamba zoezi la uondoaji wa ushuru katika kipindi cha mpito (*transition period*) cha utekelezaji wa Umoja wa Forodha linaathiri mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji madhubuti wa Umoja wa Forodha utajenga imani kwa wananchi kwamba mtangamano wa nchi zetu unawezekana. Tukifanikiwa vizuri kutekeleza hatua hii muhimu, tuna uhakika na kuendelea na hatua zinazofuata za mtangamano bila matatizo makubwa kwa kuwa msingi imara na endelevu utakuwa umewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuthibitisha hili napenda ninukuu kutoka kwenye Hotuba ya Waziri wa Fedha Mhe. Zakhia Hamdani Meghji wakati akiwasilisha katika Bunge lako Tukufu mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

"Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilianza kutekeleza mfumo wa viwango vya ushuru wa Forodha wa pamoja mwezi Januari, 2005. Katika kipindi cha Julai 2005, hadi Machi 2006, Mapato kutokana na Ushuru wa Forodha yalikuwa asilimia 52 zaidi ya mapato ya kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2004/2005. Huo ni

uthibitisho kwamba, Tanzania ilifanikiwa kulinda mapato yake ipasavyo wakati wa majadiliano ya kuanzisha Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki". Mwisho wa Kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha, Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki pia limepitisha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya mwaka 2004 (*EAC Customs Management Act, 2004*).

Aidha, ili kujenga mazingira mazuri ya ushindani ndani ya Afrika Mashariki, Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuwa na sera moja na sheria itakayosimamia ushindani miongoni mwa wafanyabiashara na watoa huduma katika nchi zetu tatu. Muswada wa sheria hiyo ya ushindani (*East African Community Competition Law*) sasa upo mbele ya Bunge la Afrika Mashariki katika hatua za mwisho. Aidha, Bunge la Afrika Mashariki tayari limekwisha pitisha sheria itakayosimamia ubora wa bidhaa zitakazouzwa katika soko la Afrika Mashariki yaani Sheria ya *The Standards, Quality Assurance, Metrology and Testing Act, 2006.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha ni hatua muhimu sana kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama chombo cha kiuchumi na biashara. Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umetoa fursa ya kukuza na kuendeleza uchumi wa nchi wanachama kwa kufungua mipaka ya nchi zetu na kuwa soko moja kubwa. Serikali, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla tunao wajibu wa kujipanga vizuri kila mmoja kwa nafasi yake, ili tuweze kunufaika na fursa zinazotokana na Tanzania kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla mambo yanakwenda vizuri katika kujenga Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vikao vya Kamati za kisekta na vya asasi mbalimbali za Jumuiya kama vile Bunge la Afrika Mashariki na Mahakama vinafanyika kama vilivyopangwa. Sekretarieti ya Jumuiya inazidi kuimarika kwa kuongezewa watumishi na vitendea kazi kila mara inapojitokeza haja ya kufanya hivyo. Aidha, mipango, programu na miradi mingi ya maendeleo na ushirikiano imebuniwa na mingine ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengi yamepatikana tangu Jumuiya ya Afrika Mashariki ianzishwe. Kutokana na muda sikusudii kuyataja yote. Nitayataja baadhi tu ya mafanikio hayo katika sekta za miundombinu, nishati, elimu, mazingira, maliasili, utalii na mawasiliano. Katika sekta hizo yamefanyika yafuatayo:

Kuwekwa saini kwa Mkataba kuhusu uchukuzi wa barabara (*Tripartite Agremeent on Road Transport*) ambazo lengo lake kuu ni kuwa na mtandao wa barabara imara unaounganisha nchi zetu tatu ili kuimarisha usafiri na uchukuzi baina ya nchi zetu na hivyo kukuza biashara. Mradi wa mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 15,273 unazihusu barabara zifuatazo:

(1)Mombasa - Malaba - Katuna - (Kenya na Uganda). (2) Dar es Salaam - Mutukula - Masaka (Tanzania - Uganda). (3)Biharamulo - Mwanza - Musoma Sirari - Kisumu - Ladwar - Lokichoggio (Tanzania na Kenya). (4) Tunduma - Mbeya -

Iringa - Dodoma - Arusha Namanga – Isiolo – Masabiti – Mayale (Tanzania na Kenya). (5)Nyakanazi - Kasulu - Tunduma (Tanzania**).**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba Waziri wa Miundombunu wakati akiwasilisha bajeti ya Wizara yake, sehemu mbalimbali za mradi huu zimeombewa fedha kutoka kwa wahisani na wahisani wengi wameonyesha nia ya kusaidia utekelezaji wa mradi. Kwa mfano, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* imekubali kufadhili matengenezo ya barabara itokayo Arusha - Namanga hadi *Athi River* kwa upande wa Kenya. Maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo yako katika hatua za mwisho. *Nordic Development Fund* imekubali kugharamia usanifu wa kina wa barabara ya Iringa – Dodoma na kadhalika.

Mpango wa Kuendeleza nishati katika Jumuiya (*East Africa Power Master Plan*). Mpango huu umetayarishwa ili kuhakikisha kuwepo na umeme wa kutosha, wa uhakika na bei nafuu na hivyo kukuza uchumi wa nchi zetu tatu. Taarifa ya mwisho kuhusu mpango huo imekamilika na mapendekezo yake yanasubiri uamuzi wa Serikali za nchi wanachama wa Jumuiya.Itifaki ya kuhifadhi Mazingira na Matumizi endelevu ya maliasili imekamilika na kuwekwa sahihi na nchi wanachama.

Kuanzia Novemba, 2005 Jumuiya ya Afrika Mashariki inatangazwa sasa kama eneo moja la Utalii. Aidha, vigezo vya kuweka viwango vinavyofanana vya hoteli za kitalii na vivutio vingine vimekwisha kukubaliwa na nchi wanachama. Vilevile sasa upo usare katika viwango vya malipo kwa huduma zinazotolewa katika hoteli za kitalii na kwenye mbuga za wanyama katika nchi zote tatu (*Non-discriminatory rates and fees).* (*Makofi*)

(e) Katika ngazi ya Elimu ya Juu (Chuo Kikuu), nchi wanachama zimekubaliana kuhusu mpango wa kubadilishana wanafunzi na kuweka usare katika gharama za malipo kwa wanafunzi wote (*Non-discriminatory fees).* Pia limeundwa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (*Inter-University Council for East Africa*) litakalokuwa na uwakilishi wa vyuo vikuu vyote vya nchi za Afrika Mashariki.

(f) Wafanya biashara wa nchi zetu tatu tayari wameshaunda chombo cha pamoja ambacho kitasaidia kujenga ushirikiano katika nyanja ya biashara. Wafanyabiashara wa Afrika Mashariki katika maamuzi yao wameanzisha Baraza la Wafanya Biashara wa Afrika ya Mashariki (*The East African Business Council).*

(g) Kwa upande wa kuwianisha sera za fedha na bajeti masuala mbalimbali yanaendelea kushughulikiwa.

(h) Utekelezaji wa mradi wa usalama wa usafiri wa anga ambao malengo yake ni kuhuisha kanuni za usafiri wa anga katika nchi wanachama, mafunzo kwa marubani na mainjinia wa ndege, ushirikiano katika sekta ndogo ya usafiri wa anga na kuanzishwa kwa chombo kimoja kitakachosimamia usalama wa usafiri wa anga katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unaendelea vizuri.

(i) Jumuiya ya Afrika Mashariki inashiriki ipasavyo katika utekelezaji wa mradi wa *East African Submarine Cable System (EASSY)* ambao unatekelezwa kwa pamoja na *NEPAD.* Lengo la mradi huu ni kuunganisha Afrika Mashariki na mkonga wa *fibre optic* utakaopita chini ya Bahari ya Hindi toka Mtunzini (*Afrika ya Kusini*) kupitia Maputo, Beira, Dar es Salaam, Zanzibar, Mombasa, Mogadishu, Djibout mpaka *Port Sudan*. Mradi huo utakapokamilika mwambao wa Afrika yote utakuwa umeunganishwa na *fibre optic* na kuwezesha mawasiliano ya haraka na gharama nafuu hadi vijijini.Jumuiya ya Afrika Mashariki inafuatilia na kujihusisha kwa karibu na miradi mbalimbali ya kuhifadhi mazingira na kuboresha uchukuzi na usalama katika Ziwa Victoria. Mradi wa kuboresha uchukuzi na usalama katika Ziwa Victoria (*Lake Victoria Safety and Navigation Study*) umekamilika. Aidha, imeazishwa Tume ya Ziwa Victoria yenye makao makuu yake mjini Kisumu, Kenya ambayo itasimamia maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii katika Ziwa hilo kwa faida ya wakazi wapatoa milioni thelathini wanaoishi kandokando mwa ziwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na kushuka kwa kina cha maji ya Ziwa Victoria, Viongozi Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mkutano wao uliofanyika mjini Arusha mwezi Aprili mwaka huu, walielekeza Jumuiya ya Afrika Mashariki ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini kiini cha tatizo hilo na kutoa mapendekezo ya hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na tatizo hilo. Kwa minajili hiyo Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imepanga kuitisha mkutano wa dharura wa Mawaziri wa nchi wanachama ili kujadili hali hiyo ambayo inatishia upatikanaji wa maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo, viwanda, usafiri wa majini na uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina furahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki imepokea msaada kutoka Serikali ya Uingereza wa meli ndogo ya utafiti ambayo imepewa jina la *RV* Jumuiya. Meli hiyo ambayo ilizinduliwa rasmi hivi karibuni mjini Mwanza na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Juma Mwapachu itatumika kufanya tafiti mbalimbali katika Ziwa Victoria kuhusu usafi na usalama wa maji ya Ziwa, kiwango cha uchafuzi wa mazingira, bioanuai ya Ziwa hilo, kiwango cha utajiri na aina ya samaki waliopo katika Ziwa Victoria pamoja na kina cha maji ya Ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma masuala haya muhimu hayakuweza kushughulikiwa kisayansi kutokana na kutokuwepo na chombo chenye vifaa vya kisasa cha kufanya tafiti mbalimbali katika Ziwa Victoria. Tunaishukuru Serikali ya Uingereza kwa msaada huo ambao umekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kufanikisha utekelezaji na usimamizi wa karibu wa mafanikio hayo na mengine yatakayofuata, yameundwa Mabaraza ya Kisekta ili kurahisisha upatikanaji na ufuatiliaji wa maamuzi katika sekta husika za ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki umeweka bayana hatua zitakazofuatwa katika kujenga na kuimarisha ushirikiano. Mojawapo ya masuala ya msingi ni msisitizo kuwa ushirikiano wa Afrika Mashariki

utajengwa kwa awamu kwa kuanzia na Umoja wa Forodha, ukifuatia Soko la Pamoja (*Common Market*), kisha Umoja wa Sarafu (*Monetary Union*) na hatimaye Shirikisho (*Political Federation*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Pamoja ni ngazi ya Ushirikiano ambayo maudhui yake si ya kiuchumi peke yake bali yanahusu pia masuala ya kijamii, utamaduni na siasa. Maandalizi ya awali ya kuzindua majadiliano na mashauriano kuhusu kuanzishwa kwa Soko la Pamoja (*Common Market*) yamekamilika. Iwapo majadiliano na mashauriano ya nchi zetu kuhusu mtangamano wetu katika hatua hii yatapata maridhiano ya pande zote, Mkataba wa kutekeleza Soko la Pamoja utaruhusu, miongoni mwa mambo mengine, uhuru wa watu wa kwenda popote katika nchi yoyote mwanachama wa Jumuiya, uhuru wa kuanzisha makazi katika nchi yeyote mwanachama, uhuru wa kuajiriwa popote na uhuru wa uhamishaji wa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu na wananchi kwa jumla kwamba Serikali inatambua umuhimu na uzito wa kuwa na Soko la Pamoja katika mchakato mzima wa mtangamano wa Afrika Mashariki. Hatua hii ni nyeti sana kwetu Watanzania kwa sababu inagusa hisia ya ardhi yetu na ajira za watu wetu kuchukuliwa na raia wa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni ukweli usiopingika kwamba Tanzania ni nchi pekee ambayo bado ina ardhi ya kutosha ikilinganishwa na nchi za Kenya na Uganda. Aidha, kwa upande wa ajira, Kenya na Uganda wanaweza wakachukua nafasi nyingi muhimu za ajira kwa kuwa viwango vya elimu na mafunzo ya taaluma viko juu zaidi kuliko Tanzania.

Hivyo, itatulazimu tuwe makini sana katika hatua hii ili kulinda maslahi ya wananchi wetu na taifa letu kwa ujumla. Hivyo, itabidi tupate muda wa kutosha kujiandaa na masuala haya ya ardhi na ajira na tutawaomba wenzetu wa Kenya na Uganda watuelewe. Lengo la kufanya hivyo halitakuwa kukwamisha mchakato wa mtangamano bali ni kujiandaa ipasavyo ili kuepukana na madhara yanayoweza kujitokeza katika hatua hiyo iwapo tutafanya pupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uharakishwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki (*Fast Tracking of Political Federation),* katika juhudi za kuharakisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Viongozi Wakuu wa nchi Wanachama katika kikao chao maalum cha pili kilichofanyika tarehe 28-29 Agosti, 2004 mjini Nairobi - Kenya waliazimia kuteua Kamati itakayoangalia uwezekano wa kufupisha ratiba ya kuharakisha Mchakato wa Mtangamano wa kuanzisha Shirikisho ili hatua hiyo ifikiwe mapema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliyokuwa na Wajumbe wawili kutoka katika kila Nchi mwanachama wakisaidiwa na Sekratarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliwasilisha Taarifa yake katika Mkutano wa Sita wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 26 Novemba, 2004 mjini Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa upande wa Tanzania Taarifa ya Kamati hiyo ilipitiwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na kupitishwa ngazi zote za Serikali.

Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa hiyo yalipelekea Mkutano Maalum wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama uliofanyika tarehe 29 na 30 Mei 2005 mjini Dar es Salaam, kuagiza kwamba kwa kuwa kuwepo kwa Shirikisho imara kutawezekana tu iwapo wananchi wa Afrika Mashariki watamiliki wao wenyewe mchakato mzima wa kufikia Shirikisho hilo, upo umuhimu kwa kila nchi mwanachama kuweka utaratibu utakaoshirikisha wananchi kutoa maoni yao juu ya suala hilo kabla ya kuchukua hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika katika kikao hicho Wakuu wa Nchi waliagiza kuanzishwa katika kila nchi zetu tatu Wizara mahsusi ambayo itashughulikia masuala ya Afrika Mashariki tu. Aidha, Wakuu hao waliagiza ianzishwe nafasi mpya katika muundo wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Naibu Katibu Mkuu atakayesimamia mchakato wa kufikia Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha ya kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba maelekezo hayo yametekelezwa kwa kila Nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzisha Wizara inayoshughulikia masuala ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kuteua Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Afrika Mashariki.

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani aliyoonyesha kwangu kwa kuniteua kuongoza Wizara hii muhimu. Halikadhalika, Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamemteua Bi. Beatrice Kirasso raia wa Uganda kuwa Naibu Katibu Mkuu kusimamia mchakato wa kufikia Shirikisho la Afrika Mashariki. Tunampongeza na kumtakia kila la kheri katika wadhifa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza agizo la Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama la kutaka wananchi washirikishwe katika kutoa maoni yao, Wizara yangu imeandaa utaratibu wa kukusanya na kupata maoni ya wananchi Mkoa kwa Mkoa kuhusisha Viongozi mbalimbali wakiwemo Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wanataaluma, Wafanyabiashara, Wakulima, Wafanyakazi pamoja na makundi maalum katika jamii kama vile Viongozi wa Dini, Wazee, Wanawake, Vijana na kadhalika. Lengo la zoezi hili ni kupata maoni ya wananchi walio wengi ili hatimaye maamuzi yatakayotolewa kuhusu Shirikisho yawiane na maslahi ya wananchi kwa ujumla. Zoezi hilo linatarajiwa kuzinduliwa rasmi tarehe 15 Septemba, 2006. Natoa wito kwa Watanzania wote tujiandae vizuri na tushiriki kwa ukamilifu kutoa maoni yetu kuhusu mapendekezo ya kuharakisha mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya Katika Kupiga Vita Umaskini. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatambua na kuunga mkono juhudi za kupiga vita umaskini katika Nchi zetu tatu. Nchi zetu hazitafanikiwa kujenga Jumuiya imara iwapo zitabaki kuwa maskini. Hivyo, katika kutekeleza azma ya kupiga vita umaskini katika Nchi Wanachama, Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2006 - 2010 umeainisha maeneo ya msingi yatakayopewa

kipaumbele. Nchi yetu iko mstari wa mbele katika kupiga vita umaskini kama MKUKUTA unavyoainisha. Baadhi ya Sera na Mikakati zinazochangia kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi ni pamoja na:-

(i) Sera ya Maendeleo endelevu ya Viwanda - *Small and Medium Industrial Development Plan – (SIDP)* - 1996 - 2020 lengo lake ikiwa ni kuongeza kasi ya maendeleo ya viwanda nchini. Ukuaji wa Sekta hii ni muhimu sana katika kuongeza pato la Taifa na ajira kutokana na bidhaa za Tanzania zitakazozalishwa na viwanda vyenyewe. Hali kadhalika, ukuaji wa sekta hii utaongeza bidhaa za Tanzania katika soko la Afrika Mashariki na hivyo kutoa mchango mkubwa katika kupunguza umaskini.

(ii) Sera ya Uwezeshaji ya mwaka 2004 na Sheria ya Uwezeshaji ya mwaka 2004.

(iii) Kuwepo kwa Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) kwa ajili ya kujenga mazingira mazuri na endelevu ya wawekezaji.

(iv) Mkakati wa kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA), lengo ikiwa ni kuwawezesha wananchi katika jitihada zao za kuwekeza na kujiletea maendeleo kwa kutumia raslimali walizo nazo na hatimaye kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa kadri tutakavyofanikiwa kupunguza umaskini katika nchi wanachama wa Jumuiya, na ndivyo kazi yetu ya kujenga Jumuiya ya Afrika Mashariki itakavyoongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** aidha, Nchi zetu Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatambua juhudi za sekta zisizo rasmi zinazotambulika kama Jua Kali/Nguvu kazi kutokana na mchango wake katika utoaji wa ajira, kukuza teknolojia na kuongeza kipato kwa wananchi wenye kipato kidogo.Ili kuhamasisha, kuwaunganisha na kukuza masoko ya bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na Nguvu Kazi/Jua Kali, maonyesho ya bidhaa yanafanyika kila mwaka (mwezi Novemba hadi Desemba) kwa mzunguko wa Nchi wanachama. Mwaka 2005 Maonyesho yalifanyika mjini Kampala, Uganda. Mwaka 2006 Tanzania ndio mwandaaji wa Maonyesho hayo. Maonyesho yanaratibiwa na *East Africa Confederation of Informal Sector Organisation (ECISO).*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa kutambua mchango wa Kilimo katika uchumi wa Nchi, Nchi Wanachama wa Jumuiya zimekubaliana kuhusu kuandaa Sera na Mkakati wa pamoja kwa ajili ya kuendeleza masuala ya kufikia azma ya kuwa na uhakika wa chakula katika nchi wanachama wa Jumuiya. Baadhi ya makubaliano ni pamoja na maandalizi ya Sera ya Kilimo na Maendeleo ya Vijijini **(***The Agricultural and Rural Development Policy for the EAC)* na Mkakati wa Kilimo na Maendeleo ya Vijijini wa Jumuiya, *(The Agriculture and Rural Development Strategy for the EAC***).**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwenyekiti wa Tanzania Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka 2005 Tanzania ilikuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wakati wa Uenyekiti wake masuala mengi muhimu yalitekelezwa ikiwa ni

pamoja na uanzishaji wa Umoja wa Forodha. Masuala mengine yaliyotekelezwa ni pamoja na:

(i) Kuandaa Mkakati wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2006 - 2010.

(ii) Kuanza tathmini katika hatua za awali maombi ya nchi za Rwanda na Burundi ya kutaka kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(iii) Kuanzisha Kamisheni ya Ziwa Victoria na kufuatilia kwa karibu suala la ukame katika Afrika ya Mashariki.

(iv) Kuanza maandalizi ya awali ya Mkakati wa Kuendeleza Sekta Binafsi katika Afrika Mashariki.

(v) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo na Mkakati wa Kuendeleza Viwanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yalitekelezwa.

(vi) Maandalizi ya Majadiliano (*Negotiations)* kuhusu Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki yalianzishwa.

(vii) Kuhuisha na kuainisha Sera mbalimbali zikiwemo za fedha, kodi, uwekezaji rasilimali na masoko ya hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi ya Rwanda na Burundi. Nchi za Rwanda na Burundi zimewasilisha rasmi maombi ya kutaka kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki umeweka utaratibu, kanuni na masharti ya kutimizwa kabla nchi mwombaji kukubaliwa kuwa mwanachama.

Maombi ya nchi hizo yalianza kufanyiwa kazi mwezi Machi, 2005 wakati Timu ya Wataalam ilipotembelea Rwanda na Burundi kuhakiki utekelezaji wa vigezo vya kujiunga na Jumuiya kulingana na Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Taarifa ya Timu ya wataalam iliwasilishwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki na inaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, hatua ya kwanza ya kuanza majadiliano ya kina na nchi za Rwanda na Burundi kuhusu maombi yao ilizinduliwa tarehe 8 Julai, 2006, mjini Arusha.

Kukamilika kwa majadiliano hayo kutategemea utayari wa nchi za Rwanda na Burundi kutekeleza vigezo na masharti yaliyowekwa ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC HEADQUARTERS*). Suala la ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki limepatiwa ufumbuzi baada ya Serikali ya Tanzania kutoa eneo la ekari kumi na moja (11) kwa ajili ya ujenzi huo Mkoani Arusha. Aidha, Serikali ya Ujerumani imetoa kiasi cha fedha za kigeni *Euro* milioni nane kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu hayo. Ujenzi unatarajiwa kuanza baadaye mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto Ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ushiriki wa nchi katika Jumuiya ya kiuchumi ya aina yoyote, una changamoto zake na ndivyo ilivyo kwa uwanachama wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kipindi kirefu Tanzania haijaweza kufaidi kikamilifu matunda yatokanayo na ushiriki wake katika Jumuiya mbalimbali za Kikanda, Kimataifa na hata baina ya nchi na nchi (*Bilateral*).

Hali hii inatokana na kiwango kidogo cha tija na uzalishaji hususan katika sekta ya kilimo, viwanda na huduma. Kwa maana nyingine, Tanzania haijajizatiti vizuri katika kuwa na bidhaa na huduma za kutosha, zenye ubora wa juu ukilinganisha na zile zinazohitajika katika masoko husika, pamoja na uwiano usioridhisha uliopo kati ya sekta ya viwanda na kilimo. Kwa maantiki hiyo changamoto ya kwanza kwa watanzania ni kukuza uchumi wetu na kuongeza uzalishaji mali katika michepuo ya biashara, viwanda na kuongeza tija na ufanisi. Uzalishaji wa bidhaa usio ridhisha na tija duni kwa kiwango kikubwa unatokana na vikwazo vya kiuzalishaji (*supply side constraints*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vikwazo hivyo ni pamoja na:-

(a)Miundombinu duni mathalan barabara, reli, maghala na usafiri wa anga.

(b) Gharama kubwa za uzalishaji zinazotokana na bei ya juu ya umeme, maji, mawasiliano na uchukuzi.

(c) Matumizi ya teknolojia na nyenzo duni za uzalishaji, mfano jembe la mkono, pembejeo zisizo tosheleza;

(d) Huduma hafifu za ugani kwa wakulima, wafugaji na wavuvi;

(e)Michepuo michache ya bidhaa na masoko (*Product and Market Diversification*) kutokana na tafiti kuwa chache au tafiti kutolenga mahitaji ya soko, kukosekana taarifa za masoko na vilevile huduma;

(f)Ufinyu wa mitaji utokanao na urasimu na masharti magumu ya taasisi za fedha na mabenki;

(g)Uwiano usioridhisha baina ya sekta ya viwanda na kilimo katika kuhimiza usindikaji wa bidhaa ghafi kabla ya kuuza nje; na

(h)Taratibu za kiutawala zenye urasimu mkubwa zinazokwaza mwenendo wa biashara ndani ya nchi na mipakani mathalan kuendelea kuwepo vizuizi barabarani hata pale Serikali Kuu inapoamua viondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kukuza uchumi, changamoto nyingine ni namna ya kukabiliana na ushindani. Wafanyabiashara wengi wa Tanzania bado hawana uzoefu wa kutosha katika biashara ya kimataifa na bado ni wazito katika kutumia fursa za masoko hata pale zinapojitokeza. Dhana ya ushirikiano wa kiuchumi ikiwa ni

pamoja na kuanzisha Umoja wa Forodha, lengo lake ni kuunganisha masoko ya bidhaa ya nchi zaidi ya moja na hivyo kuunda soko moja kubwa la ndani.

Kwa mantiki hiyo kuwemo kwa Tanzania katika Umoja wa Forodha maana yake ni kwamba idadi ya watumiaji wa bidhaa za Tanzania imeongezeka kutoka idadi ya walaji milioni 36 hadi milioni takriban 90 ambayo ni idadi inayokadiriwa ya watu katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo, iwapo tutakuwa na uwiano mzuri kati ya sekta ya kilimo na viwanda na kuhimiza usindikaji wa bidhaa ghafi kabla ya kuuzwa nje; na iwapo tutazalisha bidhaa nyingi na bora zaidi na kwa bei ndogo zaidi kuliko bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, na iwapo wazalishaji wa bidhaa zetu watawekeza katika kuzitangaza bidhaa zao kwa nguvu na ukakamavu, sisi tunaamini kuwa bidhaa za Tanzania zina fursa kubwa ya kununuliwa katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki ukilinganisha na bidhaa zinazotoka nje ya Jumuiya kwa sababu bidhaa zetu hazitozwi ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ipo haja ya kujenga na kuinua uwezo wa Watanzania wa kufanya biashara katika mazingira ya ushindani. Ushindani wa ubora wa bidhaa na huduma na ushindani wa bei ya kuvutia wateja ndani ya Afrika Mashariki na kwenye Soko la Kimataifa. Juhudi zinazofanywa na Serikali za kuweka mazingira bora yanayochochea ukuaji wa uchumi kwa kuondoa vikwazo vya kisera na kiutendaji pamoja na mipango mbalimbali ya kuwawezesha watanzania ili waweze kuwa wabunifu na hatimaye wawe na uwezo wa kuwekeza katika miradi ya uchumi na huduma, zitasaidia kuwaandaa watanzania katika kutumia fursa zinazotokana na Tanzania kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pamoja na kuchukua hatua za makusudi za kuwawezesha Watanzania, ipo pia haja ya kuboresha teknolojia tunayotumia na kuinua kwa haraka ubora wa elimu na kuongeza idadi ya wanafunzi katika fani zote ili kukabiliana na ushindani kutoka Kenya na Uganda katika soko la ajira. Msukumo zaidi uwekwe kwenye mafunzo ya ufundi na sayansi na teknolojia kwa sababu wahitimu wa mafunzo hayo ndio watakaotakiwa zaidi katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya tatu kwa watanzania hasa wafanyabiashara na wakulima ni kutumia vizuri muda uliobaki wa kipindi cha mpito. Wafanyabiashara na wenye viwanda nchini wanapaswa wajipange vizuri kwa kufanya kazi kwa bidii na maarifa na kwa kujituma ili kuongeza uwezo wao wa uzalishaji na hivyo kujiimarisha. Hatua hiyo itawawezesha kumudu ushindani pindi muda huo utakapomalizika ifikapo tarehe 1 Januari 2010 ambapo bidhaa zote zinazoingia katika soko la Tanzania kutoka Kenya hazitatozwa ushuru tofauti na ilivyo sasa. Hii ni changamoto nyingine kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine changamoto kubwa kuliko zote zilizo mbele yetu katika mustakabali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni namna ya kupunguza au kuondoa tofauti iliyopo ya viwango vya maendeleo kati ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tanzania, Kenya, na Uganda zinatofautiana katika uwezo wa kiuchumi. Kenya haimo katika kundi la nchi maskini sana duniani (*Least Developed Countries*) na kwa hiyo inamiliki sehemu kubwa ya biashara ifanyikayo miongoni mwa Nchi Wanachama. Jedwali Na.1 linaonyesha kwamba mauzo ya Tanzania katika Jumuiya

ya Afrika ya Mashariki yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Mathalani mauzo yaliongezeka toka Dola za Kimarekani 40.7 Millioni Mwaka 2000 hadi 96.4 Millioni mwaka 2005, sawa na ongezeko la sailimia 140.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyosalia ni jinsi ya kupunguza nakisi katika urari wa biashara. Nakisi katika urari wa biashara ya Tanzania katika Jumuiya imekuwa ikipungua na kuongezeka kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 3. Hata hivyo, kwa wastani nakisi katika urari wa biashara imepungua ikilinganishwa na viwango vya mwanzoni mwa miaka ya 1990. Changamoto hii imekuwepo hata kabla na baada ya Umoja wa Forodha kuanzishwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** haupo ubishi kuwa kwa muono wa muda mfupi Tanzania yaweza isinufaike sana kutokana na uwanachama wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, kwa mtazamo wa muda wa kati na muda mrefu sisi tunaamini kuwa Tanzania ina nafasi nzuri ya kunufaika zaidi na uwanachama wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki iwapo agenda ya kukuza uchumi tutaifanya kuwa agenda ya kudumu na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya amani na utulivu iliyopo nchini ni kuvutio kikubwa kwa wawekezaji na pia ni kichocheo muhimu cha maendeleo. Aidha, Tanzania ina rasilimali nyingi ambazo bado hazijatumika kikamilifu. Tuna ardhi tele na yenye rutuba ambayo tukiitumia vizuri, hasa katika kilimo na ufugaji bora, itachochea kuinua tija na kukuza uchumi. Sekta ya maliasili, hususan uvuvi, utalii na sekta ya madini ni maeneo mengine yenye umuhimu wa pekee katika kuongezea Tanzania nguvu ya ushindani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na katika ngazi ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Mashariki mwa Jamhuri ya Kongo ambazo hazina bahari **(***Landlocked***)** zimekuwa zinatumia barabara, reli, na bandari za Tanzania kwa bidhaa zao za nje. Kwa kweli iwapo tutafanikiwa kupata sehemu kubwa ya biashara ya nje ya nchi hizo jirani kupitia Tanzania tutakuwa tumejihakikishia mapato makubwa ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivyo, changamoto kubwa tuliyonayo Watanzania ni kujizatiti kufanikisha azma hiyo kwa kupunguza gharama za kufanyia biashara, ikiwemo gharama za nishati na kuboresha miundombinu.Tunapaswa tuongeze ufanisi kwa kuboresha utendaji wa taasisi zinazowahudumia wawekezaji na wafanyabiashara kama vile bandarini na kwenye vituo vya Forodha na uhamiaji mipakani kwa kuondoa kwa haraka vikwazo vilivyopo vinavyoleta usumbufu kwa biashara ya nje ya nchi hizo jirani na kufukuza wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu sahihi la kuondoa tofauti iliyopo ya viwango vya maendeleo katika nchi wanachama wa Jumuiya yetu ni kukabiliana kikamilifu na changamoto hizo. Hivyo, iwapo misingi ya kuimarisha uchumi jumla itaendelezwa kwa kasi, na iwapo malengo ya kukuza uchumi wetu kupitia mipango maalum ya maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii tuliyojiwekea yatafanikiwa, Tanzania ina nafasi ya pekee ya kunufaika zaidi ya Kenya na Uganda kwa sababu ya ukubwa wake na kutokana na kuwa na rasilimali nyingi na Soko kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hizo ni vizuri ikakumbukwa kwamba kuongezeka kwa kasi ya ushindani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kutafanya baadhi ya nchi wanachama kuendelea kwa haraka kuliko nchi nyingine. Kusema kweli itakuwa miujiza iwapo nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zitapiga hatua sawa. Lakini, ili Jumuiya yetu mpya isikumbwe na misukosuko ya kutokuaminiana na hivyo kujenga chuki miongoni mwa nchi wanachama, itabidi pawepo na utaratibu wa kuhakikisha kuwa Jumuiya hii mpya tunayoijenga inaleta faida sawa kwa nchi zote wananchama. Likifanyika hilo ndipo kila nchi mwanachama itakavyojihisi kuwa kweli nayo ni mshiriki kamilifu na atakayefaidika na ushirikiano huu wa Afrika Mashariki. Hilo lisipozingatiwa Jumuiya yetu tunayoijenga itayumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuwajengea uwezo wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kunufaika na fursa zilizopo kwenye soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Hatua hizo zinatekelezwa kama sehemu ya mageuzi yenyewe ya kiuchumi, kupitia mipango maalum ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii tuliyojiwekea. Mipango hiyo ni pamoja (*Makofi*)

(a) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza UmaskiniTanzania (MKUKUTA).

(b) Sera ya Uwezeshaji ya mwaka 2004 pamoja na Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji ya mwaka 2004.

(c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za Biashara Tanzania **(**MKURABITA).

(d)Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA).

(e)Mpango Maalum wa kuharakisha maendeleo Tanzania (*Tanzania Mini Tiger Plan – 2020)*

(f)Sera ya Biashara na ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Mashauriano. Serikali katika kutekeleza Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Treaty*) na Itifaki zake imekuwa na utaratibu madhubuti wa kushauriana na wadau mbalimbali katika kubuni sera na mikakati ya utekelezaji.

Kwa mfano, Sera za Kodi zinawashirikisha wadau kupitia Kamati ya Sera za Kodi (*Task Force on Tax Reforms***),** vile vile, utaratibu wa Rais kukutana na wazalishaji na wafanyabiashara pamoja na ushiriki wa Wadau wa Asasi zisizo za Kiserikali katika utaratibu wa kufanya mapitio ya Fedha za Umma (*Public Expenditure Review Consultative meetings*). Kimsingi mbinu hizo zinaweka wigo mpana wa ushiriki wa Watanzania katika kutoa maoni yao katika sera na sheria za nchi. Aidha, mchakato huu unawezesha kupanua ushiriki wa Wananchi katika masuala mbalimbali yanayohusu

mustakabali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali imepania kutimiza wajibu wake. Tunaziomba sekta za uzalishaji na wananchi kwa ujumla nao watimize wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kazi Zilizopangwa Kutekelezwa Katika Mwaka Wa Fedha 2006/2007. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za kisekta pamoja na wadau mbalimbali itaendelea na juhudi zake za kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Itifaki zake, pamoja na Mkakati wa Tatu wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuwawezesha Wananchi kushiriki kikamilifu katika kuzitumia fursa mbalimbali za kiuchumi kwa ufanisi na kwa faida yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu yatakayopewa kipaumbele na Wizara katika mwaka 2006/2007 ni kama ifuatavyo:(i) Kujenga uelewa kwa wananchi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani, Sekta binafsi, Baraza la Wawakilishi la Mapinduzi Zanzibar, Bunge na Viongozi wa Serikali kwa ujumla kuhusu masuala ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. (*Makofi*)

(ii) Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa Umoja wa Forodha na Majadilia

(iii) Kufanya maandalizi ya kutosha kuhusu majadiliano na Kenya na Uganda katika hatua zinazofuata za Mtangamano, kufanya utafiti kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya na Itifaki zake kwa lengo la kubainimapungufu yaliyopo na kutoa mapendekezo ya kuboresha.

(iv) Kuratibu na kuandaa taarifa kuhusu maoni ya wananchi, sekta binafsi na wadau wengine kuhusu haja ya kuharakisha Mtangamano wa Afrika Mashariki.

(v) Kuwasiliana na Wizara, Sekta Binafsi na Wadau wengine katika kubuni Sera, Mikakati na Programu za Utekelezaji katika kukuza na kuendeleza uzalishaji mali na biashara.

(vi) Kutumia Balozi zetu nchini Kenya na Uganda katika kuwezesha Watanzania kuendeleza biashara.

(vii)Kuratibu kwa karibu utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya vyombo vya Jumuiya ikiwemo Mikutano ya Wakuu wa Nchi, Baraza la Mawaziri, Bunge na Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(viii) Kufuatilia kwa karibu miradi na programu za maendeleo endelevu ya Ziwa Victoria na ukanda wake.

(ix)Kuendelea kushawishi nchi wanachama kuweka mkazo zaidi katika masuala yahusuyo maendeleo badala ya biashara peke yake.

(x)Kuratibu na kutoa mapendekezo ya kuimarisha taasisi na sekta zinazojihusisha na masuala ya Jumuiya.

(xi)Kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji kwa kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam wa Wizara.

(xii) Kusimamia mchakato wa Mtangamano wa kuelekea kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuboresha Mazingira Ya Utendaji Kazi Na Upatikanaji Wa Nyenzo Za Kufanyia Kazi. Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki bado ni changa na ina upungufu mkubwa wa watumishi wa taaluma mbalimbali pamoja na vitendea kazi hasa katika Idara zinazotekeleza majukumu ya msingi ya Wizara.

Ili kukabiliana na tatizo hili, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wasiopungua 40 katika mwaka 2006/2007 ambao kati ya hao ni wataalam wa masuala ya fedha, biashara, uchumi, sheria, sayansi ya jamii, takwimu na mawasiliano. Aidha, Wizara imeandaa mpango wa kuwapatia mafunzo wataalam wa Wizara katika stadi za majadiliano (*Negotiation Skills*), eneo ambalo ni muhimu katika kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilipoanzishwa ilikuwa haina jengo la ofisi lakini kutokana na ushirikiano mzuri ndani ya Serikali, Wizara imefanikiwa kupata eneo la Ofisi katika jengo la *NSSF, Water Front.* Baada ya kukamilisha matengenezo ya ofisi, Wizara itashughulikia ununuzi wa samani pamoja na vitendea kazi. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Fedha kwa kufanikisha haya. Aidha, naishukuru Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kutupatia nafasi ya ofisi kwa kipindi chote tangu Wizara ianzishwe mapema mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yametokana na Ushirikiano wa Serikali yetu, Taasisi binafsi, Mashirika yasio ya Kiserikali, Wafanyabiashara pamoja na Wafadhili mbalimbali. Naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wote waliohusika kwa njia moja ama nyingine katika mchakato wa mtangamano wa Afrika Mashariki.

Kwa namna ya pekee napenda niwashukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne kila mmoja wao kwa nafasi yake, kwa uongozi wao mahiri, kwa hekima na busara zao, kwa muono wao wa mbali na moyo wao wa kujituma uliowezesha Tanzania kuwa mshiriki mzuri na wa kutegemewa katika majadiliano ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wenzangu katika Wizara waliowezesha hadi leo kusomwa kwa Hotuba hii katika Bunge lako Tukufu.

Kwa heshima, napenda nimshukuru Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala Mbunge wa Nkenge kwa msaada wa karibu alionipa katika kusimamia shughuli

za Wizara hii mpya. Napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu, Bwana Omar Bendera, Wakuu wa Idara na Vitengo, pamoja na wafanyakazi wenzangu wote wa Wizara.

Nawashukuru kwa kuweza kukamilisha bajeti hii kwa wakati pia ninawapongeza kwa utendaji kazi wao wenye tija pamoja na uchache wao, na mazingira magumu hususan katika kipindi hicho ambapo Wizara haikuwa na ofisi zake za kudumu. Naomba waendelee na moyo huo huo wa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na ili kufanikisha utekelezaji wa kazi Mbalimbali za Wizara, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya Shilingi 7,157,257,000/- (bilioni saba milioni mia moja hamsini na saba mia mbili hamisini na saba elfu) kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2006/2007 kwa mchanganuo ufuatao:

- Shilingi 4, 900, 000,000/- Mchango wa Uanachama wa Nchi yetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

- Shilingi 363,587,000/- Kwa ajili ya Mishahara (*PE*) ya Watumishi wa Wizara na

- Shilingi 1,893,670,000/- Ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida *(OC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Naafiki!

*(Hoja iliamuliwa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu kutoa taarifa ya Kamati sasa *I World like to introduce to you the delegation from United Status* ambao wako hapa na watakuwa na sisi hapa kwa mambo mbalimbali, naona wazo lao kubwa wanataka kufanya mambo yanayohusi *Inter Parliamentary Exchange* lakini *they will be also discussing some Investment Issue* na *they will be also meeting some Chairs of our Parliament Committees* katika siku hizi mbili ambazo watakuwa hapa.

Wanaongozwa na Mr. Mathew yeye ni *Chief of Staff Inter Parliamentary Exchange l*akini wana Mr. Sein yeye ni *Concretion Staff* ambaye wako naye, yuko pia Mr. Brian yeye ni *Professional Staff of the Small Business Committee and Inter Parliamentary Exchange* huko kwao. Lakini pia wana Mr. Dely yeye ni *Deputy Chief of Mission US Embassy* lakini yeye yuko hapa Dar es Salaam na pia wanaye Miss Catherine yeye ni *Second Secretary US Embassy* hapa Dar es Salaam.

Kwa hiyo tunawakaribisha sana, *thank you very much*.

Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kamati, Mheshimiwa Zaynab Matibu Vullu, aweze kutoa hotuba ya Kamati.

**MHE. ZAYNAB MATITU VULU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwepo hapa ikiwa ni mara yangu ya kwanza leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje. Pia nawashukuru wananchi wa Mkoa wa Pwani hususani wanawake walionichagua kushika wadhifa huu, hali kadhalika namshukuru Mama yangu Mpendwa Bi Saida na Babu yangu Sheikh Nurdin Hussein Shadhiria na Baba yangu Mzee Matitu kwa malezi yao mazuri na hatimaye kupokezana kijiti cha malezi kwa Mume wangu Mpenzi Bwana Yahya Vulu. (*Makofi*)

Baada ya shukrani hizo kwa mara nyingine tena kuungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Yusuph Rajab Makamba kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi. Aidha, naipongeza Sekretarieti nzima ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** awali ya yote naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje kwa hekima na uzoefu wao kuhusiana na masuala mbali mbali katika nyanja za ushirikiano wa kikanda ambao umesaidia kujadili kwa kina masuala hayo pamoja na bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mbunge, na Naibu waziri Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mbunge, Katibu mkuu wa Wizara na wataalam wengine kwa kuwasilisha mbele ya kamati mapendekezo ya Bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** li kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyoelezwa na Mheshimiwa Waziri, Wizara inaomba jumla ya sh. 7,157,257,000/= kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mishahara, michango ya nchi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi na wadau wengine kuhusu kuharakisha uanzishwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki na matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati. baada ya kujadili mapendekezo ya wizara hii kwa kina Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi waendelee kuelimishwa kuhusu kuwepo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zilizopo ili waweze kunufaika na kuwepo kwa Jumuiya hii. Katika mchakato huu wabunge wa Bunge hili pamoja na wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki washirikishwe kikamilifu ikiwa ni pamoja na kutafuta mbinu mbadala.Aidha, viongozi katika ngazi mbalimbali waelimishwe ili

wasiwape wageni ardhi, ili wageni hao wasije wakamiliki ardhi ya nchi yetu kwa kisingizio cha Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idara ya forodha ifanye utafiti kujua sababu zinazowafanya Watanzania na wafanyabiashara wengi kuingiza nchini mizigo yao kupitia bandari ya nchi jirani badala ya bandari za nchi yetu ili kuondoa kasoro zilizopo kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali kwa kutumia bandari zetu kwa maanaya *Transit Trade*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wa viwanda wajizatiti vizuri ili kuweza kushindana na nchi jirani kiuzalishaji na hatimaye kumudu ushindani katika soko la Jumuiya hii. Serikali ihamasishe watanzania kutumia fursa zilizopo ndani ya Jumuiya kwa kuzalisha bidhaa bora zikiwemo za kilimo na sanaa za mikono kwa kuweka vivutio maalumu.

Aidha, yawepo mawasiliano ya ndani kuhusu bidhaa na mazao yanayopatikana nchini kabla ya kuagiza kutoka nje ya nchi, suala hili liende sambamba na kuhimiza uzalendo kwa Watanzania kutumia bidhaa na mazao yanayozalishwa nchini badala ya kupenda bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa moja ya hatua muhimu ya kufikia Shirikisho la Afrika Mashariki ni kuwa na soko la ajira la pamoja, Kamati inashauri Serikali iboreshe elimu katika nyanja mbali mbali ikiwemo sayansi na ufundi, lugha za kimataifa na maadili ya kazi ili kumudu ushindani kwa kuwa kuna wasi wasi miongoni mwa Watanzania kuwa soko la ajira la pamoja likianza ajira nchini zitachukuliwa na wageni. Hata hivyo hiyo ni dalili ya kutojiamini kwa kuwa kuna Watanzania wengi wenye elimu ya juu ambao hawana ajira nchini.

Ni vema watanzania wakajua udhaifu uliopo badala ya kudhani kuwa kuna wasomi wachache nchini kwani kwa sasa Tanzania ina Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki 26 na bado vingine vinaendelea kuanzishwa ambavyo vinatarajia kuwa vinatoa wahitimu wengi, kwa mfano, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Vyuo Vikuu nchini vilidahili yaani *enrolment* jumla ya wanafunzi wapatao 48,000

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa kuwa kuna baadhi ya Watanzania ambao bado wanahofu juu ya hatma ya Tanzania ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naomba kumnukuu mwanafalsa mmoja wa India aitwaye Alankrita Banerjee aliyesema maneno yafuatayo, nanukuu:-

*"The greatest asset in the quest for success and happiness is our measure of self-confidence. More than half of life's battles are won or lost in the mind. Therefore, a person needs to saturate his or her mind with positive thoughts at all times. Our mind will then play host to many big ideas. Converting these big ideas into practical goals and long-term success calls for dollops of vision, hard work and perseverance*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, nukuu hiyo inasisitiza dhana ya kujiamini, dunia ya sasa inaongelea kuungana, hatuwezi kupata maendeleo kwa kujitenga na wenzetu, tukijipanga vizuri na kutumia raslimali zetu kwa makini Kamati inaamini kuwa Tanzania itanufaika sana na Jumuiya hii na itakapofikia hatua ya kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki manufaa hayo yatakuwa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki haina jengo lake yenyewe kwa ajili ya matumizi ya ofisi, kwa mwaka huu wa fedha Wizara hii imetenga kiasi cha sh. 216,000,000/= kwa ajili ya pango. Kamati inashauri Wizara itafute kiwanja na kujenga jengo lake yenyewe au hata kununua jengo badala ya kukodi kwani kiasi hicho cha fedha kinaweza kutosha kujenga jengo linaloweza kufaa kwa matumizi ya ofisi ya wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika ya Masharikiinaendeshwa kwa michango ya nchi wanachama, ili iweze kuendelea kutimiza azma yake ya kufikia shirikisho Kamati inashauri kila nchi mwanachama iwe na mpango maalum wa kuhakikisha kuwa michango yake inatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** zaidi ya watu milioni 30 wanaishi kwa kutegemea bonde la Ziwa Victoria, Serikali yetu kwa kushirikiana na wadau wengine washirikiane kukabili uharibifu mkubwa unaolikabili Bonde la ziwa hili kwa kutunga sheria zitakazolinda ziwa hili na mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki inafanya kazi ya uratibu tu lakini utekelezaji wa maamuzi muhimu ya vikao mbali mbali vya Jumuiya ni jukumu la kila wizara, idara za serikali sekta binafsi na watanzania wote kwa ujumla. Kamati inashauri sera na mipango ya serikali iende sambamba na mikakati ya Jumuiya hii hususan katika nyanja za mawasiliano, nishati, barabara, mazingira n.k. ambazo zimo katika rasimu ya Mkakati wa Tatu wa Jumuiya wa 2006-2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika ni dhahiri kuwa Serikali yetu pia ina mikakati ya ndani inayolenga kuendeleza maeneo kama hayo, hivyo ni vema kuwa waangalifu ili raslimali zetu zielekezwe katika maeneo ambayo yako nje ya mikakati ya Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zina uhuru wa kujiunga na Jumuiya mbalimbali za kikanda kwa kuzingatia maslahi ya nchi husika. Hata hivyo kamati inashauri Jumuiya hizi za kikanda zisiathiri ushirikiano baina ya nchi zetu. Mpaka sasa Jumuiya za kikanda ambazo nchi za Afrika Mashariki ni wanachama ni *COMESA* (Kenya na Uganda), *SADC (Tanzania), IGAD* (Kenya na Uganda), *IOC* (Uganda), *Nile Basin* (Tanzania, Kenya na *Uganda), EAC (Tanzania,Kenya* na *Uganda).* Kwa kuwa nchi hizi zinaelekea kwenye shirikisho ni vema tofauti hizi zikaanza kuondolewa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Jumuiya inaendelea kukua kwa maana ya kuanzishwa kwa asasi mbali mbali zinazosimamia majukumu yanayohusu Jumuiya hii. Kamati inashauri Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ikishirikiana na Wizara zingine

ijitahidi kuwa na ushawishi mkubwa ili makao makuu ya baadhi ya asasi hizo yawe nchini mwetu ili kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa kuwa shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea kupanuka ni vema sheria balimbali zikatungwa ili kusimamia utekelezaji wa hughuli hizo. Aidha Mkataba ulianzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The Treaty for the Establishment of The East African Community*) uangaliwe upya ili kuondoa mapungufu yaliyopo katika Mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho. napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kuhusu mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha wa 2006/2007. Ni kweli kwamba fedhazilizotengwa kwa ajili ya wizara hii hazitoshi, hata hivyo Kamati inasisitiza kuwa kuweko na nidhamu ya hali ya juu katika kutumia fedha iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ili mchango wa Kamati uweze kuleta maana kwa serikali tunashauri Kamati iwe inashirikishwa katika kutoa mapendekezo ya bajeti kabla ya Wizara ya Fedha kuweka kiwango cha mgao *(ceiling)* wizara,utaratibu huu wa sasa hausaidii sana kwa vile maoni ya kamati hutolewa baada ya Serikali kutoa uamuzi kuhusu mgawanyo wa fedha ya bajeti

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Mwisho nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa kuandaa taarifa hii na kunipa heshima ya kuiwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wajume wenyewe ni Mheshimiwa Annah M. Abdallah, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Mheshimiwa Mussa A. Zungu, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wengine ni Mheshimiwa Mohamed R.Abdallah, Mheshimiwa Ame P. Ame, Mheshimiwa Abubakar Kh. Bakary, Mheshimiwa Mohamed G. Dewji, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Yono S.Kevella, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Muhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha,
Mheshimiwa Zainab Matitu Vulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** baada ya kusema hayo, napenda kulishauri Bunge lako tukufu likubali kujadili na hatimaye kupitisha mapendekezo ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo ni jumla ya sh. 7,157,257,000/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena wewe binafsi, vile vile nawashukuru waheshimiwa wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha naunga mkono hoja ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti, ya Wizara ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa hai na wazima. Pili naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuchangia katika Wizara hii, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi zetu za Afrika ya Mashariki. Tatu naomba nilishukuru sana Jimbo langu la Mgogoni Pemba kwa kunichagua kwa 95% kuwa Mwakilishi wao na pia nilishukuru Baraza la Wawakilishi kwa kunichagua mimi miongoni mwa waheshimiwa wabunge wenzangu 5 tuliochaguliwa kwa kuliwakilisha Baraza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi yetu ya Upinzani inapenda kutoa mawazo na maoni yake kuhusu Wizara hii kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya ushirikiano katika Afrika ya Mashariki ni ya zamani sana, karibu miaka 109 sasa ukitilia maanani kwamba ushirikiano wa mwanzo ulianza kwa ujenzi wa reli baina ya Kenya na Uganda mwaka 1807 na 1901. Baada ya hapo ilifuatia ushirikiano wa mambo yafuatayo:-

1. Kituo cha ukusanyaji ushuru baina Kenya na Uganda 1900.
2. Utumiaji wa sarafu moja baina ya Kenya na Uganda 1905.
3. Shirika la Posta 1905 .
4. Mahakama ya Rufaa ya Afrika ya Mashariki 1909.
5. Umoja wa Forodha 1919 ambao ulianzishwa na Kenya na Uganda na baadae Tanganyika ikajiunga 1922. Umoja huu ulikubaliana kutokutozwa ushuru kwa bidhaa zilizotengenezwa nchi hizo za Afrika Mashariki, na zile zilizotoka nje zilikuwa zinatozwa ushuru.
6. Kuundwa kwa Kamisheni ya Afrika Mashariki baina ya 1947 na 1966 ambayo ikisimamia shughuli zote za ushirikiano; ambayo baina ya 1961 na 1966 kulikuwa na Shirika la Huduma za Pamoja la Afrika Mashariki kabla Jumuiya hasa ya Afrika Mashariki haijaundwa katika mwaka 1967. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilihusisha nchi nne za Afrika Mashariki; Kenya, Tanganyika, Uganda na Zanzibar. Shughuli za pamoja zilikuwa ni Reli na Bandari, Shirika la Ndege, Shirika la Posta na Simu, Bodi ya Sarafu, Baraza la

pamoja la Chuo Kikuu, Mahakama ya Rufaa, Utafiti wa magonjwa ya mimea na wanyama, Sayansi ya Bahari, Takwimu na Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya na kwa masikitiko makubwa tunasema kuwa, Jumuiya hiyo haikudumu sana. Miaka kumi tu baada ya kuundwa kwa Jumuiya hiyo, ilivunjwa rasmi na nchi hizo zilizokuwa wanachama, ambapo kwa wakati huo ilikuwa ni nchi tatu badala ya nne (Kenya, Tanzania na Uganda). Sasa ni vyema tukajiuliza, kwa nini Jumuiya hiyo ilivunjika; je, sababu hizo zingalipo au zimeshaondoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zipo nyingi ambazo Kambi ya Upinzani inahisi zilichangia kuvunjika kwa Jumuiya hii. Lakini kwa faida ya Bunge lako Tukufu, sababu tatu ambazo ni lazima tuzitazame vizuri, ndizo tunazopendekeza kuzitaja hapa. Kwanza, tunahisi ushirikiano uliokuwepo, haukuwa wa kweli na thabiti. Ulikuwa ni ushirikiano wa kutegemeana ili aliyemzidi mwenzake kwa ujanja, basi afaidike zaidi. Nia za nchi zetu kisiasa tunahisi hazikukamilika. Jumuiya ilikuwa na mapato na hasara zake. Sikuwahi kusikia hata siku moja, kuwepo kwa utaratibu maalum *(formula)* ya mgawano wa mapato au hasara. Pengine Sheria ya Msituni ndio iliyotumika *(survival of the fittest)***.** Hili ni kosa kubwa ambalo lilijitokeza wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la tatu ni kuwa, Kenya ilikuwa na uchumi tofauti na Uganda, Tanganyika na Zanzibar, kinyume chake kwa nchi hizo, yaani ni kusema kuwa, kila nchi ilikuwa na uchumi tofauti na kwamba, Kenya ilikuwa na uchumi mkubwa na mzuri kuliko nchi nyingine wanachama. Chumi hizi tofauti, zilifanya kila nchi kupiga hatua tofauti katika maendeleo yake, ambayo taathira yake ni kusababisha utekelezaji mbaya wa shughuli za Jumuiya hiyo. Hivyo, kila nchi ikaona kana kwamba, mwenzake anajilimbikizia neema kwake tu au mwengine kuona kwamba, ananyimwa fursa fulani na hivyo kuathirika na shirikisho hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi yetu ya Upinzani inahisi kuwa, sababu hizi bado zipo na ni lazima zifanyiwe kazi kubwa sana, vinginevyo bado misingi ya kuanzishwa tena kwa Jumuiya hii, itakuwa ni mibovu na isiyofaa *(Shaky Foundation)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ni vyema tukajiuliza kwamba, kwa kuwa sababu hizi zilizoiangusha Jumuiya bado zipo; je, Watanzania tujifunze nini katika kadhia hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajifunza nini kutokana na sababu za kuanguka kwa Jumuiya? Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni fundisho kubwa tulilolipata katika nchi zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, inaonesha wazi kuwa, nchi wanachama hazikutafakari kwa kina suala hili na lilichukuliwa kihamasa tu za kisiasa zaidi kuliko za kiuchumi.

Pili, haikutiliwa maanani uwezo wa nchi hizi kiuchumi kwamba, baadhi yao walikuwa na uwezo mzuri wakati wengine walikuwa na uwezo duni.

Tatu, baadhi ya nchi hizi ziliona kwamba, wao hawafaidiki na umoja huu kwa sababu ya uwezo wao mdogo na hivyo kudumaza zaidi maendeleo ya nchi zao kuliko kuyanyanyua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo haya ni lazima sisi Watanzania tuyasome kwa Jumuiya yetu ya hivi sasa, ili yasije yakatupata yale ya zamani. Pamoja na kwamba, zipo hatua ambazo zimeshachukuliwa kuziba au kupunguza kasoro hizo, lakini ni vyema tukawa kila wakati, tunakuwa makini ili kasoro hizo zisije zikajitokeza tena. Pia ni vyema Mheshimiwa Waziri, akatuelezea kama tahadhari imechukuliwa ya kuziba kabisa au kupunguza angalau kwa kiwango kikubwa athari hizi, ambazo zinaweza kuleta athari kubwa kwa Tanzania na Jumuiya kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kweli Kenya, Tanzania na Uganda, wako tayari kwa ushirikiano huu na hatimaye kuundwa kwa umoja huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Tanzania imejizatiti vipi kuzungumzia au kulinda haki za Zanzibar kwa yale mambo ambayo si ya Muungano, lakini yanashughulikiwa moja kwa moja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar? Je, Tanzania wanaelewa kuwa Uganda imeshapata mafuta na sasa wanafanya utafiti wa *Uranium* na kwamba Kenya nayo iko karibu kupata mafuta na bidhaa hizi zinaweza kabisa kuchafua Jumuiya hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naeleza haya kwa sababu matatizo haya ndiyo yanayoleta migongano isiyokuwa ya lazima na pia isiyokuwa na maana kwa Tanzania. Migongano ambayo nitaielezea kwa kirefu hapo baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hatuoni kuwa haraka zetu za chura zinaweza zikatufikisha pabaya? Hamasa za kisiasa tu za kuonesha tutafarijika kwa kuwa na utulivu wa kisiasa au kwa kuwa na uhakika wa usalama wa nchi zetu na kuwa na chombo cha uchumi kitakachosaidia nchi kuondoa umasikini, haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tamaa tu za kuwa fulani atakuwa Rais wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nayo haitoshi, kama ilivyokuwa haitoshi kufikiria tu kwamba, umoja huu ni lazima ili tuweze kuleta maendeleo ya kudumu ya kiuchumi katika nchi zetu hizi. Fikra hizo ni potofu kidogo na mimi binafsi pamoja na Kambi yetu, hatukubaliani nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini msimamo wa Upande wa Kambi yetu, kila mmoja wetu na katika nchi zetu sote tunauhitaji umoja huu. Wadau wote wangelipenda kwanza tuanze na misingi iliyo bora zaidi na yenye uhakika wa kuhimili vishindo. Ni hapo tu ambapo watu wa nchi hizi wangeliweza kufurahia uhuru ulio mpana zaidi kwa kuwa na uendeshaji wa kidemokrasia wa chombo hiki, ambacho hatimaye kingetoa fursa sawa kwa wananchi wa nchi zote tatu, wakiwemo na wananchi wa Zanzibar, ambao nao kuna mambo mengi wanayopaswa kuyashughulikia wao wenyewe kama nchi na ambayo hayamo katika orodha ya mambo ya Muungano. Hivyo basi, mambo hayo hayatoshughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Umadhubuti wa aina hii ndio

utakaofanya hata nchi jirani, kutuonea wivu na wao kushawishika kutaka kujiunga na umoja huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi, Kambi yetu inahisi kwanza tungelitazama matatizo na kuyatatua na baadae kufanya shirikisho lililo madhubuti zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya matatizo ni pamoja na:-

(a) Kuweka bayana mambo ambayo Zanzibar, kama nchi inayoshughulikia mambo yake yasiokuwa ya Muungano, watayashughulikia wenyewe. Ama kuweka utaratibu maalum ambao Zanzibar inawakilishwa vizuri katika shughuli hizi na sio tu ule uwakilishaji wa kupelekwa Afisa mmoja kusikiliza na kupewa posho.

(b) Vipi ikiwa mambo yatashughulikiwa na Jamhuri ya Muungano na pale ambapo masuala hayo sasa yamewekwa kuwa miongoni mwa shughuli za umoja huo, Zanzibar itawasilishwa namna gani wakati ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio wanaoingia katika vikao hivyo?

(c) Mgao wa faida na hasara kwa nchi hizi tatu katika Jumuiya na vipi Zanzibar itafaidika au itaathirika kutokana na faida au hasara hiyo? Je, tusubiri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pale watakapofurahi ndipo watugawie faida itakayopatikana kutokana na Jumuiya hiyo au kuna utaratibu gani wa kufuatwa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara? *(Makofi)*

(d) Vipi vyombo kama Bunge la Afrika Mashariki au Mahakama ya Afrika Mashariki vitakuwa na uwakilishi unaokubalika kwa Zanzibar, hasa ukitilia maanani kuwa, masuala ya Bunge na Sheria si mambo hasa ya Muungano na hivyo basi uwakilishi huo wa Zanzibar usifanywe na chombo cha Muungano kama vile Bunge?

Kwa maana hiyo basi, ikiwa utaratibu mzuri haukuchukuliwa, kutakuwapo na migongano ya wazi baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, kwa mambo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika yale mambo ambayo si ya Muungano. Ni maoni na mapendekezo ya Kambi hii ya Upinzani kwamba, ni lazima yasawazishwe mambo madogo madogo kama haya ili hatimaye yasije yakaleta tofauti zisizokuwa za lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migongano iliyopo, licha ya Waheshimiwa Wabunge, kila mtu anaielewa vyema Ibara ya 4(3) na nyongeza ya kwanza ya Ibara hiyo inayoelezea mambo ya Muungano na yale yasiyokuwa ya Muungano. Orodha hiyo ya mambo 22 ambayo kwayo ina utata, inayatoa mambo mengi kuwa si ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo si ya Muungano, sasa yamewekwa chini ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa maana hiyo, yatashughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa maana nyingine pana, kubwa na ya wazi ni kuwa, Zanzibar yenye mamlaka ya kushughulikia mambo hayo yasiyokuwa ya Muungano, imepokonywa mamlaka hayo na kuambiwa kwamba, sasa mambo hayo ingawa si ya Muungano, lakini yanashughulikiwa na Serikali ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuoni kwamba, sasa tunakwenda kwenye hadithi ya mchungaji na ngamia wake, alipomkaribisha ngamia huyo kuficha baridi yake sehemu ndogo ya kichwa na mwili wake? Lakini sasa inaonesha wazi kuwa, mambo hayo yameshaingizwa ndani ya kundi la mambo yanayoshughulikiwa na Jamhuri ya Muungano, yaani sasa ni Mambo ya Muungano kwa mkono mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cheche hii imeanguka kwenye majani makavu, hala hala na kushika moto. Vinginevyo ni vizuri na muhimu kuyaona na kuyawekea mkakati mzuri wa kuyatatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi mambo aina hiyo ni kama yafuatayo:-

- Ibara ya 24 ya Mkataba wa Jumuiya inayohusu Mahakama ya Jumuiya.

- Ibara ya 48 ya Mkataba ambapo haitoi uwakilishi kwa Zanzibar na kwamba hata Bunge hili Tukufu, halikuona haja angalau ya nafasi tatu kupelekwa Zanzibar kwa kupatikana Wajumbe watakao chaguliwa na Baraza la Wawakilishi na sio mfumo wa sasa wa Bunge kuwachagua Wazanzibari wanaowakilisha katika Bungehilo la Afrika Mashariki.

- Ibara ya 76 ya Mkataba wa Uanzishaji wa Soko la Pamoja *(common market).*

- Ibara ya 79 ya Mkataba kuhusu uendelezaji wa viwanda.

- Masuala ya uendelezaji wa miundombinu kama yalivyoelezewa katika Sura ya 15 ya Mkataba huo wa Afrika ya Mashariki.

- Elimu na Mafunzo (Ibara ya 102) ya Mkataba huo

- Ibara ya 105 inayohusu chakula na usalama wake, mifugo (107) udhibiti wa maradhi ya miti na mifugo (108) na umwagiliaji maji (109).
- Mazingira (Ibara ya 177) ya Mkataba wa Jumuiya.

- Utalii na Wanyama Pori (Ibara ya 115), Afya (118), Mila na Utamaduni (119 na 120) na mengi mengineyo, ambayo yameelezewa kikamilifu katika Mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo nimeyaorodhesha hapo juu, yanahitaji uangalifu mkubwa jinsi ya kuyashughulikia. Hii ni kwa sababu Zanzibar inayotakiwa ishughulikie wananchi wake, imenyanganywa madaraka hayo na hivyo kuwa yanashughulikiwa na chombo kingine, yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambacho hakihusiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ni kuwa je, utata huu hautoifanya Zanzibar kukosa haki zake za Jumuiya? Kwa maana hiyo, hapatakuwa na mgogoro wa Jumuiya ndani ya Tanzania na hivyo kukuza matatizo au kwa jina maarufu, kero za Muungano ambazo hadi hii leo hazijapatiwa ufumbuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kuyatatua matatizo haya kabla hayajakomaa, baada ya kusawazisha hayo tuingie katika Jumuiya ikiwa sote tumefurahi. Jumuiya ni kitu kizuri, ambacho ni lazima tuwe nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matarajio mema ya baadaye kwa Jumuiya hii. Madhumuni ya Jumuiya yamewekwa bayana katika Mkataba wa Jumuiya, ikiwa ni pamoja na kuandaa mipango ya kuwanufaisha wananchi wa Afrika Mashariki ikiwemo Zanzibar na kuleta maendeleo na ustawi wa kisiasa, kiuchumi kijamii na kiutamaduni. Nayo sera mpya ya mambo ya nje Ibara ya 34, ukuasa 14 inayo maelezo na malengo hayo hayo yakiwemo kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hili ni zuri sana na likitekelezeka, Afrika Mashariki inaweza kupiga hatua kadhaa mbele. Lakini napenda kumpa Mheshimiwa Waziri, ushauri wetu wa dhati kwa faida yetu sote Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe na vyombo vinavyoweza kuwajibika. *Secretariat* ya Jumuiya ipewe uwezo zaidi wa kiutendaji, vinginevyo chombo hicho kitakuwa ni mzigo tu wa kutekeleza maagizo ya wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni lazima Tanzania iwe na utaratibu maalum, kwa vipi yale mambo yasiyo ya Muungano kwa Zanzibar nayo yatafanyiwa kazi moja kwa moja, kwa kuihusisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hii itaondoa malalamiko mengi ambayo hivi sasa yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ikiwa hapatakuwepo chombo cha udhibiti na uchukuaji hatua, basi Jumuiya hii itakuwa ni kama mbwa asiyekuwa na meno. Hii inatokana na sababu kubwa kuwa kila nchi itajipendelea kwa kiasi fulani. Hivyo basi, ni lazima kuwe na adhabu Fulani, pale ambapo nchi mwanachama haikutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kwamba suala la kuichukulia hatua nchi ni suala lenye mjadala mkubwa katika Sheria za Kimataifa, lakini walio wengi wanakubaliana kuwa, kuwepo kwa kanuni bila ya chombo kinachoweza kuchukua hatua kwa kuvunjwa kanuni hizo, basi huwa hakuna utendaji mzuri na wa maana katika chombo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Kambi yetu inahisi nchi wanachama hatujakuwa na ukweli. Mazungumzo marefu ndio yanayojitokeza kuliko ukweli wa vitendo. Fedha za michango huwa hazilipwi kwa wakati na hivyo kusababisha pengo kubwa la shughuli za utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo mengine yapo katika Mahakama na Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni kama vyombo hivi navyo vimepewa jukumu maalum la kuendeleza na kuharakisha ujengaji mzuri wa Jumuiya. Vyombo hivi vyote vimebanwa sana na uwezo wao ni mdogo. Kuna haja ya kuyatatua haya, kwa kuvipa uwezo mkubwa zaidi. Hivi sasa vyombo hivi vinahusika zaidi kama ni vyombo vya ushauri tu na kwa maana hiyo, huwa havina nguvu za kutafuna.

Pia Mahakama ya Rufaa, haina madaraka makubwa ya kushughulikia hasa matatizo ya wananchi wa Jumuiya hii, kinyume na matakwa ya wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna uhakika kwamba, matatizo yaliyojitokeza zamani na kusababisha kuvunjika kwa Jumuiya hii, yamerekebishwa kikamilifu. Woga huu ndio unaowafunga ile hamu ya nchi hizi kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo na ni lazima lisawazishwe kwa wananchi wa nchi hizi kuelimishwa na kutolewa woga huo. Elimu kwa raia hawa wa Afrika Mashariki ni muhimu sana na lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote na mengi mengineyo kama yatatafutiwa ufumbuzi uliokuwa mzuri, naamini Jumuiya hii itakuwa ni kioo kizuri cha kuwavutia wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba, Wizara hii itayaona hayo na kuyafanyia kazi kwa faida ya Tanzania na Watanzania wote. Dawa kubwa ya haya yote ni kujaribu kupitia upya Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya hii ili uweze kurekebishwa kulingana na hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu mwingine mkubwa ni kuhusu kutopewa muda maalum wa ukamilishaji wa shughuli hizo kama vile kupewa muda maalum wa miaka minne kuwepo kwa Umoja wa Forodha mara tu baada ya Jumuiya kuanza. Huu ni upungufu mkubwa katika mkataba huo na hivyo kuna haja pia ya kurekebisha kasoro hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ni vizuri kuwa na msimamo juu ya mwenendo unaotakiwa kufuatwa, kuhusu utekelezaji wa hatua mbali mbali za mtengamano ama kwenda hatua kwa hatua au kuzitekeleza baadhi na kuziruka nyingine. Hili linagusia suala la shirikisho kwa ujumla. Mimi binafsi na Kambi yangu, hatukubaliani na wazo la Dr. Kwame Nkrumah, alilolisema kwa kuanzishwa Umoja wa Afrika kwamba: *"Seek the political kingdom first, everything would be added to it."* Siamini kwamba, tutapopata Ufalme wa kisiasa wa shirikisho kwanza na mengine yote yatajileta yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi yetu inaamini na tungemshauri Mheshimiwa Waziri kwanza, kuwa na misingi madhubuti ya kiuchumi na ya kijamii ili utengamano wa kisiasa, ulio mzuri ufuatie baadae. Naomba Wizara nalo hili walifanyie kazi. Hasara tulizozipata, haraka zetu za kujiunga na Jumuiya zimetugharimu kidogo. Maana

tungeliweza kabisa kujiunga na Jumuiya kama Tanzania yenye nchi mbili na hivyo kila kitu kupata sehemu mbili. Hata Wabunge wa Afrika Mashariki basi ni rahisi kwa Zanzibar, ingelipata nafasi zake tisa na Tanzania Bara ingepata nafasi zake tisa. Hii ingelikuwa ni faraja kubwa kwa Watanzania. Pia kuna utaratibu wa mzunguko wa Maafisa Watendaji wa Jumuiya na hivyo pia tungelikuwa na nafasi mbili kwa Tanzania na kufaidi zaidi matunda ya Jumuiya hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la muhimu hapa ni kuwa, sisi kama Watanzania, basi tuingie kwa maelewano katika Jumuiya hii ili tuweze kuvuna zaidi. Kama kuna matatizo, basi yarekebishwe na kusawazishwa mapema ili tunapoingia katika Jumuiya, tuingie sote kwa nia moja. Ni vyema tukazitatua kwenye kero za Muungano ili nazo zisiwe kero za Muungano ndani ya kero za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu gani Tanzania haikuzungumzia juu ya kukuza usafiri wa bahari kwa miji ya mwambao kama vile Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Unguja, Pemba, Tanga Mombasa na Lamu? Ni kwa nini pakazungumziwa suala la *East African Road Network,* yaani *Tripartite Agreement on Road Network,* kwa kuunganisha nchi hizi tatu kwa barabara tu na ikasahauliwa usafiri wa baharini, kwa maeneo ya mwambao ambao ni wa lazima kwa wakazi wa maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shirikisho hili ni vyema pia sisi Watanzania tukajizatiti sana katika kupiga vita biashara za magendo baina ya nchi zetu hizi, hasa katika maeneo ya Tarakea, Lungalunga, Shimoni na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharakishwaji wa Shirikisho *(Fast Tracking),* mtengamano wa kiuchumi na kisiasa ni jambo ambalo haliwezi kuepukika katika dunia hii ya leo. Kwa maana hiyo ni vizuri kufupisha muda wa kufikia shirikisho kamili, lakini kwa misingi niliyoielezea hapo juu. Misingi hii ni pamoja na kusoma kutokana na makosa yetu tuliyoyafanya wakati wa Jumuiya hii hapo awali na sababu za kufa kwake. Vile vile ni vyema kuyatatua matatizo niliyoyaainisha hapo awali, yaliyopo ndani ya Tanzania yetu na yale yaliyopo nje ya Tanzania yetu ili tuweze kuwa na shirikisho zuri na la kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ni lazima kwa vyovyote vile, wahusishwe wananchi mbalimbali na taasisi mbalimbali ili waweze kutoa maoni yao na pia kueleweshwa zaidi kwa ajili ya kukijenga na kukiimarisha chombo hiki cha Jumuiya, ambacho ni muhimu sana. Hayo tunaamini kwamba, nayo yatarahisisha katika kujenga Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu nami kutoa maoni yetu ya jinsi ya kuiimarisha Jumuiya yetu. Naamini mawazo yangu na ya Kambi yetu, yanaweza kusaidia katika kujenga vyema Jumuiya yetu hii. Ni wajibu wetu sote kuyaona matatizo hayo na kuyashughulikia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kusema kuwa, tutaunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ikiwa maoni tuliyoyatoa, yatatiliwa maanani na

kufanyiwa kazi kwa faida yetu Watanzania sote na kwa faida ya Jumuiya yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na ninasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, ninakushukuru sana kwa kutoa taarifa hiyo ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea sasa na mchango wa jumla, ninaomba nimtambue Mheshimiwa Hulda Stanley Kibacha, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwamba, yeye yuko hapa ndani, yupo pamoja nasi leo. *(Makofi)*

Lakini ninawaomba niwatambue mbele yetu, wachangiaji ambao wameshawasilisha maombi ya kuchangia hoja hii hapa Mezani, kwa utaratibu ambao wameleta maombi yao na ninaomba kama wapo nje ya Ukumbi wa Bunge, basi wakisikia warudi ndani ili waweze kujiandaa. Tutaanza na Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, atafuatia Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Balozi Hamis S. Kagasheki, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na mwisho tunaye Mheshimiwa Manju S.O. Msambya. Kwa hiyo, nawaomba hao wajiandae na hiyo ndiyo orodha ambayo imefika Mezani kwangu mpaka sasa hivi.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru sana, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niungane na wenzangu waliotangulia kuchangia hoja hii ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuona umuhimu wa kuunda Wizara, ambayo italiangalia suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki na ushirikiano huu wa Kikanda kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukua nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Andrew J. Chenge, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala na uongozi mzima. Ninaamini ni watu ambao wataichukua Wizara hii kwenda mahali ambapo tunatarajia iende. Wana kazi kubwa sana ya kuandaa uwezo wa Wizara wa kiufundi na kiutendaji ili iweze kufanya kazi ambayo inatarajiwa katika Afrika yetu ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba pia niseme kwamba, Mkataba wa Afrika Mashariki ni mzuri. Nafikiri wakati umefika kwa nchi yetu, kutosita kwenda katika Shirikisho la Afrika Mashariki na badala yake tujiandae kinagaubaga kuhakikisha kwamba, tutakuwa na faida katika kuwa wanachama wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili wazo la *Fast Tracking* ya *East African Cooperation* kutoka kwenye Ushirikiano wa kiuchumi na kuingia kwenye ushirikiano wa kisiasa na Shirikisho. Nafikiri ni wazo zuri, lakini ningependa wananchi wa kawaida washirikishwe kiasi cha kutosha ili tutakapofikia wakati wa Shirikisho, isiwe tu ni suala la viongozi wachache waliamua. Lakini wananchi wetu wote wapate nafasi ya kushiriki katika maamuzi ya litakalokuwa Shirikisho la Afrika Mashariki, ikiwa ni pamoja na kuangalia nchi ambazo zimeomba (Rwanda na Burundi). Wengi wanazungumzia uwezekano wa *DRC.* Nafikiri Afrika Mashariki kubwa itakuwa ni nzuri kwa Tanzania. Sasa hivi watu milioni 90, inakadiriwa baada ya miaka kadhaa Afrika Mashariki itafikisha watu zaidi ya milioni 100 na soko la watu milioni 100 ni zuri kwa uchumi na kwa maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme suala la Zanzibar, kwa mawazo yangu litazamwe, ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndiyo maana katika Bunge hili, tunao Wabunge wa Zanzibar. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kimsingi lina wajibu wa kuangalia maslahi ya nchi kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tukifika mahali tunataka kila kitu kiende kama nchi mbili tofauti, hata dhana nzima ya Muungano haitakuwa na sababu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wenzangu wa Kambi ya Upinzani, hilo lisiwape shaka. Wajue kwamba, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla wake, inazingatia maslahi siyo tu ya Zanzibar pekee yake, bali ya kila mwananchi na ya kila Mkoa na Wilaya katika Jamhuri hii Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie sasa juu ya suala la maslahi ya nchi, inapoingia kwenye Jumuiya kama mshindani. Ningependa nitoe angalizo kwamba, kila nchi katika hii Jumuiya, ina maslahi yake. Kuna sababu Uganda kukubali kuwa mwanachama wa Afrika Mashariki, kuna sababu Kenya kukubali kuwa mwanachama wa Afrika Mashariki na kuna sababu kwa nini Rwanda na Burundi wanaomba kuwa *members.* Kwa sababu jambo la kwanza ni maslahi ya nchi inayohusika na sisi kwa kwenda katika Jumuiya ya Mashariki Afrika, jambo la kwanza ni maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kabla ya maslahi ya mtu mwingine yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wenzangu katika hii Wizara, wapate nafasi ya kuangalia *strategic interest* ya nchi yetu zinalindwa vipi. Kuna suala linalojitokeza sasa hivi juu ya uwiano wa nguvu za kijeshi katika nchi hizi za Afrika Mashariki. Watu wengine wanaweza wakafikiria hilo halina maana wala halina sababu, lakini siku akitokea kichaa mmoja katika baadhi ya nchi akawa Rais na akaamua kuwageuka na kwa sababu ninyi mlikuwa mmemwamini kwa asilimia 100, anaweza akawashangaza usiku wa manane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *military balance* katika Afrika Mashariki haina uwiano kabisa. Nafikiri Serikali inajua zaidi ya sisi *back benchers* tunavyojua. Ukiangalia Uganda, *military equipments superiority* na ukahesabu wao wana *helicopter* na *ships* ngapi za Kijeshi, *potential* ya *positio*n ya *mini size* za Kijeshi zinazoweza kurushwa na kupiga Mji wa mbali wanazo ngapi; *short range* na *long range* wana ndege

ngapi za kivita zinazoruka? *Potential* ambayo inaweza ikarushwa na sisi tuna *lead capability* kiasi gani inayoweza ku-*monitor* wenzetu wanafanya nini kijeshi? Rais maarufu sana wakati wa *Cold War,* Leonard Regan, alikuwa amekubaliana na *Soviet Union* kwamba, sasa tupunguze silaha za nyuklia, lakini akaja na msemo unaosema *trust but verify* na hakuna tatizo sisi kumwamini kila mtu katika Afrika Mashariki, lakini *we must verify*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake, aniambie Waziri wa Afrika Mashariki anafahamu nini kuhusu *standing army capabilities* za nchi zinazotuzunguka? Wanajeshi wangapi walio na uzoefu kiasi gani katika *combat,* dhidi uwezo wetu kama Tanzania, kwa sababu katika nchi zinazowazunguka, lazima nchi ambayo ni huru, iangalie uwezo wake wa kijeshi. Kwa sababu hilo ni suala la kwanza la uhuru wa nchi, ambalo kila mwenye nchi ahakikishe kwamba anao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Uganda, wana *factor* nyingine imekuja ya mafuta na itabadilisha sana *balance* ya mapato. Kwa sababu mafuta waliyogundua Uganda, wataalam wanasema yatawawezesha kwenda mbele kuliko ilivyokuwa mwanzo na sisi tunajiandaa vipi ku-*compete* nao? Ni wenzetu ndiyo, lakini tujue kwamba, tuna majirani ambao pia wana *interests* zao na mara nyingi sio vizuri kusema kwamba, tunashirikiana halafu ukamuacha mtu anafanya anachofanya bila wewe kuangalia *strategically,* yeye anachofanya kitakuathiri nini wewe katika nchi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika duru za watafiti, Rwanda inatajwa kwamba ni moja ya nchi ambayo imekamilika sana kivita katika Afrika ya Mashariki na ya Kati. Uwezo wa Jeshi, *intelligence capability* ya ndani kuweza kuangalia Tanzania mnafanya nini, *may be* wanatujua zaidi tunavyowajua, mna nini hamna nini. Kwa upande wao kwa sababu wamekuwa katika malumbano na vita vya ndani kwa ndani kwa muda mrefu, wamefika mbali. Napenda tujue ugomvi wa Uganda na Rwanda, ambao hauishi na wote tunajua ni *personality conflicts,* unaweza ukaathiri vipi Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala madogo lakini unapokuwa na ushirikiano haya sio masuala madogo. Haya ni masuala ambayo *potentially,* yanaweza yakaingiza nchi mahali pagumu sana kama hatujajiandaa, hatujayajua. Ni nani ambaye ana-*supply* silaha na vifaa vya nchi ya Rwanda? Ni kiasi gani *capability* yao? Kwa upande wa Kenya tunafahamu kwamba, wao wana *Strategic Military Corporation* na US wana *US Base.*

Kuna mtu mmoja alisema kwamba, Wamerikani wamekata misaada Kenya wala sio kweli. Kwa sababu misaada mingi inatolewa na Jeshi na haitangazwi, inabadilisha *balance* ya nguvu za kijeshi na hatujajua kwamba, wanasema *in order to be interdependent, you must be independent.*

Mimi ninachotaka kuzungumzia ni *interest* ya nchi yetu. Tutajizatiti kiasi gani kuwa *independent* kama nchi? Zamani sisi tulikuwa tunategemea sana China, lakini China wana *new deal* na Kenya kupitia bandari ya Mombasa ambayo ina-*jeopardised*

Bandari ya Tanga. Uwezo wetu wa kuweza kuifufua Bandari ya Tanga utapungua kwa kiasi kikubwa sana, kama makubaliano ya China na Kenya kuitumia Bandari ya Mombasa yatafikiwa. Reli inayotoka Mombasa kwenda Nairobi, imepata mbia kwa kushirikiana na Uganda, ambayo ita-*affect possibility* ya sisi kuwa na reli kutoka Tanga kupitia Serengeti kwenda Victoria, kwa ajili ya kukamata soko la Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni vitu ambavyo lazima tuviangalie. Hivi karibuni *University of Kenyatta* walikuwa *assigned* kufanya *study* juu ya *Tanzania competitiveness economically*. Kazi yao ilikuwa kuangalia *competitiveness* ya Tanzania katika miaka kumi kiuchumi itakuwaje? Lengo ili wakae, kwa sababu mnapokuwa mnashirikiana kama Shirikisho, kila mtu ana *interest* yake kuhakikisha kwamba, watapata *maximum utilisation* ya huu uchumi na kitu ambacho napenda na sisi tuangalie. Sasa hivi macho ya Kenya na Uganda yote yako Jubbah, kwa sababu *Southern Sudan* wamekuwa na *The Government of Southern Sudan* wanashirikiana kwa mafuta na *Northern Sudan*. Kwa hiyo, *in terms of financial liquidity,* wana fedha. Kwa hiyo, biashara nyingi sana za Nairobi, *consultancy* na kuuza vitu vingi vimeelekezwa Jubbah. Napenda tuangalie Tanzania inaweza ikafaidi vipi *the coming of the Southern Sudan,* ambayo Nairobi wanazungumzia kwamba, kama *Southern Sudan* watashindwa kuelewana na Sudan, itabidi wawavute haraka sana waje Afrika Mashariki. Lengo ni kuhakikisha kwamba, wanauza vitu vingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sio kuzungumzia hofu ni kuzungumzia umuhimu wa sisi kujiandaa, umuhimu wa sisi kuangalia ndugu zetu wanafanya nini, hasa katika nyanja muhimu sana za kiusalama. Nina uhakika hatujaweza kufika mahali tushirikiane juu ya *military intelligence,* tujue *exactly* adui zetu wa nje wa pamoja ni nani lakini na wale wa ndani. Kwa sababu demokrasia hizi zote ni chama. Wewe utashangaa nchi inaamua, Rais anaamua kwenda kumwingilia mwenzake kwenye uchaguzi ili atoke. Tuna tatizo ambalo ni lazima tuhakikishe kwamba, pamoja na kwamba tunajiandaa na ushirikiano wa Tanzania, lazima ifanye mambo yafuatayo: La kwanza, lazima tujue hawa wenzetu wamejiandaa nini katika kila eneo, wanategemea kufaidi hii Jumuiya katika njia zipi? *Competitiveness strategy* zao wanazoziandaa ili waweze kutushinda kibiashara ni zipi, kuanzia kwenye *receipt* za utalii?

Kila mtu anafahamu kwamba, kwa sababu hatujatangazwa kiasi cha kutosha, Nairobi imetengenezwa kuwa *hub* ya Afrika Mashariki na ya Kati. Kwa hiyo, kila mtalii anayekuja Tanzania ataambiwa kimsingi upite Nairobi kwa sababu zifuatazo: Kwanza, *it is cheaper,* wamehakikisha hata mafuta ya ndege ukili-*fuel* Nairobi ni *cheaper* kuliko kuja ku-*fuel* Dar es Salaam. Hizo ni *strategies* tu wamefanya. Kwa hiyo, ndege nyingi zaidi *naturally* zita-*fly into* Nairobi, wameambiwa *landing fees* Nairobi ni *cheaper* kuliko uki-*land* Kilimanjaro kwa mfano. Kwa hiyo, *as a result* watu wanaambiwa kama unataka kwenda Tanzania sawa mzee, lakini uanzie Masai Mara na wanawaambiwa *by the way* Masai Mara na Serengeti zimeungana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hii hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nichangie katika Wizara hii mpya ya Afrika ya Mashariki, lakini ni muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Ofisi yao, kwa kutuletea hotuba hii nzuri, ambayo tunachokifanya hapa ni kuirekebisha ili malengo ya jumla ya Wizara yenyewe na nchi yetu kwa ujumla, yaweze kufikiwa. Niseme tu tunatoa fikra hapa kwa sababu ya kujenga zaidi na sio kwa sababu mtu anasema kwa ajili ya ubinafsi au nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa kusema kuwa, mchango wa fedha ambao unatakiwa kutumika katika Wizara hii ni mkubwa kuliko fungu walilopewa. Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri hapa, ameeleza kuwa moja ya majukumu yao ni kuwafikia wananchi na kupata maoni yao juu ya nini hasa kiwe katika Shirikisho hili la Afrika Mashariki. Hilo peke yake, linahitaji fedha nyingi. Hawa watu imeshasemwa hapa, hata ofisi hawana mpaka sasa, halafu tunawatengea shilingi bilioni saba. Nafikiri kweli kwa mara hii labda ndiyo bajeti imepita, lakini tuna haja ya kuongeza mchango mkubwa katika Wizara hii kwa sababu ina majukumu ya kufikia mwananchi mmoja mmoja. Watanzania wamechawanyika sana katika nchi yao, ukitaka kweli kupata maoni yao ni lazima uwafikie. Sio uende katika mji uchukue sampuli ya watu, matokeo yake useme asilimia 80 au 90 italeta malalamiko yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mimi nasema tusiwe na woga, inaonekana tuna tabia sisi Watanzania ya kuogopa ogopa mambo hivi. Tumeamua kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, tuingie. Tukishafikia *point of no return,* hatuwezi kusema kuwa tunakataa, hatuwezi kukataa leo tukasema hatutaki Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunahitaji matayarisho basi na matayarisho haya kama hatukuyafanya kikweli kweli katika nyanja za kuwasomesha vijana wetu, katika nyanja za kuimarisha vyombo vyetu vya ulinzi vya kuimarisha mipaka yetu, kuimarisha biashara zetu, hatutafika huko, itakuwa yale yale tukifika tunasema wenzetu wa Kenya, wenzetu wa hapa, lakini kosa ni letu wenyewe.

Wakati mmoja mimi nilihudhuria semina, tukagawa vikundi hivi. Sasa katika utangulizi ikawa kila kikundi kichague Mwenyekiti wake. Nilicheka sana, kwa sababu katika vikundi sita, Wenyeviti wote waliopewa nafasi katika vikundi vile walikuwa ni Wakenya. Tunazungumzia *fast truck integration,* lakini mimi ikanijia kwamba, hii sasa ni *Kenyan domination in East African Intergration.* Kwa sababu wote wamekuwa Wakenya. Ni *incidence* iliyotokea, lakini utakuta wamechaguliwa watu pengine kwa sababu ya uwezo wao, kwa sababu wanaweza kuwa na ushawishi fulani katika vikundi vyao. Sasa haya haya yanaweza yakatupata, ni lazima tuwasomeshe watu wetu mapema. Leo hii hatujafikia huko, lakini ukiangalia katika mahoteli karibu yote ya nchi yetu, ukiiangalia ile *staff* basi utakuta asilimia 70 au 65 ni watu kutoka Kenya. Ni kwa sababu watu wanapotangaza soko, wanatazama uwezo wa mtu, hawatazami huyu anatoka wapi? Akimwona mtu ana *Hotel Managem*ent ndiye atakayemwajiri kuliko mtu ambaye anamjua tu kwa sababu ni jamaa yake. Sasa lazima tuwasomeshe watu wetu ili

tuwatayarishe kuingia katika Jumuiya hii muhimu, lakini yenye uzito mkubwa kama tutakuwa tuko wengi.

Tatu, ni uzalendo. Mimi nafikiri pia tunapaswa kuwa wazalendo. Sioni sababu mtu anakataa kutumia sabuni ya Foma, kwa sababu inatoka Tanzania na anaona lazima apate sabuni ya Omo inayotoka Kenya, eti ndiyo atakase nguo zake. Nadhani kama kuna tofauti kubwa. Tujenge uzalendo wa kupenda bidhaa zetu na wa kuimarisha viwanda vyetu ili tuweze kuwa kweli washindani katika Jumuiya hii. Tunaona sote hapa kuwa leo katika sera yetu mpya, tunauza viwanda vingi na watu hawa wanaonunua viwanda wengine hata hawazalishi zile bidhaa ambazo zinakusudiwa, ndiyo kama tumesikia hapa juzi katika Wizara ya Biashara, watu wameshanunua viwanda wanaviacha tu *dormant,* vingine havifanyi kazi, wengine wanakongoa kongoa vitu, sasa yote haya *in the long run,* yanaweza yakatuumiza sana. Kwa sababu kama hatuwezi kuzalisha kwenye viwanda, hii biashara tutaifanyaje? Itakuwa ni yale yale, sisi tunaingia lakini kuwa soko sasa, lakini pia ni kuimarisha vyombo vyetu vya utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi katika nchi yetu yenyewe ukiangalia wafanyabiashara wengi, wanashusha bidhaa zao katika Bandari ya Mombasa, *simply* kwa sababu pale hawasumbuliwi. Akileta biashara Dar es Salaam, gari linaweza likakaa katika *long room* kwa muda wa siku 21 au zaidi, nenda rudi, nenda rudi, mfanyabiashara gani ambaye anataka kufanya faida atataka usumbufu huo. Sasa haya yote ni matatizo ambayo tunapaswa kuyaangalia wenyewe kwanza, kabla ya kusema kuwa wenzetu watatutawala, wenzetu wamesoma, hapana. Haya mengine hayahitaji kusoma, yanahitaji uwajibikaji tu. Watu walioko katika vyombo muhimu wawe waangalifu sana, wawe na uwajibikaji ambao utaifanya nchi yetu iwe *very serious* katika mambo yake, matokeo yake watu wata-*opt* wenyewe tu. Hana sababu mtu apitishe mzigo wake Tarakea kuja nao Dar es Salaam, ikiwa anatumia siku tatu kule na Dar es Salaam atatumia siku tatu. Sidhani kama atafanya hivyo ni kwa sababu wenyewe hatujawa waangalifu katika mambo haya. Sasa zote hizi ni changamoto, ambazo tunatakiwa tuzikabili kabla ya kuingia kwenye Jumuiya hii ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa rasilimali muhimu kwa mfano, ardhi, watu wanasema ardhi yetu isije ikachukuliwa, hivi sasa inachukuliwa. Watu wananunua ardhi hivi sasa. Kama Wizara hii watatumia *machinery* yao, wakafanya utafiti, utakuta ardhi nyingi katika sehemu hasa za mipakani, hata hapo Dar es Salaam, tayari watu kutoka nchi nyingine wameshanunua ardhi na wananunua kwa kujiandaa kuja kuitumia baadaye, wakati wa hiyo *federation* ambayo tunaitegemea.

Sasa yote haya ni mambo ambayo tunapaswa kujitayarisha nayo, ikiwa tunataka kweli maendeleo ya nchi yetu, ikiwa tunataka usawa wa nchi yetu katika Jumuiya hii nzuri sana ya Afrika ya Mashariki. Watu wanachokizungumzia, ghafla mtu anakuambia tusainishe mambo haraka, yaani tuweke mambo wepesi, kwa haraka ili watu wapate kuja, msingi wake mkubwa ni biashara tu. Wanataka watu waje wafanye biashara, waje wanunue bidhaa, walete bidhaa na matokeo yake, wao waweze kunufaika zaidi kuliko sisi.

Mimi nilipata bahati mwanzo wa kuasisiwa jambo hili, nilikuwa Arusha siku hiyo. Wakenya walileta watu karibu 250, Waganda walileta watu kama 140, Watanzania tulikuwa kidogo sana. Wabunge tuliokuwa pale tulikuwa kwenye Kamati tukaambiwa twende angalau tuongeze ile sura ya Watanzania waliopo. Sasa unanipeleka mimi Mbunge niende nikaangalie, mimi sio mfanyabiashara wala sielewi habari hizo. Sasa haya mambo ya kujidanganya danganya wenyewe, hayatutasaidia sana ni vizuri tukawaelimisha watu wetu, wakawa *very serious, very competitive,* tukaweza kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa nguvu ambayo inahitajika na itakayoweza kuwasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeulizwa suala hapa pana, hoja hii ya Zanzibar. Mimi nafikiri tujiulize tulikuwa na Muungano tokea mwaka 1964 na Jumuiya ile ya mwanzo ya Afrika Mashariki ilivunjika mwaka 1977. Tulikuwa wakati ule nchi mbili tulipata hasara kwa kuwa nchi mbili? Tungejiuliza hivi tulipata hasara kwa kuwa nchi mbili na sasa tunapata faida kubwa kwa kuwa Zanzibar haina uwakilishi wake binafsi? Huko mbele tunakokwenda, tunakwenda kwenye *federation,* ikifikia hapo kwa maoni yangu mimi, basi ndiyo itakapoumia hasa Zanzibar kama nchi, itaumia sana. Sasa hivi tunapeleka Wabunge tisa, amesema hapa Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na wengine watasema pengine. Kama ingelikuwa tunakwenda kama nchi mbili, kama tulivyokuwa katika Jumuiya ya kwanza, tungelipeleka watu 18. Sasa hivi kweli tisa na 18 wanalingana? Yote haya ni mambo ambayo tunapaswa kujiuliza na lazima tukubaliane kuwa sisi katika nchi yetu wenyewe tuna makubaliano ya Muungano.

Yako mambo ambayo ni ya Muungano na yako mambo ambayo si ya Muungano. Sasa haya ambayo si ya Muungano katika Jumuiya hii mpya ya Afrika Mashariki, yatashughulikiwa vipi? Sote tunaona hapa sasa hivi kuna mipango chungu nzima, lakini kila anayesimama hapa atahoji mara asilimia 4.5, mara atahoji hivi, kwa sababu tayari tuna matatizo yetu wenyewe ndani. Ni vizuri tukayatatua kikweli kweli, tukaangalia upya ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya hii ili tukiingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki, tuwe tuna nguvu ya kikweli kweli kama nchi. Hayo ni moani yangu na mimi nayatoa kwa nia safi kabisa, wala sikusudii kujibu kwa sababu mwenzangu amesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna suala hili la kudhibiti rasilimali. Mimi natoka sehemu za Mwambao wa Bahari ya Afrika Mashariki na pia ni mvuvi, maana yake kuna baadhi ya siku nakwenda pwani mimi mwenyewe. Inatisha sana kuona meli za kigeni tena za kutoka Kenya, zinavua katika Mwambao wetu kila siku. Halafu ni wajanja sana, kwa sababu kama pale Pemba Kaskazini, kuna Kampuni fulani imekata leseni ya kufanya hoteli hizi *Aflot*, ni meli fulani zinakaa wanakuja watalii wanaingia kwenye meli wanafanya *diving,* ni ujanja tu zile zinakuwa hoteli mchana lakini ukiwafuatilia usiku, wanachokifanya ni kuzamia chini ya bahari kuvua na kuchukua matumbawe, pale sehemu walipo pana matumbawe ambayo hapana katika sehemu nyingine yoyote katika dunia nzima, yapo pale. Ikifika usiku wanaingia na *drill* wanakata wanachukua. Huo ni wizi kabisa na ukiwaambia watendaji wa Serikali wao wana *trivialize,* wanaona *it is a minor issue*. Lakini *it is not a minor issue,* kwa sababu unaharibu uchumi wa nchi kwa kutojali mwenyewe thamani ya rasilimali yako.

Jana nilipokuwa nikiangalia ile picha, nilishtuka sana, nikaona hawa watu wa ajabu sana. Wewe unafanyaje Kiwanda cha Samaki, halafu unaharibu mazingira kwa kiwango kile. Sisi ni wanyonge, ukikuta kitu ukaona kinakufaa utachukua, hivi hawakuweza wawekezaji hawa kuhifadhi ule uchafu wao unaotoka viwandani mpaka wawatupie wananchi wale na sisi tunakubali wanafanya vile, tunawaona wanatupa tunakubali tu tunanyamaza kimya? Matokeo yake wanatuharibia mazingira, wanaharibu kila kitu na vyote hivi ni vitu vya kuangalia.

Bahari zetu hizi au hata hawa samaki wanaovuliwa leo, tuna nchi moja moja utakuta pengine Tanzania labda sehemu yetu kwenye Ziwa Victoria na kwenye bahari, tunao wengi lakini wenzetu wa Kenya na Uganda kwa jinsi *speed* waliyowavua wameshafikia pahali pabaya sana. Tukifanya shirikisho kesho utakuta wanamaliza kila kitu. Mambo yote haya ni ya kujiuliza, tunadhibiti vipi rasilimali hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, umoja wowote ni muhimu sana lakini ili uingie katika umoja na uwe na haki inayofanana na wenzako, lazima uwe umejitayarisha vizuri.

Naomba sana Serikali yetu kwa nia safi kabisa, iwatayarishe Watanzania kikweli kweli katika kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki. Vinginevyo tutakuwa ni watazamaji badala ya kuwa ni wachezaji katika mechi hiyo muhimu.

Nakushukuru Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja hii. Lakini shukrani zaidi ni kwa kunikubalia ombi langu, kwa sababu kama nilivyoeleza nina dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nitamke kwamba, naiunga mkono hoja. Lakini pamoja na kuunga mkono hoja, nina mambo matatu tu ya kuchangia na inawezekana nikachukua muda mfupi sana. Jambo la kwanza, liko kwenye jalada la kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Jambo la pili, liko ukurasa wa 36 nalo linahusu maombi ya Rwanda na Burundi na jambo la tatu ni ukurasa wa 37 mpaka 42 nazo ni changamoto ambazo Mheshimiwa Waziri, ameziainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na changamoto. Niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 42, ibara ya 48. Kwa idhini yako naomba nisome sehemu ya yale aliyoyasema. Amesema: "Mheshimiwa Spika, pengine changamoto kubwa kuliko zote zilizo mbele yetu katika mustakabali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni namna ya kupunguza au kuondoa tofauti iliyopo ya viwango vya maendeleo kati ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki." Mimi sidhani kama hii ndiyo changamoto kubwa kuliko zote. Kwa maoni yangu, changamaoto kubwa kuliko zote na haikuainishwa katika zile ambazo zingetakiwa kuanishwa ni elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji wa kwanza kuhusu hoja hata wa pili, wamezungumzia suala la elimu na ambalo linapelekea Watanzania kupata ajira katika Jumuiya. Mimi nilidhani Mheshimiwa Waziri, angezungumzia kwamba, changamoto kubwa kuliko zote ni elimu ambayo inatunyima sisi nafasi. Inatunyima ushindani wa

kutosha Watanzania sasa tunaingiaje? Serikali imetoa kauli majuzi hapa, wakati wa mchango wa Wizara ya Elimu ya Juu ni watu gani watatakiwa kupata ufadhili wa Serikali. Sasa kama tunatoa ufadhili kwa mafungu, hivi kweli tuna nia ya kuwaelimisha wananchi wetu waweze kuingia kiushindani katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki? Kwa maoni yangu nasema, Mheshimiwa Waziri angeweka changamoto kubwa kuliko zote, Serikali yetu kuhakikisha inatoa fursa yao vijana wetu wa Kitanzania, wapate elimu ili waweze kwenda kushindana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hilo nimeona niliseme kwa ufupi na nadhani Serikali itakuwa imeelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nadhani ndiyo hasa kiini cha mimi kuomba kuchangia ni hili lililoko kwenye ukurasa wa 36 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri; maombi ya Rwanda na Burundi kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mimi nilidhani kwenye masuala mazito kama haya, yasianzie na kuishia kwenye Vikao vya Kiserikali na uamuzi ukachukuliwa huko. Suala zito la Burundi, Rwanda au nchi nyingine kujiunga na sisi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, lingetakiwa tulifanyie *referendum*. Sisi wenyewe tukiwa hapa kama Afrika Mashariki ya nchi tatu, unasikia michango ya Wabunge humu wanahoji pengine hawa wanatuzidi hiki au watakuja kutugandamiza kwa hiki. Rwanda na Burundi kujiunga na Jumuiya hii, mimi binafsi ningeulizwa ningesema hapana.

Ningesema hapana kwa sababu hawa kwanza, kwao hawajatulia. Sasa tunataka ku-*import* matatizo ya Rwanda na Burundi, yaje yajumuike na matatizo yetu sijui tutaishi vipi? Hawa ni *expansionist,* matatizo yaliyoko *Eastern Congo* yanasababishwa na watu hawa. Sisi tulioko Kigoma tunafahamu. Pengine matatizo mengine ya kisiasa yaliyoko kwenye maeneo ya mipakani, yanasababishwa na watu hawa. Leo tunawakubali hawa wajiunge na Jumuiya ya Afrika Mashariki, maana yake tuna-*import* matatizo ya kutoka kwa wenzetu hawa, yaje yawe ni sehemu ya matatizo yetu sisi. Watanzania, hawaulizwi Serikali inaamua kivyake tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama ni sahihi. Waswahili wanasema "Mkataa wengi ni mchawi," lakini hukaribishi wingi wa namna hii. Ukikaribisha wingi wa namna hii, wewe ndio unakuwa mchawi. Kwa sababu unamkaribisha mtu ambaye atakuja hapa kwako akuvuruge, atahamisha matatizo yaliyoko kwake alete kwako wewe. Sasa namwomba Mheshimiwa Wazirin kwa sababu nasema kama ilivyo kwenye ibara hiin huu ukurasa wa 36 hizi ni hatua za kwanza mlizofanya. Naishauri Serikali itafute maoni ya Watanzania kuhusu hili na pengine muwaambie wenzetu wa Kenya na Uganda, nao kwao wafanye *referendum* vilevile. Hili si suala jepesi, tunawakaribisha watu ili waje wajiunge na sisi halafu watatuletea matatizo yao. Nimezungumzia sisi tulioko Kigoma tunalielewa hili. Wanakuja Warundi, Wanyarwanda na kwa sababu lugha wanayozungumza na sisi ni lugha zinazofanana, kwa kule Kigoma Kirundi na Kiha tofauti yao ni lafudhi tu, Mrundi anasema "R" Muha anasema "L". Wamejipenyeza wameingia mpaka kwenye baadhi ya vijiji, ni Wenyeviti wa Vijiji na ni viongozi, wanavuruga amani iliyoko katika maeneo yetu. Sasa mnawakaribisha kama nchi, itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itafakari kwa kina, sana suala hilo la kuwakaribisha hao watu kujiunga na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Tunapenda wingi,

tunapenda umoja. Tuliambiwa hapa Bungeni siku moja kwamba, hata Ulaya pamoja na uwezo walionao, wanaji-*group* pamoja, wanaongeza wingi ndiyo maana wanapata ile *European Union*, sawa. Lakini ninyi wenyewe ni mashahidi, mnaona wanavyosuasua kuzikubali baadhi ya nchi katika *European Union,* ni kwa sababu wana mashaka na nchi hizo. Sasa sisi tusikubali tu watu wakajiunga na baadaye wakatuletea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kama nilivyosema nitachangia kwa muda mfupi, niende kwenye jalada la kitabu hiki. Kama sikosei, yameulizwa maswali mengi hapa kuhusu na inawezekana hili halimhusu sana Mheshimiwa Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini kwa sababu limetokea kwenye kitabu chake, inabidi nilieleze. Yameulizwa maswali kadhaa Bungeni hapa, kuhusu mpaka wetu sisi na Malawi kwenye Ziwa Nyasa. Sasa Mheshimiwa Waziri, tazama mipaka iliyomo kwenye Maziwa matatu makubwa yanayotuzunguka sisi. Ziwa Victoria mpaka umo ndani ya maji, Ziwa Tanganyika mpaka unakatiza katikati ya Ziwa, lakini kwenye Ziwa Nyasa mpaka uko upande wa Tanzania. Hivi watu wa Malawi wakisema kweli huu ndio mpaka halisi, mtakataa? Naambiwa ni ramani ya Malawi, lakini imechorwa kwenye kitabu kinachowasilishwa na Waziri kwenye Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema hili linaweza likaonekana kama jambo dogo na wenzetu wanaweza wakachukua hii kama hoja. Sasa wakati mwingine ni vizuri tunapoangalia vitu kama hivi, kwetu sisi hii ni *document* halali, leo *document* halali ina mpaka unaopotosha ukweli wa mipaka ya nchi yetu. Sasa tunaweza tukalichukulia kipuuzi puuzi hili, lakini sio la kipuuzi hili. Mtu wa Malawi akichukua hiki kitabu, anasema Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ametusaidia sisi wa Malawi kujenga hoja mpaka wa Malawi tutakatalia wapi? Nilikuwa naomba tunapotayarisha vitu kama hivi, tuwe makini sana. Sisi tunajenga hoja mpaka wetu na Malawi ni katikati ya Ziwa Nyasa na ubaki hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, niliomba ombi maalum nichangie mapema kabla ya muda ulionipangia na hoja zangu zilikuwa hizo tatu na baada ya kueleza hayo, namweleza tena kaka yangu Mheshimiwa Andrew J. Chenge, asiwe na wasi wasi mimi naunga mkono hoja, lakini ilibidi nieleze hayo ambayo niliyoyaona yanafaa kufikishwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** *Bismillah Rahman Rahym.* Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nichukuke nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii na mimi kuwa mmoja katika wachangiaji katika hoja iliyokuwepo mbele yetu.

Kwa kweli nilikuwa sina mengi sana ya kuyazungumza, hasa tukizingatia kwamba, ingenibidi nirudie rudie. Lakini kabla sijaanza mchango wangu, ningeomba nitumie nafasi hii kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi hiki, kwa uamuzi wake sahihi wa kuanzisha Wizara hii na akamteua Mheshimiwa Andrew J. Chenge, pamoja na Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala kuwa, ndio Viongozi wa Wizara hii katika kuendeleza gurudumu la Jumuiya hii ya Afrika Mashariki.

Nawapongeza sana na nawatakia kila la kheri pamoja na viongozi wote wa Wizara hii, ambao katika muda huu, naamini watakuwa na kazi ngumu na kubwa ya kuhakikisha kwamba, Jumuiya hii inafikia malengo yake iliyoyakusudia ya kufikia Jumuiya kamili ya Shirikisho hili la Afrika ya Mashariki.

Vile vile, kabla sijaenda mbali, naomba nichukue nafasi hii, kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoelewa, duniani kama kuna jambo ambalo ni la kulizingatia na lakulifikiria katika dunia hii tuliyokuwa nayo ni umoja. Mtu anapokuwa na umoja na akaweza kuutekeleza umoja ule, nasema amefanikiwa katika dunia yetu hii ya leo na hata iliyopita na inayokuja. Kwa hiyo, kuanzishwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki, nafikiri hili ni jambo la busara na Watanzania wote hatuna budi kuliunga mkono, kwa hali yoyote itakavyokuwa ili tuhakikishe kwamba, tunafanikisha suala hili.

Lakini pamoja na yote hayo, ningependa nipate ufafanuzi kidogo kuhusiana na suala hili la Jumuiya hii ya Shirikisho la Afrika Mashariki. Tukingalia katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 10 fungu la 12 (i) naomba kunukuu: "Wizara itajielekeza katika mambo yafuatayo: Kuratibu kwa karibu utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya vyombo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukiwemo Mkutano wa Wakuu wa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Baraza la Mawaziri, Bunge na Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa suala hili, kwenye Bunge lako hili Tukufu, tulichagua Wabunge wa Afrika Mashariki, ambao sisi kama ndiyo wadau wao wakuu, ili kutuwakilisha katika sekta hizi zilizotajwa hapa na Mheshimiwa Waziri kwamba, itajielekeza. Jambo la kusikitisha ni kwamba, tokea tumewachagua viongozi hawa; je, tumepata *report* gani hapa kama Bunge lako Tukufu, kuhusu maendeleo yanayokwenda na Bunge letu hili zaidi ya pale tulipokaa kitako na kujadili *Treaty* ya kuanzishwa kwa Jumuiya hii? Sasa ningependa sana kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, kuwe na utaratibu kwa sababu kuanza jambo siku zote kuna matatizo. Kwa hiyo, ikiwa kama kuna matatizo sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge wa Kenya na Wabunge wa Uganda, ndiyo wadau wakuu wa chombo hiki ambao tunawawakilisha wananchi.

Sasa sisi Wabunge tuna taaluma gani hasa inayohusiana na Jumuiya hii ya Afrika Mashariki? Kama hii ndiyo hali, je, hawa wananchi wetu ambao tunawawakilisha katika Bunge hili watapata taarifa gani au kuna utaratibu gani wa chombo hiki cha Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuwafikia wananchi na kuwapa taaluma ya kuanzishwa kwa Jumuiya hii? Huu ukiwa ndiyo mwenendo hatuoni ile hali ya kujiona kwamba, Tanzania tunashindwa katika nchi hizi na kubaki na malalamiko, kwa sababu hatuna taaluma na nyezo za kuwaeleza wananchi wetu mwenendo kamili wa Shirikisho hili la Afrika Mashariki. Je, itakuwaje hapo tutakapofikia shirikisho kamili? Kwa hiyo, naishauri sana Wizara hii, pamoja na Bunge lako Tukufu, tuweze kuwa na taaluma za kuweza kujua tukishirikiana na Wabunge wetu hawa tukifika majimboni mwetu tuwape

taaluma wananchi kuhusiana na chombo chetu hiki ambacho kwa kweli ni chombo kilichokuwa na manufaa na faida kubwa sana katika nchi yetu hii ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuwa, tulipokuwa na Shirikisho la Afrika Mashiriki ambalo kwa bahati mbaya lilivunjika pakatokea mgawano hapa wa mali na tulichokipata tunakielewa. Sasa leo linakuja Shirikisho hili la Afrika Mashariki na kwa kiasi Makao Makuu tunasema ni Arusha, lakini kwa taarifa niliyokuwa nayo ni kwamba, kuna eneo ambalo limechaguliwa kwa ajili ya kujenga Ofisi Kuu ya Shirikisho hili la Afrika Mashariki na eneo hili tayali litengwa. Kwa taarifa ninazozielewa, kuna mvutano kwamba, inavyoonesha wenzetu bado hawako tayari kuona ofisi hii inajengwa. Sasa eneo lipo, Tanzania ina maeneo makubwa ya kutosha ya kuhakikisha kwamba, tunaweza tukapata eneo. Hofu yangu, isije ikafika wakati tukajenga Makao Makuu ya Shirikisho hili katika eneo dogo kiasi cha kwamba, kesho na kesho kutwa tukitaka kujenga majengo zaidi, tukaja kukosa nafasi. Ningeomba sana Wizara hii kwa kushirikiana na taasisi zote ambazo zinahusika, kuhakikisha kwamba, eneo kubwa zaidi ambalo lipo, linajengwa ofisi nzuri ya kuweza kutuwezesha kuendesha Shirikisho letu hili ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo kuhusiana na Shirikisho hili kama tunavyoelewa kwamba, binadamu anaanza kucheka mara moja wakati akimwona mtu kajikwaa na kitu cha kwanza kitakachoanza kujitokeza atacheka au kagongwa na gari atapiga kelele huyo, kaisha huyo. Lakini anapookota pesa, hakuna mtu anayecheka ananyamaza kimywa. Kwa hiyo, kwa mantiki hii ni kwamba, kila tutakapojitia kwenye matatizo ya Shirikisho letu hili, watu wako tayari kutucheka na watakapoona tunafanikia wataanza kuwa maadui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri sana kwamba, katika Shirikisho mbali na yote ambayo tunayazungumza ni kuhakikisha kuwa mfano ambao umejitokeza au unajitokeza kwenye Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao ni mfano duniani na kielelezo cha Muungano kiwe ndiyo mfano wa kuanzisha Shirikisho la Afrika Mashariki. Wakati huo huo tukijaribu kutafuta kila taratibu na mbinu ambazo kwa kadri inavyowezekana zinaweza zikatupeleka mahali pa kuhakikisha kwamba, hatutakuwa na migongano na mivutano ya baadaye. Hasa ikiwa kama Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama kielelezo cha wenzetu kuweza kuona ni jinsi gani tunavyendesha Muungano wetu huu kwa amani, utulivu na kukaa kitako kwa masikilizano mazuri kabisa bila ya mvutano.

Kama patajitokeza kuwa na mvutano, jambo la busara ni kukaa kitako kujadili na kusuluhisha ili tuepukane na vicheko, ambavyo wengine bado wanatoa macho kuvitizama vitajitokeza lini. Najua wapo Watanzania humu humu, wapo Waganda na wapo Wakenya, ambao hawapendi kuona Shirikisho hili linajitokeza. Lakini mimi kwa msimamo wangu na imani yangu, naamini wazi kwamba, Shirikisho letu hili litafikia muafaka na tutafanikisha kadri inavyowezekana, kwa manufaa ya wananchi pamoja na nchi yetu yote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono haja kwa asilimia mia moja asante sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia machache katika hoja hii iliyotolewa asubuhi ya leo na Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri kabisa, ambayo inatupa matumaini na napenda kumhakikishia kwamba, tutakuwa nae, tutamuunga mkono, hii ni Wizara changa na ndiyo anaanza. Mambo yake ni mengi na ni makubwa kwa hiyo, hapana shaka utahitaji ushirikiano wetu sote na tutakupa ushirikiano na naweza kukuhakikishia kwamba, ushirikiano wangu mimi kama Mbunge wa Bukoba Mjini, unao Mheshimiwa Andrew J. Chenge. *(Makofi)*

Pili naomba nimpongeze ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, kwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Naomba niweke kwenye rekodi, wakati nilipokuwa kwenye mchakato wa uchaguzi katika Jimbo langu la Bukoba Mjini, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, alinisaidia sana. Alikuja katika mikutano minane, alinipigia kampeni ya kutosha kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi na kwa niaba yangu mimi mwenyewe kama mgombea na alitoa changamoto kubwa sana na hatimaye tukawashinda wale jamaa zetu, ambao tunawaita *nkangabwe*. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, napenda niwape pongezi Maofisa wa ngazi ya juu na ngazi ya chini walionao katika Wizara hii. Tunamshukuru Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwanza, kwa kuweka hii Wizara, kwa sababu ndugu zetu Wakenya walikuwa nayo kwa muda mrefu. Ndugu Biwoti kabla hajabadilishwa alikuwa Waziri wa *East African Cooperation* na inaonesha kwamba Wakenya walikuwa tayari wamejiandaa na nafikiri hata Waganda vile vile. Lakini sasa sisi ndiyo tumeanza na kuunda Wizara. Sasa ningependa kujua hii Wizara ina watu wangapi? Maana yake tunaweza tukawa tunazungumza tu, juu ya majukumu ya Wizara, juu ya Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Napenda niambiwe hii Wizara ina maofisa wangapi, ambao wako *responsible* katika *activities* za Wizara hii; una watu wangapi Mheshimiwa Waziri?

Mbali ya kuwa na watu wangapi, naomba Mheshimiwa Waziri ukiwa unajibu hizi hoja, utuambie una wataalam wangapi? Kwa sababu hii ni Wizara inayoshughulikia suala ambalo linawagusa Watanzania wote, *without exception*. Sasa napenda kujua una wataalam wangapi, ulionao katika Wizara yako, ambao unasaidiana nao kusukuma ajenda hizi ambazo umezitoa katika hoja yako asubuhi ya leo?

Pia napenda kuweka msisitizo kwamba, hii Wizara haiwezi ikasimama peke yake, unapozungumzia masuala ya *Common Market* na *Customs* na hata masuala yanayokwenda katika *political federation, actually* unazungumzia Serikali ya Tanzania. Sasa nafikiri upo umuhimu wa kuwa na ushirikiano wa karibu sana na Wizara nyingine ambazo zinahusika, kwa sababu ni lazima zitakuwa *directly involved* katika kuhakikisha kwamba, hii *enterprise* yote ya kuhakikisha kwamba, tunakwenda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, inakuwa sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianzie mahali ambapo wenzetu wa Kambi ya Upinzani amemnukuu Hayati Kwame Nkrumah, alisema *"Seek for yourself a political kingdom and then everything would be added to it.*" Nafikiri hivyo ndivyo alivyosema na ni kweli. Lakini napenda kama angekwenda *a step further,* kwa sababu hii *argument* ya Kwame Nkrumah ilifika kilele chake mwaka 1964, wakati alipopambana uso kwa uso, jicho kwa jicho na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika Mkutano wa *OAU* mwaka 1964 huko Cairo. Wakati Nkrumah alikuwa na *phases* yake hiyo ya kutaka *political federation* na Mwalimu, alikuwa anasema hapana lazima twende *through regional integration*.

Kwa hiyo, hizi zilikuwa ni *approach* mbili, ambazo zilikuwa zinavutana na zilifikia kilele kabisa cha hadhara mwaka 1964 na kusema ule ukweli, Mwalimu aliweza kushinda kwa hoja, lakini baadaye kidogo ndiyo Mheshimiwa Kwame Nkrumah hakuchukua muda kwa sababu ilikuwa ni 1964 na 1966 akapinduliwa na hakuweza kurudi katika Urais mpaka alipofariki. Nadhani Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika hoja yake, ataona kabisa kwamba, hata hii *thrust* tuliyonayo ni ya *regional integration* na ni *step by step approach*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani upo umuhimu wa kuwashirikisha Watanzania wote katika *enterprise* hii. Kama walivyosema wenzentu waliotangulia ni kwamba, hili lisiwe suala la viongozi peke yao, hili ni suala kubwa na linamgusa kila mtu. Unapozungumzia *common market* unazungumzia kila Mtanzania, unapozungumzia mambo ya *tariffs* unazungumzia juu ya wafanyabishara wetu wote hapa Tanzania, kwa hiyok hili si suala la kufanyiwa maamuzi peke yake na Serikali ama viongozi katika Serikali. Nadhani sasa upo umuhimu katika hii *process* ndefu, kuwashirikisha Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *European Union* hii ambayo tunaisikia, ilianza *federation* na kuanza kwake ilikuwa ni mwaka 1957 kama sikosei, kupitia katika *Treaty of Rome* na wao walianza wakiwa wachache, walikuwa wanane wakaenda kumi, mpaka leo tunazungumza baada ya miaka karibu 49, lakini hawajafikia kilele cha *political federation*. Wamekuwa na mambo humu katikati na wamekuwa na *referendums* mbalimbali. Kwa mfano, mpaka leo wana-*common currency (Euro),* ambapo wapo baadhi yao ambao si *part* ya *Euro*. Wana-*common exchange mechanism* ya *Euro* na *currencies* nyingine, lakini bado wengine hawajaingia katika hiyo. Kwa hiyo, hilo si ajabu ni kwamba nia ipo, kama hapa Tanzania nafikiri nia ipo na kwetu baadhi yetu tunasema kwamba, nia ya kuwa na *federation* iwepo lakini tuingie katika kitu ambacho tunakielewa na tunajua *implication* zake ni nini.

Mheshimiwa Waziri hapa amezungumzia juu ya *tariffs,* ambazo zinakwenda zinapungua, *I think gradually* amesema kwamba, mwaka 2010 tutafikia *zero tariff* kwa bidhaa ambazo zitakuwa zinaingia pote katika eneo la *East Africa*. Kwa hiyo, unapozungumzia 2010 na hii ni 2006, unazungumza kwamba, tumebakiza miaka mitatu. Kweli unataka kuniambia kwamba, katika miaka mitatu Tanzania itakuwa tayari? Mimi siamini na naiweka kwenye *record, I don't believe it*, kwa sababu ukitazama tulikotoka

mpaka hapa tulipofikia, hatujajiandaa vizuri. Hii *East African Cooperation* ilivunjika, imevunjika imekuja imeanzishwa, *fine*. *(Makofi)*

Tunakubali na ni kitu kizuri na ulimwengu mzima unakwenda *in integration*. Latin American wanazo *Andean* G*roups,* ambazo wako Brazil, Argentina, Uruguay, Paraguay na wana-*form a common market.* Ukitazama wana-*establish even the larger common market,* ambayo itakuwa *America* inatoka Canada, *United States* mpaka Latin America. Bado unakuta kwamba, *the sovereign* na *interest* za nchi, bado ziko pale pale na itachukua muda mrefu. Sasa kuniambia mimi leo kwamba, Tanzania i-*move* na ni kweli nasema twende, lakini hatuwezi kwenda kasi hivyo. Kwanza, wananchi wengi hawaelewi. Nikienda katika Jimbo langu la Bukoba Mjini leo, nizungumze na wananchi juu ya mkataba ambao una-*establish East African Community* na *protocol* zake, itakuwa kazi kubwa, hawajui hii *enterprise*, maana yake, hawajui *implications* zake. Hii ina-*aply* katika Tanzania nzima *and I will not be even surprised* kwamba, inagusa hata Wizara mbalimbali tulizonazo. Serikali watu wanachukulia maeneo yao, lakini hawawezi kujua *broader implication* ya kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, kweli twende lakini tuwe *conscious* na tuweze ku-*guard interests* zetu jinsi tunavyokwenda. *The Community* ya kwanza ilipo *break, of course* watu wanaweza kueleza sababu mbalimbali. Lakini *actually the cracks of the matter* ilikuwa ni *political*. *The political differences, it was the haughty of the cold war,* ambapo Mwalimu alikuwa amesimama kidete katika masuala ya Afrika *and he was well known*. Kwa hiyo, alipigwa vita yeye *personally and then* tulikuwa na *situation* ya Uganda, *where we had* a *military* Idi Amin. Kwa hiyo, yalichangia mambo mengi *apart from the internal issues* ambazo ziliweza ku-*contribute* lakini zilikuwepo *external factors*. Leo unapopambana na Kenya kiuchumi, hupambani na Wakenya *in such,* unapambana na *multinational cooperation,* ambazo ziko *based* katika uchumi wa Kenya. *(Makofi)*

Wewe jiulize tangu tumepata uhuru mpaka leo, *currency* zote katika Afrika *South of Sahara,* zimekuwa zina *crumble into peaces.* Lakini ukitazama *currency* ya Kenya imebaki *stable why*? Ni kwa sababu wana-*vested interest* na wamejiingiza kwa undani katika uchumi wa nchi ile. Sasa sisi tunapotaka kuingia katika *competition with them,* tunaingia namna gani? Hili ni suala la mkakati, ni suala la *education* na mimi nasema sidhani kama tumejiandaa vya kutosha na nasema twende kama wengine wanavyokwenda, lakini twende *on step by step approach* na kila *step* tunaihakikisha kwamba, hii hapa ina manufaa na Watanzania wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Rwanda na Burundi, mimi silipingi ni zuri, lakini *what does it mean*, lina *implications* gani kwa Mtanzania wa hapa? Maana yako masuala tuliyonayo bado hatuja-*resolve* juu ya *community* hii na juu ya *union* ambayo tunataka kuiweka, *of course* tunazungumzia *expanded union*. *Europeans* kama unazungumza *expansion of the union,* wamekuwa wakifanya hii *expansion after long years.* Lakini wao wana *political aim,* wanataka ku-*weaken the former Soviet Union, which is the Russian Federation* na wanahakikisha kwamba, zile nchi ambazo zilikuwa ni *Social Republic,* wanaweza kuzivuta huku na kuhakikisha kwamba, *frontier European*

*Democracy* kama wanavyosema wao na *frontier* za *European* zinakwenda *as far as they can,* kufikia katika mpaka wa *Russian Federation*. *They have the aim, it is* a *political aim*. Lakini sasa unaponiambia kwamba, unataka Rwanda na Burundi waingie, nataka niulize *what is your aim,* unataka ku-*extend* kufanya nini? Sikatai, sina *problem* nayo, lakini *I need explanations* na nataka niji-*satisfy* kwamba, kweli tuna-*move* katika kitu ambacho kina manufaa kwa Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Mradi wa Kuendeleza Ziwa Victoria, hili ni suala muhimu kwa sababu nimeona kabisa katika *report* yako na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, wameweka meli ya utafiti. *Fine,* meli ya utafiti ni nzuri lakini kwa mtu wa Bukoba, meli ya utafiti haimsaidii sana, hii nasema wazi. Anataka meli ya usafiri, anataka meli ya kusafirisha abiria na anataka meli ya kusafirisha mizigo yake. Bado watu wana zile *dreams* walizokuwa nazo zamani, meli ilikuwa inatoka Bukoba inakwenda *Port Beri,* inakwenda Mwanza, Musoma hadi Kisumu. Kuna *movement* ya biashara, watu na kuna *movement* ya pesa, hicho ndicho kitu wanachotaka na ningependa Waziri atuambie kuhusu hicho au mkifanyie kazi.

Utafiti kweli uendelee, sitaki kudiliki kusema hauna maana, lakini kwa mtu wa Bukoba kwa sasa hivi, ukimwambia juu ya utafiti kwa kweli atasema hiyo ni ndoto. Yeye anachotaka ni kitu ambacho ni *practical,* kitakacho mwongezea kipato leo na kesho na tusisahau *MV* Bukoba ilipozama kulikuwa hakuna *replacement.* Kwa hiyo, usafiri katika Ziwa Victoria ni tabu. Iko ile *MV Victoria*, ambayo ilianza ku-*operate* tangu mwaka 1964 mpaka leo ni hiyo hiyo, mara matengenezo mara nini. Kwa hiyo, naomba hilo mlitazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti, kwa taarifa tulizonazo na hili kaligusia Mheshimiwa Mbunge mwenzetu hapa, kuhusu ujenzi wa Makao Makuu, kumekuwa na mvutano mkubwa sana. Tanzania wametoa ardhi, Wajerumani wametoa pesa kiasi cha *Euro* milioni nane, lakini kumekuwa na mvutano kwa nini hii haifanyiwi kazi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, atupe sababu nzuri za kueleza zaidi na kuona nini kifanyike kuhusu hilo, lakini tungependa Makao Makuu yawe Tanzania kama ilivyo katika mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu matumizi ya fedha, ambayo tunakwenda kulipia na hii imezungumzwa kwenye ripoti yetu ya Kamati ya Mambo ya Nje. *Rent* watakayolipa inakuwa shilingi milioni 216 kila mwaka. Sasa milioni 216 kila mwaka, kwanini ulipe kodi ya namna hiyo kila mwaka? Hii inatosha kabisa kulipa *mortgage* kila mwaka na mkawa na jengo lenu, mkawa mmetupunguzia sisi matatizo ya kuwa tunalipa kodi ya kila mwaka. Kwa sababu hii inakuwa ni mali ya Serikali na ni ya Watanzania. Kwa hiyo, naomba kabisa Mheshimiwa Waziri, ufanye kila njia na sijui mna utaratibu gani huko na kama iko haja hata sisi baadhi ya Wabunge, tunalizungumza kwa sababu tunaona ni kitu ambacho kina mantiki ndani yake.

Huwezi kuchukua kila mwaka shilingi milioni 216 unalipa kodi; *why*? Kama unachukua pesa hizo ukawa una jengo ambalo ni lako, ambalo mnaweza kufanya kazi, mkatufanyia kazi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, nafikiri ingekuwa nzuri sana. Kwa

hiyo, naomba nichukue nafasi hii, niwaunge mkono kabisa. Naomba nimwambie yeye Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwamba, ninawaonea sana huruma, hii ni Wizara changa, lakini *enterprise* na *challenges* mlizonazo ni kubwa sana na nisingependa tuwalaumu, kwa sababu mmeingia katika kitu ambacho ndiyo kinakwenda. Kwa hiyo, mmeingia katikati na mnajaribu kukiweka katika hali iliyokuwa sawa. Naomba msichelewe wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kuhusiana na Wizara hii mpya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nafahamu kwamba, mwaka 2004 Marais wetu watatu; Rais Mwai Kibaki, Rais Yoweri Museveni na Rais Benjamin William Mkapa, waliunda Kamati kwa ajili ya kufanya *fast tracking* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, chini ya Mwanasheria Mkuu wa Kenya, Bwana Wako na wakawa wamependekeza kwamba, zianzishwe ku-*deal* na masuala ya Afrika Mashariki pekee. *(Makofi)*

Kenya wakawa wa kwanza, Tanzania tukafuata na juzi pia Rais Yoweri Mseveni, amemteu Ndugu Elia Kategaya, ambaye ni *prominent politician* kuwa, Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, napenda sana kuwapongeza Marais wote, kwa kutekeleza agizo hili la Kamati.

Lakini hawakupendekeza kuanzisha Wizara tu, vile vile wamependekeza kwamba, Mawaziri hawa wakae Arusha. Kwa hiyo, natarajia kabisa kwamba, utekelezaji wa wazo hili la Kamati ya Wako, hautaishia kuwa na Wizara. Kwa hiyo, mjomba wangu na kaka yangu, Mheshimiwa Andrew J. Chenge na Naibu wake, wajiandae kuhamia Arusha, kwa sababu ndiko Makao Makuu ya Afrika yalipo na wataweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana, kwa sababu kwa dunia ya sasa, kila nchi zinajiunga katika *groups* mbalimbali. Kwa hiyo, Wizara hii ni muhimu sana kwetu, tukiipatia rasilimali za kutosha, itaweza kutatua matatizo mbalimbali, ambayo tumekuwa tukilalamikiwa kuhusiana na kutokujiandaa, kutokuwa na mkakati na kutokuwa na uratibu mzuri wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, mimi binafsi kwa umuhimu wa Wizara hii, nasema kabisa kwamba, nitaunga mkuno hotuba na bajeti hii ya Wizara hii ili waweze kuanza kazi zao vizuri na naamini baadaye wataweza ku-*improve* zaidi. *(Makofi)*

Napenda nianze na suala la woga na inawezekana nikawa tofauti na wenzangu, Watanzania tumegubikwa sana na woga. Tumegubikwa na woga wa kuwaogopa Wakenya, tumegubikwa na woga wa kuwaogopa Waganda na sasa hivi tumeanza kugubikwa na woga wa kuwaogopa Wanyarwanda na Warundi. Uwoga unatoka wapi, ukisoma hotuba ya Waziri kuna maeneo matatu, ambayo yanaonesha kabisa *pessimism* kana kwamba, sisi tunaenda lakini ni wanyonge. Sasa mimi nashindwa kuelewa hii tabia ya unyonge Watanzania wameianza lini? Ukurasa wa 28 anapozungumzia soko la pamoja, naomba ninukuu: "Hatua hii ni nyeti sana kwetu Watanzania kwa sababu

inagusa hisia ya ardhi yetu na ajira za watu wetu kuchukuliwa na raia wa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki." Waziri anaendelea anapozungumzia changamoto ni namna gani ya kupunguza au kuondoa tofauti ya maendeleo iliyopo kati ya hizi nchi tatu, ukurasa wa 43 ibara ya 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ubishi kuwa kwa muono wa muda mfupi, Tanzania inaweza isinufaike sana kutokana na uanachama wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kamati ya Mambo ya Nje, Ibara ya 6.1. Aidha, viongozi katika ngazi mbalimbali waelimishwe ili wasiwape wageni ardhi ili wageni hao wasije wakamiliki ardhi ya nchi yetu kwa kisingizio cha Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu uwoga tunautoa wapi? Kamati uwoga, Serikali uwoga! Mimi nadhani jambo la msingi ni kujiandaa ni jinsi gani kuwapa nguvu Watanzania na wao waweze kuchukua fursa zilizoko Uganda na zilizoko Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu, mimi nawaambia tutake tusitake, Jumuiya ya Afrika Mashariki na hata Shirikisho, vitakuja tu kwa sababu ndiyo *Order of the Day*. Tupo kwenye *globalization*, Tanzania kama nchi, haiwezi kupambana peke yake na *Global Forces* za Dunia. Haiwezekani, ni lazima tuungane na wenzetu, tuchanganye nguvu za pamoja, tuweze kupambana, tuhakikishe kwamba, eneo hili la Kanda hii ya Afrika Mashariki, linaweza kufaidika na *Global Economy*. Lakini sasa huu uwoga ambao tumeujaza, kunyang'anywa ardhi, kunyang'anywa ajira. Nani kasema kwamba, Watanzania wote walipo hapa Tanzania wameajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachojua nimesoma na Wakenya hapa Tanzania, nimesoma na Wakenya Ujerumani, hajatokea hata Mkenya mmoja, ambaye alinishinda Darasani. Siyo kwamba, eti wao wana akili sana kuliko sisi. Watanzania wana uwezo mkubwa, isipokuwa hatujaweka mikakati ya kuwafunulia fursa zilizopo katika nchi nyingine, hilo tu. Sasa, matokeo yake tunakuwa *Protectionists*. *Protectionism* haiwezi kutusaidia hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninamwomba Waziri, mwaka ujao hotuba iwe na *optimism*. Hakuna sababu ya kuwa *pessimistic*, ni lazima tutembee kifua mbele, tujione kwamba, sisi tuna uwezo wa kuchukua fursa kuliko wenzetu, badala ya kuanza kung'ang'ania *protectionism*, matokeo yake kila siku tunawafukuza Wakenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mambo ya Ndani, tokea aingie ameshatoa *PI* kibao za kuwarudisha Wakenya. Wakenya walioajiriwa na Mengi, Wakenya waliofanya nini; ya nini? Kitu kimoja, *competition* ndio silaha pekee ya maendeleo ya nchi yoyote Duniani. Tuingie kwenye soko, tushindane nao, vijana wetu waweze kupata ujanja wa kushindana nao, kwa sababu kama mtu unaona kwamba anakushinda, si ujiunge naye ujifunze jinsi gani ambavyo anafanya. Ndio njia pekee, epukeni kabisa *protectionism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninataka kulizungumzia na amelizungumzia ndugu yangu, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya na mjomba wangu, kaka yangu na mzee wangu, Mheshimiwa Balozi Hamis Sued Kagasheki. Hivi mnaogopa nini Rwanda na Burundi kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki? Kuna sababu! Mnasema kwamba Rwanda na Burundi wana fujo, watahamisha fujo! Hivi nani hajui kwamba, *Northern Uganda* kuna *Lord's Resistance Army,* wameleta fujo Tanzania? Njia pekee ya kumaliza matatizo ya Rwanda na Burundi ni wale watu kuingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ndio suluhisho pekee, kwa sababu tutaweza kuwadhibiti, tutaweza kuzuia wakimbizi wanaokuja nchini kwetu na kuharibu mazingira yetu.

Kwa sababu wanapoingia kwenye Jumuiya, kuna masuala ya mahusianao ya Kijeshi, kuna masuala ya mahusiano ya kiusalama. Tukiona wale wenzetu wanaenda kinyume na misingi ya demokrasia, tunaweza tukawaminya, lakini, mnapowaacha peke yao, ndio wanapigana, wanauana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mwalimu alikuwa anasema kwamba, hao wenzetu wanaokimbia kuja Tanzania, tusiwaite wakimbizi. Mwalimu alikuwa anawaita Wageni wa Kazi. Sasa leo kwa sababu ya *Global Forces* na sisi tumekuwa kama Wazungu tu, Waafrika wenzetu walioko Rwanda, Waafrika wenzetu walioko Burundi ni wakimbizi. Lakini, mimi sijui inatoka wapi, sisi ni Waafrika na njia moja muhimu ya kuhakikisha kwamba, tunalinda hizi nchi zisiingie kwenye vita tena, ni Jumuiya ya Afrika Mashariki tu. Wala hamna sababu, mimi napingana kabisa kabisa na Mheshimiwa Manju S. O. Msambya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho la matatizo ya Rwanda na Burundi ni Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwisho. Ndio suluhisho pekee. Kwa hiyo, ninaomba Tanzania iwe mstari wa mbele kuhakikisha hizi nchi zinaingia. Lakini zaidi ya yote, hizi nchi ndio masoko yetu pekee ya uhakika. Ukiagalia urari wa biashara kati ya Tanzania na Burundi; Tanzania na Rwanda, sisi ndio tunaofaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunajenga Isaka pale, Bandari ya Nchi Kavu, ni kwa ajili ya nini? Kwa sababu ya mizigo inayokwenda Rwanda. Biashara itakuwa rahisi zaidi kama Rwanda itakuwa mwanachama wa Afrika Mashariki. Mimi sioni sababu ya uwoga na ni uwoga ambao ni *unjustified.* Kuna *myth* ambayo imeingia hapa kwamba, Wanyarwanda wanauwana, Warundi wanauwana, watakuja kusababisha ugomvi Tanzania. Kama Wanyarwanda na Warundi wanakuja Kigoma, wanagombea uongozi wa vijiji wanapata, ni upuuzi wa nani? Ni wale wananchi kutokuwa na *strict measures* za kuzuia wageni wanaoingia na wala hii haiwezi kuwa sababu ya kutuzuia kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Andrew J. Chenge, awe mstari wa mbele. Najua Waganda wanaizuia Rwanda kuingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa matatizo ya kibinafsi kati ya Paul Kagame na Yoweri Museveni. Sisi tuwe mstari wa mbele, tuhakikishe kwamba, hawa watu wanaigia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, tuweze kufaidika na biashara kwa sababu wale watatumia Bandari yetu na wale watasababisha maeneo ya mipakani kama kule Kagunga na Karagwe, yaweze

kufanya biashara na watu wa Rwanda na Burundi na ni soko kubwa, Rwanda ina watu milioni kumi, Burundi ina watu takriban milioni sita. Hili ni soko letu, kwa hiyo, mimi sioni sababu yoyote ya kuwa na uwoga kuhusu hii kitu. Mimi niko mstari wa mbele kabisa na ninaomba niwe *labeled* kabisa kwamba, *I am Pro*-Rwanda na Burundi kuingia kwenye Jumuiya ya Afrika ili kuweza kupunguza matatizo na tuweze kuwadhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uwoga mwingine kuhusu Shirikisho. Mimi naona Shirikisho la Afrika Mashariki ndio suluhisho la matatizo yetu ya Muungano, kwa sababu Shirikisho litatufanya tuuangalie upya Muungano, tuu-*define* upya Muungano. Je, tutaingia kwenye suluhisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki na *United Republic* au itabidi kurudi kwenye *constituent parts* za 1964 ili tuweze kuingia na kuwa na *Federation* ambayo ni *meaningful?*

Hii ndio *challenge* tulionayo na hii ndio *challenge* ambayo naomba Wizara iweze kuiangalia na kui-*spearhead* hata katika kutafuta haya maoni, tuweze kuangalia *the question of Zanzibar* katika suala zima la *Federation* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, ninaomba tuangalie hii kitu kwa mapana yake kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninavyofahamu, Wabunge wa Afrika wanapeleka taarifa za kazi zao kwa Kamati ya Mambo ya Nje ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ninachokiomba tu ni kwamba, Uganda tayari wamechagua Wabunge wao Novemba, maana yake wale Wabunge tuliowachagua wanakuja kuomba tena kura, tunatakiwa tuwachague, nadhani na sisi mwezi Novemba tutaweza kuwachagua. Uganda tayari wameshachagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho napenda nishauri na naomba ushauri huu uangaliwe kwa makini sana, tujaribu kuangalia *continuity*. Tumepeleka Wajumbe wa *EALA,* kipindi ambacho ndio Bunge linaanza. Kuna *a lot of experiences,* ambazo watu wamezipata. Tuwe makini sana, tukiingiza watu wapya wote, *one hundred per cent*, tuna-*loose*. *We have to be very very careful with this*. Tuhakikishe kwamba, kunakuwa na *continuty*, kuna watu ambao wameshapata uzoefu, kuna watu ambao wameshakuwa ni Wenyeviti wa Kamati mbalimbali, kuna watu ambao wameshajifunza mambo mengi kule. Tuhakikishe kwamba, *strategically as a country*, kwa sababu hatupeleki kule kuwapa watu ajira, hii *notion* naomba nayo tuweze kuiangalia. Tunapeleka watu kule kwa ajili ya kwenda kutetea *interests* za nchi yetu. Kwa hiyo, tuangalie suala zima la *continuity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo ninapenda kulizungumzia, ni suala la mahusiano, Jumuiya ya Afrika Mashariki, *SADC* na *COMESA*. Kwa mujibu wa *Custums Management Act,* ambayo imeunda *Customs Union* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Ibara ya 112, Sehemu ndogo ya (ii), inasema kwamba, itakapofika Desemba, 2006, *Preferential Trade Arrangement* zote ambazo nchi zetu; yaani Kenya, Uganda na Tanzania, walikuwa wanazitoa kwa *SADC* na *COMESA*, zinakufa. Mpaka sasa hivi kulikuwa kuna juhudi za Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kuleta Bungeni katika *EALA Bill* ya *Join Trade Nagotiation Act* kwa ajili ya ku-*take care* hii *problem,* ambayo inaweza ikatokea kwa sababu kutakuwa na *vacuum* itakapofika mwezi Desemba, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ninamwomba Mheshimiwa Waziri waliangalie, aidha, tuhakikishe ile *Joint Trade Negotiation Act*, inapitishwa mapema ndani ya *EALA or* tufanye *ammendment* ya hii Sheria kwa sababu Desemba ni karibu sana na mpaka sasa bado hatujaweka hizi *preferential*. Sisi tuna *preferential arrangement* na *SADC* na Kenya na Uganda wana *preferential arrangement* na *COMESA*.

Kwa hiyo, *section 112*, aidha ifanyiwe *ammendment* kuongeza muda kwa sababu muda umekwisha au *immediately* tuhakikishe kwamba, *Joint Trade Negotiation Act,* ambayo inazitaka nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki ku-*negotiate Trade* na makundi mengine kwa pamoja, iweze kupitishwa na Jumuiya ili kuhakikisha kwamba, tunaondoa hili tatizo la kisheria mbalo linaweza likatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda niwape moyo viongozi hawa wapya wa Wizara hii na kuwaambia kwamba, tuko tayari kuwaunga mkono kwa mawazo na kwa michango ndani ya Bunge, kuhakikisha kwamba, Wizara hii inafanya kazi vizuri na nchi yetu inapata faida kutokana na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami nichangie kwenye hoja hii ambayo kwa kweli kutokana na mazungumzo yanayoendelea, ni nyeti na ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali naomba nimpongeze Waziri na Naibu wake, kwa hotuba nzuri na iliyowasilishwa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nitazungumzia mambo matatu tu: La kwanza, nataka nizungumzie suala ambalo linajikita kweye mipaka kati ya nchi zetu za Afrika Mashariki, miradi ya maendeleo ambayo inafanywa kando kando ya mipaka yetu na matatizo yaliyojitokeza kutokana na miradi inayofanywa katika nchi zetu, ambayo iko maeneo ya mipakani mwa nchi hizi. Mfano matatizo tunayoyaona kwenye Ziwa Victoria ya uvuvi pamoja na uchukuzi, matatizo tunayoyaona kutokana na kupanuka kwa kilimo, *Commercial Farming* upande wa Masai Mara katika Serengeti na Masai Mara ilivyoathiri *Wildlife* au wanyamapori katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti vile vile matatizo ambayo yanaweza yakajitokeza kwa vile wanyama tulionao Serengeti, pamoja na wale wanaotembelea maeneo ya Amboseli, kwa kweli ni hao hao, kwa vipindi mbali mbali huzunguka, wanakuwa Tanzania, wakati mwingine wanakuwa Kenya. Sasa miradi yoyote ambayo inaendelea maeneo haya ya mipakani, inaweza ikaathiri uchumi au mazingira ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hilo, najua kwamba, hivi karibuni kulikuwa na Mwongozo ulioandaliwa wa kutathmini athari za mazingira unaoitwa *EIA Guidelines,* kwa ajili ya nchi za Afrika Mashariki. Nia ni kuzingatia au kuelekeza namna ya kufanya miradi iliyo mipakani iwe endelevu, isiathiri mali au rasilimali katika nchi jirani. *Guidelines* hizi nazifahamu kwa sababu nilipata fursa ya kushiriki kuziandaa, najua maandalizi yake yalikamilika mwaka 2004. Katika utaratibu ule, maeneo

yanayozungumziwa, yameainishwa au yamebainishwa kwamba ni *distance* kiasi fulani kutoka kwenye mpaka na kwa kweli Ziwa Victoria lote liko kwenye maeneo hayo, maeneo yote yanayozunguka Mlima Kilimanjaro, Mlima Meru na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mikutano ya kuweza kupata maoni na michango ya wananchi na wataalam katika nchi zote tatu, ilifanywa na ninaelewa kwamba, Mwongozo huo *(Guidelines)* ulipitishwa. Nataka kujua kama Mwongozo ule, Mheshimiwa Waziri ana taarifa nao na kama Tanzania imeuridhia na je, tunalazimika kufuata Mwongozo ule au hapana?

Kwa sababu nitatoa mfano, Mradi kama ule wa Magadi wa *Lake Natron,* kisheria kufuatana na Mwongozo huu, hatuwezi tukautekeleza bila kupata maoni na ridhaa ya wenzetu Wakenya, kama vile Mradi wao wa Umeme wa Waso - Nyiru tulivyoukataa sisi kwa sababu ulikuwa na athari kwenye Ziwa Natron na kwamba, ungeweza kuathiri wanyama kule hasa Flamingo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kujua kama Mwongozo huu umepitishwa na nchi hizi tatu na kama sisi tumeuridhia na umeanza kufanya kazi? Kama jibu ni ndiyo, ni miradi gani kwa mfano, hapa nchini ambayo imeshafanywa kwa utaratibu huo na matokeo yake labda yalikuweje? Hilo ilikuwa ni mchango wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa pili, ninataka kuzungumzia kitu kinachoitwa *Centres of Excellence*. Sekretarieti ya Afrika Mashariki, imebainisha Taasisi kadhaa hapa Afrika Mashariki na kuziita kuwa zitakuwa Taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Centres of Excellence)*.

Mfano hapa Tanzania ni Chuo cha Wanyamapori cha Mweka. Najua kuna Taasisi nyingine hapa nchini kama nne hivi, ambazo zimewekwa kwenye utaratibu huo. Najua vile vile kwamba, kwa upande wa Kenya, mfano ni Chuo cha Utalii pale Nairobi na kwa upande wa Uganda ni pamoja na Chuo kile cha kusomesha Marubani. Hizo ni kati ya Taasisi ambazo zimeainishwa kuwa *Centres of Excellence* za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kujua kutoka kwa Waziri kwanza, kama ana taarifa na hilo; kama anayo, makusudio yake ni nini ya kuwa na *Centres of Excellence* ambazo kwa sasa ni mali ya nchi husika na sasa zitahamia kuwa ni *Centres of Excellence* za Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Huku kuhamisha Taasisi kutoka kwenye nchi husika na kupeleka kwenye Jumuiya, makusudio yake ni nini na utaratibu wa kuhamisha Taasisi hizi kutoka kwenye nchi kupeleka kwenye Jumuiya ukoje? Faida zake ni nini?

Tanzania tutafaidikaje kwa mfano, kama Chuo cha Wanyamapori cha Mweka kitakuwa ni *Centre of Excellence* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuzungumzia suala la matumizi endelevu ya Ziwa Victoria, lililoainishwa ukurasa wa 25 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Katika hotuba, anasema kuna Kamati imeundwa na anaendelea kusema, itafanya kazi na hakusema inafanya tayari, bali itafanya. Ina maana kwamba, labda kama imeundwa halafu haijaanza kufanya kazi, nashangaa maana yake nini?

Lakini nia yake ni kuratibu miradi inayotekelezwa katika Ziwa Victoria, pengine na maeneo yanayozunguka na kuhakikisha kwamba, iko endelevu na kuhakikisha kwamba, miradi hiyo bila shaka haiathiri mazingira ya majini, pengine mazingira ya maeneo yanayozunguka hilo Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu ni kwamba, Kamati hii sijui ni lini ilianza kufanya kazi, kwa sababu tumeendelea kuona matatizo mengi sana katika Ziwa Victoria? Matatizo ni ya kiuchumi na matatizo ya kimazingira. Kwa mfano, tumeona matatizo ya kupungua maji na tunaambiwa pengine inawezekana wenzetu wa Uganda, wamechangia kwa kuanzisha mradi wa mwingine wa umeme, unaotumia maji mengi kuliko ilivyokuwa huko nyuma.

Tumeona jinsi ambavyo sekta ya kilimo cha maua hapa Afrika Mashariki na hasa Kenya na Uganda, walivyoweka miradi mingi sana kando kando ya Ziwa Victoria na hasa ukiruka tu unapotoka nje ya Entebbe, kama unaruka na ndege utaona viwanda vingi sana. Viwanda hivi vinachangia sana kuchafua maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile jana labda wengine tumesikia habari ya Filamu hii, ambayo mwenzetu mmoja anaichambua Tanzania kwa mtazamo anaoujua yeye. Lakini tumeona jinsi Viwanda vya Minofu kule Mwanza vilivyo na matatizo hasa namna ya ku-*dispose* takataka. Kinachoitwa mapanki yale kwa kweli ni *wastes* za viwanda vya minofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa kwamba Viwanda hivi vimeendelea kufanya kazi lakini havina utaratibu unaoeleweka wa ku-*dispose wastes*. Mapanki yale yangeweza kuwa *animal feeds* nzuri sana, yangeweza kuwa *chicken feeds* nzuri sana.

Nashangaa kwamba, hakuna Serikali hapa kwetu, sijui Uganda na Kenya kama wamefikiria kwamba wangeweza kuweka viwanda, tena malighafi ni rahisi, ni kukusanya hizi takataka ambazo wengine tumeziona kwenye Filamu na kutengeneza *animal feeds* na *chicken feeds*.

Sasa sijui kwa vile ni miradi endelevu, kuna Kamati hii inaandaliwa kuhakikisha miradi hii inakuwa endelevu. Kama Kamati hiyo imeanza kufanya kazi, kwa nini suala hili halijaangaliwa ili kuhakikisha kwamba, Miradi ya Minofu ya Samaki katika Ziwa Victoria inakuwa endelevu kwa maana ya kwamba, hatuchafui Ziwa halafu italeta athari kwenye *productivity,* lakini inaleta athari kwenye uuzaji wa minofu hiyo nchi za nje na kutuharibia uchumi ambao ungewa ukatuletea faida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yalikuwa ni hayo matatu niliyotaka kuchangia. Naomba tena nimshukuru Waziri, kwa hotuba nzuri na ninapenda ku-*declare* kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona sasa tumefika mwisho wa shughuli zetu za asubuhi.

Naomba nimtangaze msemaji wetu wa kwanza leo jioni tutakaporudi, atakuwa Mhehimiwa Dr. Raphael M. Chegeni na baada ya hapo, Mheshimiwa Naibu Waziri, ataendelea kutoa maelezo na Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja na yeye atafuatia.

Ninaomba sasa nisitishe shughuli hizi za Bunge mpaka hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.51 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki pamoja na Naibu wake kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti ambayo napenda ku-*declare interest* yangu toka mwanzo kwamba naiunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuunda Wizara maalum kwa ajili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara hii imekuja katika muda ambao ni muafaka. Sisi kama Watanzania ili tuweze kushiriki kikamilifu katika suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki tulihitaji sana kuundwa kwa Wizara hii ambayo itakuwa ni mahsusi kwa ajili ya kusimamia suala zima la Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uamuzi sahihi na kama kulingana na ilivyo *protocol* ya *East African Community* nadhani tumetimiza azma hiyo kwa kuwa na Wizara kamili. Katika suala hili, hii Wizara bado ni changa, ndiyo imeanza haina muda mrefu, lakini ina majukumu makubwa sana ya kutekeleza ambayo yako mbele yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ningeomba sana sana ianze kuzingatia kwanza ni namna gani Watanzania waweze kushirikishwa na kuhamasishwa kuelewa mustakabali wao na ushiriki wao kikamilifu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu sote tunajua kabisa kuundwa kwa Jumuiya hii mpya kulitokana na ile ya awali ku-*fail* mwaka 1977. Lakini tunaamini kwamba hii mpya sasa imejaribu kuainisha mapungufu ambayo yalikuwepo wakati ule na kufanya changamoto kubwa zaidi katika huu mfumo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina jukumu kubwa sana kufanya kila Mtanzania ajue nini hatma yake, ajue nini nafasi yake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Watanzania wengi wanaona mpaka saa hizi Jumuiya hii haiko *people centred*

kwa sababu hawakushirikishwa toka mwanzo. Lakini wamekuja baadaye kuelewa kwamba kuna haja ya kuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ni muhimu sana kwa sababu *we need the regional intergration, we need the regional block* ili tuweze kuwa na sauti ya pamoja. Lakini ukichukua nchi zote za Afrika Mashariki ambazo ni Tanzania, Kenya na Uganda bado tuna mapungufu yetu ya kila nchi na kila nchi inakuwa na mambo yake ambayo nchi nyingine haiwezi kuyaingilia. Ninaamini kwamba bado tuna tatizo kubwa sana kwa nchi ya Tanzania na Uganda kuweza ku-*match up* na wenzetu wa Kenya. Lakini maadamu sisi siyo Kisiwa, ni lazima tuingie kwenye Jumuiya kikamilifu. Tunaingia kwa kufanya maandalizi yaliyo sahihi ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha Watanzania wote.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hatua nne za muhimu sana katika kufikia Jumuiya tenganifu ya nchi zozote zile. Kuna masuala ya *custom union,* kuna masuala ya *common market,* kuna masuala ya *common currency* na kuna masuala ya *political intergration/federation*. Sisi tumemaliza moja, hili la *custom union.* Kulingana na ile *protocol* ya *East African Community* tumemaliza.

Sasa bidhaa za Tanzania zitakuwa sawa na bidhaa zinazotoka Kenya na bidhaa za Uganda hivyo hivyo. Hapo ndiyo tatizo linaanza, kwa sababu kwanza tuliweka vipengele vya kuzuia baadhi ya bidhaa kutoka Kenya zinazoingia Tanzania na Uganda kwa kuzitoza kodi. Lakini baada ya miaka hii mitano kuisha, sasa zitaingia bila kutozwa kodi. Ina maana zitakuwa *highly competitive* na *local products.(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba ni jinsi gani sasa sisi Watanzania tutaingia katika mfumo huo. Lakini jambo lingine, ni kwa vipi Watanzania tumejiandaa. Kusema ni kitu kimoja na kutekeleza ni kitu kingine. Tungependa sasa katika hili tufanye kwa vitendo na siyo kwa kusema zaidi. Kwa nchi nyingi za Ukanda wa Maziwa Makuu, wanaamini sana kwamba Watanzania ni wazuri sana wa kupanga mipango, lakini ni wazembe wa kutekeleza mipango hiyo. Hii nadhani iwe ni fundisho kwetu kwamba tuna mipango mingi mizuri sana, lakini tunaitekeleza namna gani ndiyo iwe changamoto kubwa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu siyo muafaka wa kujadili kwamba tuingie au tusiingie. Hapana, *we have to go.* Wenzetu kama wa *European Union* wao imewachukua muda mrefu sana ku-*plan* na hata walivyo-*plan* kuna baadhi ya nchi zimekataa baadhi ya vipengele. Kwa mfano, kuna wengine wameamua ku-*retain their currencies,* badala ya kutumia *Euro* wanatumia *currencies* zao, lakini ni kwa sababu za msingi tu. Sasa na sisi tuna haja ya kuangalia sana mambo ambayo yana mustakabali na maslahi ya Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki na Naibu wake kwa bahati nzuri ni watu ambao ni mahiri sana. Mheshimiwa Andrew Chenge ni mzoefu, msomi mzuri na ameshiriki sana katika hatua za awali za kuundwa kwa Jumuiya za Afrika Mashariki na Kati. Kwa hiyo, ni changamoto kubwa sana katika suala hili zima. Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala ni mchumi mzuri, ni msomi mzuri, ninaamini

kwamba watatumia nafasi yao pamoja na wataalam wengine katika Wizara yao kuhakikisha kwamba *stake* ya Watanzania katika mustakabali huu inalindwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia suala la *East African Community,* hatuwezi kuzungumza bila kufikiria wenzetu wa Rwanda, Burundi na hata *DRC,* kwa sababu unapokuwa na *economic block* ni lazima uwe na nchi ambazo kweli mnaweza mkashirikishana na mkaweza kufanya maamuzi sahihi ya pamoja na yenye nguvu zaidi. Naomba sana suala la ku-*admit* Rwanda na Burundi tulitazame upya na kwa kweli palipo na nafasi ambayo tutadhani kwamba tumeridhika ni vyema tuka-*incorporate* haraka iwezekanavyo ili sasa *Great Lakes Region* iweze kuwa kweli *is a powerful bloc in terms of negotiations* na hata namna ya kuweza ku-*trade* kama *business block. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo kubwa na ningependa sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake waliangalie ni namna gani ya kutumia raslimali zetu. Sisi Watanzania tuna tatizo moja la kuwa wavivu wa kufikiri sana na namna gani ya kuwa *diversity* na kuwa na mawazo mseto. Sasa hivi unakuta bado Wakenya wanazungumzia kwamba Mlima Kilimanjaro ni sehemu ya nchi ya Kenya. Pia*, Tanzanite* ni mali inayopatikana kutoka Kenya na wanaiuza namna hiyo na hata minofu ya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, minofu ya samaki ambayo inavuliwa kutoka Ziwa Victoria, *exporter* mkubwa ni nchi ya Kenya, siyo Tanzania. Hata ukiangalia *statistics* ambazo zipo zinaonyesha hivyo. Hili ni suala ambalo ni lazima tujaribu kuliangalia sana. Wenzetu ni wazuri kuweza ku-*market*. Kenya wana viwanda nane tu vya samaki, lakini wana asilimia sita ya Ziwa Victoria. Lakini viwanda vya samaki vinavyofanya kazi sasa hivi hapa Tanzania viko tisa tu na tuna asilimia zaidi ya 52 ya Ziwa na samaki wengi wako kwetu kwa sababu ndiyo mwanzo wa Mto Nile. Unakuta kwamba wenzetu wa Kenya wame-*set* viwanda vingi Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mwanza kiwanda kimoja ndiyo cha Mtanzania peke yake, lakini vingi ni vya watu kutoka nje, hususan Wakenya. Unakuta kwamba wanachukua samaki kwetu wanapeleka Kenya, wana-*repack* halafu wanasema wame-*export* kutoka Kenya. Ni lazima tuwe makini sana. Sisi tuna-*lose a lot of revenue.* Mapato mengi sana tunaya-*lose* kwa sababu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la kuzingatia kwa sababu ninaamini kwamba raslimali za Mwenyezi Mungu zinawahusu Watanzania. Suala la *common market* ndiyo tatizo kubwa sana. Tukifungua leo hii hapa Wakenya wote wata-*flood* kuja Tanzania na Watanzania wengi tutanyang'anywa ardhi zetu kwa sababu wenyewe wana desturi ya ku-*grab,* wana tatizo la ku-*grab* hawa, wana uzoefu huo. Watanzania tuna uzoefu wa ujamaa. Ukienda Kenya kila mita mbili unakuta kuna *ngitiri,* watu wameweka *fence* kubwa sana. Kwetu hapa unafika kijijini unasema, jamani, natafuta eneo hapa, unaambiwa, liko hapa eneo la kijiji. Ni lazima tujaribu kubadilika katika masuala haya ili tuweze ku-*move* na kuwarithisha Watanzania raslimali zao kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo hata la kazi. Mfano sasa hivi ukienda Dar es Salaam, Taasisi nyingi za fedha na mashirika mbalimbali yanaongozwa na wageni, siyo Watanzania na hii bado haijafikia kwenye mambo ya *common market.* Tukifika pale ambapo sasa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaweza kutoka nchi moja kwenda upande mwingine wakafanya kazi, wakajenga, wakaishi, waka-*settle* bila tatizo lolote itakuwa ni tatizo kubwa sana kwa Watanzania. Ningeomba hili kwa kweli mliangalie sana na hasa kulinda mustakabali na maslahi ya Watanzania. Bado mfumo wetu wa elimu nchini Tanzania haujakidhi hasa soko lililopo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia anaweza kukubaliana nami kwamba tuna-*flood* kila mwaka *graduates* karibu 48,000 lakini Watanzania tuko karibu milioni 48 sasa hivi. Kenya wao wanakimbilia kwenye 80,000 au laki moja, lakini watu wako chini ya milioni 32 au 30. Sasa unakuta kwamba wao wana watu ambao wanawa-*train*. *Curriculum Vitae* yao inakuwa inajaribu kuwafundisha siyo kuajiriwa kazi, bali ni kupata elimu wakafanye kazi. Hii inakuwa ni changamoto kubwa sana kwetu sisi, mfumo wetu wa elimu uweze kubadilika uendane na hali ya soko ilivyo, *otherwise* Watanzania watasoma, lakini bado wakisoma hawawezi kufanya kazi kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna haja ya kujaribu ku-*empower* hii *Private Sector*. Tuwasaidie kikamilifu, tusiseme tu kwa maneno. Leo unakuta kwamba watu wa *Private Sector* hawawezi kuuza mali zetu vizuri, hawawezi ku-*add value* na sisi hatuwezi ku-*compete* vizuri. Hili ni tatizo kubwa sana kwa sababu mkulima au mzalishaji anapozalisha, bila ku-*add value* ambayo inaweza ku-*compete* kwenye *market,* bado *product* zake zitakuwa na *inferior*. Ni vema zaidi hili suala tuliangalie upya, tuchukue jitihada za makusudi kuwasaidia *Private Sector* namna ya kuweza ku-*improve* na kuweza kuchukua masoko haya ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema hata tukaanzisha kampeni maalum ya ku-*market our products.* Nashangaa unakuta tunaanzisha malumbano na vyombo vya habari kwa *non issues!* Tuseme, jamani nyie watu wa habari mtusaidie ku-*promote our products.* Ingekuwa ni kitu cha muhimu sana kuliko kugombana. Tunagombana kwa kazi gani? *Lets work out* tuone kwamba tuna-*improve* namna gani *products* zetu. Watu wa *media* watusaidie kwa sababu wao wana vyombo vya kutusaidia kuweza kutangaza soko la bidhaa za Tanzania. Pia, watu kama *TIC* watusaidie zaidi, wamefanya kazi nzuri sana, lakini waongeze juhudi zaidi. Hii itakuwa ni njia rahisi ya kuweza kusaidia Watanzania tukaweza kupata mapato makubwa sana.

Suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa ni namna gani Watanzania tunaweza vile vile kujiimarisha kwa ndani. Mikoa ambayo iko pembezoni itafutiwe namna ya kuweza kushirikishwa katika suala zima hili la *Cross Boarder Trade.* Leo hii mikoa kama ya Mara, Mwanza na Shinyanga wakivuna mahindi kwa wingi soko lao la kuuza mahindi hayo ni Kenya, lakini baada ya siku mbili wana njaa. Kama ni mahindi tunayo au kama ni mpunga tunao, mchele tu-*add value* ili tunapouza nje yawe na *value* kubwa. Leo hii tunataka kuuza mifugo nchi jirani tunasema kwamba hapana, mifugo yetu ni migonjwa. Tunasema hivyo badala ya kui-*promote* kwanza mifugo hiyo ili tuweze kupata soko zaidi nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshukuru sana sisi tujivunie *products* zetu. Watanzania tumekuwa *endowed* na *products* nyingi sana, *resources* zetu ni nyingi sana tukianzia kwenye madini, samaki, mbuga za wanyama na kadhalika. Ningeshukuru sana kama Wizara hii ambayo ni mpya itatumia nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga tena mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na kuwa viongozi wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Jumuiya nzuri yenye maadili mazuri tukizingatia vyema mambo ya shirikisho na kujali na kukarabati bandari zetu kwa matajiri kupitisha bidhaa zao bila kupitisha katika bandari za wenzetu pia kutumia viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutoe elimu kwa wafanyakazi wa Jumuiya hii na kuleta ushindani wa aina zote za uwekezaji, biashara na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya hii ya Afrika Mashariki iione Tanzania kama Serikali ya Muungano kwa maana ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Basi Wizara hii iangalie kuwa na Zanzibar ina haki ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi waliokuwa wanadai kwa maana waliwahi kufanya kazi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na walifikia muda wa kustaafu na wakawa hawakulipwa mpaka sasa au leo, naomba sana Wizara hii isimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Jimbo la Magogoni, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Andrew Chenge, kuwa Waziri wa Wizara hii. Uzoefu wa siku nyingi katika maandalizi yote ya kanuni, taratibu, sheria na mikataba yote ya Jumuiya yetu hii, kwa kiasi kikubwa ni yeye aliyehusika.

Tunampongeza na kusema kweli Wizara imempata mwenyewe akisaidiwa na mwanadiplomasia, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, pia uteuzi wa Katibu Mkuu na safu yote ya Wizara, tunaiunga mkono wa dhati. Naunga hoja mkono kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maeneo ambayo ningeomba kumshauri Waziri wa Wizara ayazingatie ili kuleta hali ya usalama na maendeleo mema ya Jumuiya hii. Kwanza ni kuimarisha uongozi wa Bunge letu na lile la nchi wanachama. Mikutano au

semina za mara kwa mara zitumike ili kuondoa baadhi ya mawingu yanayosemwasemwa, kama nitakavyoyaelezea kwa ufupi hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zetu zote kiuchumi zinatofautiana na kwa msingi huo, nchi kama Tanzania inaweza kujiona kama hawawezi kupambana na Kenya na tukidekeza hilo, tunaweza kudumaza maendeleo yetu na hivyo ni vema Wizara ikaliangalia hili na kuja na mkakati wa jinsi ya kupunguza pengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar imekuwa ikidai uwakilishi katika shughuli za Jumuiya. Hapa panahitajika ufafanuzi zaidi ili hapo baadaye Zanzibar isije ikawa kikwazo katika Jamhuri yetu ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kikaundwa chombo ambacho kitakuwa kinaratibu maendeleo na matatizo ya utekelezaji wa mikataba na makubaliano katika Jumuiya yetu. Chombo hiki kinahusisha nyanja mbalimbali za wataalam wa nchi zote hizi na kipitie pia baadhi ya kasoro zinazojitokeza na kuziwasilisha kwa jopo la Mawaziri husika wa Afrika ya Mashariki. Chombo hiki kiangalie masuala yake *independently*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira kuna wanajumuiya wa kutoka nchi za Kenya na Uganda nalo linaweza kuzua migogoro na hasa inapotokea kazi nyingi zikaja kushikwa na wenzetu wa Kenya au Uganda na baadaye wa Burundi na Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Forodha ni budi ukapewa uzito unaostahili na tukiutumia vizuri tunaweza kunufaika na fursa zinazotokana na sisi kuwa wanachama. Kinachotakiwa ni kitengo hiki kipate wataalam waliobobea katika mambo ya biashara ili *programs* na mipango iliyobuniwa ya maendeleo ilete matokeo mema kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Afrika ya Mashariki zimeoanishwa na kupewa kipaumbele. Kwa kuwa barabara kati ya Nyakanazi, Kasulu hadi Tunduma imepewa umuhimu wa tano, je, kuna mpangilio wa utekelezaji wake na ratiba nzima ya kuonyesha kila moja itaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali yetu kwa kuendelea kuzitengeneza kwa kutumia fedha zetu wenyewe na wahisani, taarifa za kila nchi katika nchi zao kwa barabara hizi zinaratibiwa vipi na sisi tunajulishwa vipi kama Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa *East Africa Power Master Plan* unawezaje kutekelezwa kama nchi zetu zinaendelea kutegemea nguvu za nishati kwa mabwawa na mafuta mambo ambayo gharama zake ni kubwa na za wasiwasi kutegemeana na hali ya hewa na mfumo mzima wa uzalishaji wa mafuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa msingi huu kwa nini wazo la kuwa na *Nuclear Power Plant* kwa nchi hizi usibuniwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri atufahamishe nini matazamio ya nchi zetu katika kufikia Shirikisho la Afrika Mashariki mapema zaidi?

Tatizo liko wapi na kwa nini Kamati iliyoteuliwa isifanye kwanza kazi ya kuelimisha wanajumuiya kwanza na baadaye kuitisha kura ya maoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka tufanikiwe katika Jumuiya hii ni budi tujipange upya na tukubali kufanya biashara *(aggressively)* katika mazingira ya kushindana kwa ubora wa bidhaa na bei ya kuvutia wateja. Hatuna njia ya mkato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kuipongeza Serikali kwa kuunda Wizara hii mpya ambayo ni muhimu sana kiuchumi na uhusiano wa nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwamba Wizara hii ni daraja muhimu katika kuunganisha Serikali na sekta binafsi na wadau wengine kwa ujumla kuhusu masuala ya Afrika Mashariki, wananchi wanategemea kwamba watafaidika na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini mpaka sasa juhudi ya wananchi kwenye ushindani ni ndogo kuliko washiriki wengine wa Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara ikisimamia mikataba, ni muhimu kutazama upande mwingine wa uchumi kwamba uchumi unakua Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanategemea masoko yaliyoko kwenye nchi zote tatu zinazounganisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tatizo ni kwamba Tanzania inatumiwa na wenzetu kununua bidhaa Tanzania huku Watanzania hawanunui chochote Kenya au Uganda. Tatizo kubwa ni *Exchange Rate,* thamani ya fedha yetu ni chini sana ukilinganisha na pesa ya Kenya. Elimu ya forodha ni ndogo na wananchi kuona kwamba ni chombo cha kukusanya fedha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tanzania ina ardhi kubwa, ina amani ambacho ni kivutio kikubwa kwa wawekezaji, ina rasilimali nyingi ambazo bado hazijatumika. Lakini pamoja na hayo yote, bado tunakaa kimya huku tukiorodhesha matatizo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kosa kuwaongoza Watanzania kwenye Jumuiya bila kutoa elimu kwa wananchi na kuwaingiza kwenye chombo ambacho hawafaidiki nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi kuhusu wananchi wengi ambao wako mpakani hawajui biashara ya mifugo yao wanayiouza Kenya huku Kenya wao wamewawekea watu wao sheria na utaratibu, lakini sisi Watanzania tunaokaa mpakani tukinyonywa na wafanyabiashara wa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wanatumia mifugo ya Kenya kwa asilimia 60 na kuonekana wanafanya biashara nje ya nchi huku wanatumia utajiri wetu. Watanzania hawaelewi ni kwa nini tuko kimya. Naomba maelezo, ni kauli ya wananchi wa mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti yetu ni kubwa sana na tofauti hiyo inatuumiza sana. Sikuona mikakati ya suala hili, kilichofanyika, nakubaliana na matatizo yote yaliyobainishwa. Naomba ufafanuzi kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ametoa mtazamo wa wananchi kwamba kukuza utajiri, kuinua hali ya maisha ya wananchi wa Afrika Mashariki, kukuza uchumi na kujenga ushindani wa Kanda katika ngazi ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kueleza baadhi upungufu wa eneo letu kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki:-

(i) Ushindani huu ni mgumu kwetu kutokana na wenzetu kuwa na elimu na taaluma ya juu zaidi kuliko Watanzania.

(ii) Wafanyabiashara wa Kenya na Uganda wana ujuzi zaidi kibiashara na kutumia Tanzania kama soko lao, bila Watanzania kutumia masoko yao.

(iii) Vigezo vya Forodha ambavyo vinawabana sana Watanzania mipakani na watumishi wetu wa Forodha ni wazito kuhudumia wafanyabiashara kwa haraka.

(iv) Kushuka kwa sarafu yetu kunawanyima Watanzania kufanya biashara na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba tumeingia Jumuiya ya Afrika Mashariki huku Watanzania bado hawana uzoefu wa kutosha katika biashara ya Kimataifa. Wananchi ambao wako mpakani wanaona na kusikia Jumuiya hii kama miujiza au hadithi tu huku Wakenya wakiendelea kumiliki biashara wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, kwa nini bidhaa za Tanzania haziuzwi Kenya huku bidhaa za Kenya zimejaa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko yote ya mpakani yanamilikiwa na Wakenya huku wakinunua bidhaa kwa bei wanayotaka wa wenyewe.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutamka kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge na Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Pili, nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge na viongozi wakuu watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kuhusu suala la *(Fast Tracking)* Ushirikiano wa Kisiasa yaani kupata Shirikisho la Afrika Mashariki *Political Federation*. Kwa maoni yangu tunapaswa kuwa waangalifu zaidi katika kushughulikia suala hili kwani utaratibu uliopo kwenye mkataba wa Afrika Mashariki wa hatua kwa hatua ni muhimu sana kwa kujenga imani, maelewano na ushirikiano kamilifu zaidi. Tukumbuke Msemo wa Kiswahili usemao haraka haraka haina baraka na imani huzaa imani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba unataka tuanze na Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja *(Common Market)*, Sarafu ya Pamoja *(Common Currency or Monetary Union)* na hatimaye Shirikisho la Kisiasa. Hii haina maana lazima twende pole pole *(Snail's Pace)*, bali hatua kwa hatua, zinaweza kuwa hatua za haraka na ndefu/pana, lakini msingi ni hatua kwa hatua. Tukipitia hatua zilizowekwa na Mkataba tutapata Shirikisho bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za kuchukuliwa ardhi au ajira ni za msingi na sio woga bali kujenga imani ya kuaminiana. Ukija nyumbani kwangu kutaka tuwe marafiki, lakini unammezea na kumkodolea macho kwa uroho mke wangu, nitaukataa urafiki huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uanachama wa Burundi na Rwanda na pengine *DRC,* waingie tu mradi wanazingatia vigezo. Hoja ya vurugu au tamaa zao za kujipanua siyo za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeandaa mwongozo *(guidelines)* wa kutathmini athari za mazingira *(EIA)* za miradi inayotegemea rasilimali zilizo pamoja na Ziwa Victoria, mbuga za wanyama za Serengeti na Masai Mara na kadhalika. Mwongozo huo ulikamilika mwaka 2004, je, mwongozo huo umepitishwa rasmi? Kama ndivyo, ni miradi gani ya maendeleo katika nchi hizi tatu iliyo mipakani imezingatia mwongozo huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile kuna Tume ya Ziwa Victoria, inayotakiwa kusimamia maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii katika Ziwa hilo, je, hadi sasa Tume hiyo imefanya kazi gani wakati ambapo tunaendelea kuona uwekezaji holela kama vile katika sekta ya viwanda vya maua kandokando ya Ziwa, uvuvi holela na kadhalika vyote hivi vikiwa vinachangia uchafuzi wa Ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile uvuvi hasa ule wa kibiashara unatekelezwa na nchi zote tatu katika Ziwa Victoria na kwa vile masalio ya viwanda hivyo vya minofu (mapanki) ni mengi sana na bugudha kubwa katika kuyafadhili *(disposal)* kwa nini viwanda vya animal au *chicken feeds* visiundwe kutumia masalia hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekretarieti ya Jumuiya ya Mashariki imebaini taasisi mbalimbali kuwa *centres of excellence.* Taasisi hizo ni pamoja na Chuo cha Wanyamapori, Mweka. Je, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ina mpango gani wa kuzitumia taasisi hizi na ni vipi nchi yetu inaweza kufaidika kutokana na taasisi hizi kuchukuliwa na *EAC?*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Nafahamu uwezo wa Waziri, Mheshimiwa Andrew Chenge na uwezo wa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, hivyo sina wasiwasi juu ya

usimamizi wa majukumu yaliyomo kwenye Wizara hiyo nyeti. Jukumu kuu la Wizara hii kama ilivyojionyesha kuwa Tanzania inanufaika kwa kikamilifu kutokana na ushiriki wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wetu katika Jumuiya hii uinufaishe nchi yetu, tusiwe watazamaji na washangiliaji wakati wenzetu wanavuna rasilimali zetu. Wizara hii na Wizara zingine zitoe elimu ya kutosha ili wajue ni kwa nini tumeunda upya Jumuiya hii ni kwa manufaa gani, bila elimu ya kutosha Watanzania hawatanufaika na Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kama nilivyoeleza kuwa ina majukumu makubwa hivyo maamuzi ya haraka yafanywe ili kuweza kupata watalaam (watumishi) kufuatana na mahitaji katika kuwapata watumishi hao 40 waajiriwe kufuatana na sifa wala siyo mtoto wa fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati watalaam wakifikiria maombi ya Rwanda na Burundi kujiunga na Jumuiya, yapo masharti ambayo yanatakiwa yatimizwe lakini pia suala la usalama nalo lingeangaliwa kutokana na historia ya nchi hizo. Ili tunufaike na Jumuiya hii ni lazima kuwe na agenda maalum ya kukuza uchumi, sambamba na hilo suala la elimu ni muhimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu suala la elimu ni suala nyeti sana na Serikali imetenga shilingi milioni 400 tu kwa ajili ya kupata maoni ya wananchi, fedha hizo hazitoshi kama kweli inataka kupata maoni ya kweli nashauri kiasi hicho kiongezwe. Zipo Tume mbalimbali zilizoteuliwa kupata maoni kwa nchi nzima hazikutengewa kiasi kidogo kama hicho zilitengewa zaidi ya bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mwenyezi Mungu aniwezeshe kuchangia katika Wizara hii ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze kutoa mchango wangu kwa kuwa nchi zetu kwa pamoja zimekubaliana kuunda kwa Wizara hii. Kuwepo kwa Umoja wa Forodha ni hatua muhimu sana kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama chombo cha kiuchumi na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejengeka kwa kuwa na Marais wawili yaani Rais wa Muungano na Rais wa Zanzibar. Kwa kujua hili ni vyema basi Serikali ya Muungano itueleze ni njia gani Serikali ya Zanzibar inavyoshirikishwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kujua lengo la Jumuiya ni kukuza uchumi nchi zetu jambo ambalo Zanzibar kiuchumi iko nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ipo nyuma kiuchumi ukilinganisha Kenya na Uganda. Kuondoa kodi ya bidhaa ni vyema tungeelezwa, je, nchi yetu imejizatiti ama

imejiandaa vipi kutokana na msamaha wa kodi za bidhaa unaotolewa na Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika kuna mafanikio mengi yaliyopatikana na kwa mfano sekta ya kilimo, miundombinu, nishati, elimu, mazingira, maliasili, utalii na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Tanzania, je, imefaidika na lipi kati ya mambo yaliyopo hapo juu? Serikali ikumbuke ili ijiwekee wasiwasi juu ya Jumuiya hii. Hii inatokana na kuwepo tangu Jumuiya hii. Tanzania, Kenya na Uganda zilishirikiana na kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Historia ipo na imo ndani ya mioyo ya Watanzania, ukilinganisha wenzetu wametuzidi kiuchumi na hata kielimu. Serikali yetu ina umadhubuti gani kwa kujua ama uhakika kwamba matatizo yaliyojitokeza zamani na kusababisha kuvunjika kwa Jumuiya hii yamerekebishika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia kila la kheri Wizara hii.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima wa afya na kuniwezesha kuchangia hotuba hii. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wake wa Waziri anayeongoza Wizara hii. Pia kwa kuweka Wizara hii ikiwa inajitegemea. Pia nimpongeze uongozi wote wa Wizara kwa kufanikisha hotuba hii ambayo imeweka waze majukumu, malengo na mategemeo ya Taifa na kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hotuba hii na kwa uongozi wa Wizara uliowekwa na Mheshimiwa Rais umma wa Watanzania una imani kubwa, matatizo na migogoro iliyokuwepo na itakayotokea itatatuliwa kwa ufanisi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa Jumuiya hii ilikuwepo na ikavunjika ambapo ilisababisha usumbufu mkubwa wa wafanyakazi waliokuwa wakitumikia Jumuiya hiyo na wengine wamefika kwenda mbele ya haki bado hawajapata haki zao. Kwa hiyo, hivi sasa kuwe na mikakati madhubuti kwa mambo ambayo yatakuja kuleta kero baadaye, yazingatiwe mapema hasa kwa vile tunayafahamu na tunajifunza kutoka kwa Jumuiya iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti pia namwomba Mheshimiwa Waziri kuishauri Serikali iharakishe zoezi la kukamilisha malipo ya wafanyakazi waliofanya kazi katika Jumuiya iliyopita ili kusafisha na kuitangaza zaidi Jumuiya hii kwa jamii nzima ambapo hivi sasa kuwa watu wakisikia jina hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu hayo machache naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* ya mwanzo iliyoundwa mwaka 1967 na ilivunjika mwaka 1977. Zanzibar ilikuwa mwanachama licha ya kuwa imo katika Muungano wa

Tanzania ulioundwa 1964. Leo Zanzibar haimo katika Jamuiya hiyo mpya ambayo ni Jumuiya ya kiuchumi. Kwa kuwa nia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuisaidia Zanzibar kiuchumi, naishauri msaada wa mwanzo na wa maana ni kuiruhusu Zanzibar kuwa mwanachama na hasa ukitilia maanani kuwa baadhi ya mambo yaliyomo katika Jumuiya hii hatuwezi kuwakilishwa na Tanzania kwa sababu si ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha, imerejesha ushuru wa mafuta ghafi ya kupikia kutoka nje. Sababu kubwa ni kuvilinda viwanda vyetu vinavyozalisha mafuta ya kupikia. Kwa msingi huo ipo haja ya kuliangalia kwa makini zaidi juu kuruhusu bidhaa kutoka nchi wanachama bila ya kulipia ushuru. Kwa hali hiyo na kwa ushuru wa bidhaa hasa ya kwa nchi ya Kenya. Viwanda vyetu vitakufa na badala yake Tanzania itakuwa ni soko la bidhaa kutoka nchi wanachama wa Jumuiya hii. Ahsante.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya Rwanda na Burundi ukurasa wa 36 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Hili lazima liangaliwe kwa umakini mkubwa kwa sababu zifuatazo:-

(1) Nchi hizi mbili hazina *stability* kisiasa. Ni wagomvi na wamezoea vurugu wakati Tanzania ni kisiwa cha amani. Hatulingani wala hatufanani.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani Rwanda walidai kuwa Wilaya nzima ya Karagwe ni sehemu ya Rwanda. Siamini kuwa wazo hilo wamelifuta. Wanaweza wakatuletea matatizo siku za usoni kama Idi Amini alivyofanya.

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hizi ni ndogo kijiografia, wangependa kutanuka na ndiyo maana Wanyarwanda wamejaa Karagwe na sehemu nyingine za Mkoa wa Kagera/ pia mifugo yao imejaa Mkoa wa Kagera na kuharibu mazingira yetu na hata kusababisha ugomvi. Ahsante.

**MHE ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ya bajeti pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie eneo la wafanyakazi na iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Naomba mfuatilie kwa makini kuna baadhi ya wafanyakazi wa zamani wa Jumuiya hiyo hadi leo hawajalipwa mafao yao na hasa Mamlaka ya Bandari na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Nawapongeza pia Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

(1) Serikali lazima iwe na mwamko wa kibiashara na kujipanga kusaidia wafanyabiashara waweze kufanya biashara nje ya mipaka ya Tanzania. Kwa kuwa tumeridhia ushirikiano wa Afrika Mashariki na sasa bidhaa nyingi kutoka nchi moja kwenda nyingine ushuru wa forodha umeondolewa lakini wafanyabiashara wanaopeleka bidhaa Kenya wanasumbuliwa sana mipakani ili wakate tamaa huku Serikali ya Kenya ikihimiza na kuwasaidia wafanyabiashara wake kuuza bidhaa zake Tanzania.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hizi *Non Tariff barriers* zinakomeshwa na mikataba ya makampuni binafsi ambayo Serikali haijui na ambayo inakataza uuzaji wa bidhaa kati ya nchi na nchi hasa *Tanzania Breweries* na *East African Breweries,* Kenya inatangazwa kuwa *NULL and VOID?*

**MHE ALI HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Nawapongeza viongozi wetu walioona umuhimu wa kufufua na kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mtazamo au lengo la kuunda Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu tu ni sababu zipi Tanzania sisi mwanachama wa *COMESA, IGAD* na *IOC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha mkakati wa tatu cha mwaka 2006-2010 kinatosha kufanya utafiti wa nyanja mbali mbali za ushirki au na kubaini vikwazo na utatuzi uimara na maendeleo yake?

Mheshimiwa Mwenyekiit, kuhusu *East African Customs* (Umoja wa Forodha wa Jumuiya). Shauri hili limejadiliwa kwa kipindi kisichopungua miaka minne kwa sasa ndilo jambo pekee limekubalika na limeanza kwa sasa ni matatizo gani yanaikabili Tanzania kiuchumi, kiutendaji, kijamii na kisiasa? Kwa vile Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeanza kufanya kazi zake pamoja na mapungufu kama yapo. Ni mahusiano gani yaliyopo na uundwaji wa *East African Currency Board*? Shauri hili litafikiriwa baada ya kuundwa Shirikisho la Afrika Mashariki au kabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Waziri.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuungana na wale wote ambao wanakupongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hotuba nzuri hasa ukitilia maanani kwamba ni Wizara mpya. Kwa mantiki hiyo naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Napenda nichukue fursa hii nami nitoe indhari kwa kosa lililojitokeza katika picha ya Ramani ya Afrika Mashariki ambayo ndio kielelezo cha Gamba la Kitabu cha Bajeti cha Wizara. Katika mahusiano ya Tanzania na Malawi kuna mgogoro wa mpaka *(Demarcation)* katika Ziwa Nyasa ambapo Malawi inatambua mpaka huo kuwa ufukweni mwa Ziwa upande wa Tanzania, kama ambavyo ramani hiyo inaonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mtazamo wa ghafla suala hili linaweza kuonekana kuwa dogo lakini si dogo kwani pamoja na mazungumzo yote ya kidiplomasia kulitatua tatizo hili, bado halijatatuka. Sisi Tanzania mpaka tunaoutambua ni kinyume na ilivyo kwenye ramani iliyochapishwa kwenye kitabu. Naomba Mheshimiwa Waziri atafute jibu la kidiplomasia na kulirekebisha kosa lililofanywa na mchapishaji wa kitabu na hatimaye ramani husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba Rwanda na Burundi bado hazijawa mwanachama wa Afrika ya Mashariki lakini bado ramani iliyochapishwa imeziingiza nchi hizi katika ramani hiyo. Nchi hizi kujiunga na Jumuiya hii kwa maoni yangu si jambo baya sana kwani nahisi Jumuiya itazidi kuwa imara na hasa ukitilia maanani hivi sasa duniani karibu kila nchi kwa namna moja au inatafuta au inajiunga na umoja uwe wa kisoko (kibiashara) au vinginevyo. Masuala ya bandari, anga, mambo mengine ya huduma pamoja na masoko ni faida Tanzania itazopata kwa Rwanda na Burundi kujiunga.

Kwa mchango huu mchache, nimalizie kwa kuunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. Hii ni Wizara mpya na bila shaka mnakabiliwa na matatizo mapya ambayo kwa pamoja Wabunge tunatakiwa kusahihisha baadhi ya maeneo na hatimaye tuipitishe na kwamba waidhinishiwe fedha walizoomba. Natanguliza shukrani.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Burundi na Rwanda zimekuwa zikitamani kujiunga na *EAC*. Bahati mbaya kabisa nchi tatu mwanachama yaani Tanzania, Kenya na Uganda nazo zinashabikia kujiunga kwa nchi hizi mbili ndogo bila kuangalia athari zake kijamii na kiujirani.

Hoja siyo soko tu, lazima soko lijikite katika misingi ya usalama na zaidi ujirani mwema. Nchi hizi za Burundi na Rwanda hazina sifa hata kidogo kuwa (kwa sasa) *members* wa *EAC* wapewe masharti ili iwe ndiyo sifa ya kujiunga na sisi katika *EAC.* Nchi hizo bado zina matatizo ya kiusalama, ubaguzi wa kikabila na ubaguzi wa madaraka. Zipewe sharti la kusafisha nyumba zao kwa mfano, nchini Rwanda Serikali yake ni ya kibaguzi, ya kibabe na kamwe wao dhana ya utawala bora haipo. Ni *minority vs majority. How do such government qualify for the EAC?* Au ni kufanya *EAC* sehemu ya kujificha? Rwanda wapewe sharti la kumaliza tatizo la wafungwa zaidi ya 600,000 walioko gerezani kwa hisia za kikabila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Burundi ipo shwari ni mfano mzuri wa utengamano wa kijamii (makabila yote Wahutu na Watusi). Napendekeza *strongly* wapewe muda ili wajipange vizuri na taasisi zao za utawala ziimarike (Polisi, Mahakama zao, Usalama).

Suala la kujiunga na *EAC* lisiwe la papo kwa papo na kamwe tusikaribishe nchi kufanya maficho ya maovu yao ya utawala mbovu.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, historia inatueleza kuwa wakazi wa Afrika ya Mashariki walishirikiana sana katika nyanja

mbalimbali kama za mawasiliano uchumi na kiudugu. Lakini baada ya nchi hizi kupata Uhuru wao kutoka kwa wakoloni, tofauti za itikadi na mtazamo ziliibuka na kusababisha mahusiano yale mazuri, yaliyokuwa yamejengeka wakati wa ukoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano endelevu, lazima uanzie kwa wananchi wenyewe na sio uanzie kwa viongozi. Ushirikiano wa sasa, kati ya Tanzania, Kenya na Uganda ambao unaelekea kuunda shirikisho la Afrika ya Mashariki, ni mawazo ya viongozi wetu na wananchi hawajawahi kushirikishwa katika maamuzi haya. Kuna hatari ya malengo kutofanikiwa, kwa kuwa wenye nchi yao hawakushirikishwa katika maamuzi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo zuri sana kuunganisha nchi ili kuleta maendeleo ya haraka, lakini wakati tukifanya hivyo, lazima tuzingatie maslahi ya nchi. Sehemu moja inaweza kuwa inataka muungano kwa ajili ya kupanua masoko yake pia ajira kwa watu wake. Kipimo cha maendeleo ya kiuchumi na elimu ni kigezo muhimu kabla ya maamuzi. Leo hivi Kenya ina viwanda vikubwa vikubwa na wasomi lukuki, vipi Tanzania itafaidi muungano huo wakati wasomi hatuna wala viwanda hatuna?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya maamuzi mazito kama haya ya muungano kufikiwa, ni vyema wananchi wakashirikishwa katika maamuzi hayo. Tusione aibu kusema ukweli, muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ulikuwa ni mawazo ya viongozi wawili, wananchi hawakushirikishwa. Mpasuko unaozungumzwa kila siku katika muungano wetu na Zanzibar ni sababu ya wananchi kutoshirikishwa katika maamuzi hayo. Kwa msingi huu, muungano wa Afrika ya Mashriki utapata matatizo haya haya tuliyo nayo na Zanzibar. Ni vyema basi tuchukue tahadhari kabla hatujafanya makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,mimi naunga mkono ushirikiano, lakini kabla hatujafanya hivyo, tuwashirikishe wananchi. Kwa sasa hivi nina wasi wasi mkubwa, tunahitaji muda mrefu zaidi kutafakari huo muungano kabla ya kufanya maamuzi. Je, kweli ni sawa kushirikiana na nchi kama Uganda ambao hawataki demokrasia ya vyama vingi, je, ni sawa kwa viongozi kama hao ambao hawaamini kuachiana madaraka? Nchi yetuni tulivu, hakuna vita ya wenyewe kwa wenyewe, kwa hiyo, ni vyema tuwe waangalifu sana kabla ya kutafuta mfarakano.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa hotuba yake yenye mwelekeo wa mafanikio na mimi napenda kutoa mchango wangu mdogo kwa Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nijikite upande wa biashara. Nchi zetu hizi tatu, Kenya, Tanzania na Uganda, kwenye nyanja hii ya uchumi wa kibiashara inaonyesha kwamba Kenya na Uganda zimetuzidi kiuchumi wa aina hiyo. Je,

Mheshimiwa Waziri hakuna hatari ya kuja kuwa wananchi wa Tanzania ni wateja tu wa bidhaa zitokazo nchi hizi mbili Kenya na Uganda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali inaonesha kuwa wenzetu wa Kenya na Uganda wameshajitayarisha kwa kuwaelimisha wananchi wao, je, Tanzania nayo imeshawatayarisha wananchi wake kuhusu kukabiliana na hali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania tunazo Serikali mbili ya Muungano na ile ya Zanzibar, kutakuwa na faida zipi kwa Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama wa nchi yetu. Ushikiriano wa Afrika Mashariki ni mzuri, lakini lazima nchi yetu isisahau usalama wa wananchi wake na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa wananchi wa Tanzania wanasumbuliwa sana na majambazi. Hali hii kuna hatari ya kuja kuongezeka wakati wananchi wa nchi zetu hizi watakapopata fursa kubwa ya kusafiri kuingia nchini bila kibali maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujiunga na Jumuiya hiyo ya Afrika kwa Burundi na Rwanda, kwanza waangaliwe vya kutosha kwani nchi hizo hazijakuwa na usalama wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MUSSA AZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii, natoa ushauri wa kuwa wananchi wengi sasa hivi bado hawajaelimishwa kuhusu mpango mzima wa *community,* elimu itolewe kwa wananchi kupitia Waheshimiwa Wabunge wao na wajue faida zake.

**MHE. MOHAMMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba kuzungumza mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, hali ya mahusiano katika Mikoa ya mpakani na nchi za Afrika Mashariki. Katika miaka ya nyuma kulikuwepo na utaratibu wa Mikutano ya ujirani mwema ambayo ilisaidia sana kuzungumzia masuala ya usalama, upendo na ulinzi katika mipaka yetu. Hali haipo hivyo hivi sasa. Nashauri utaratibu ule ungefufuliwa tena.

Pili, hali ya huduma katika mpaka wa Horohoro ni mbaya hasa ukosefu wa maji katika Kituo cha mpakani. Hii inasababisha wenzetu wa upande wa Kenya kufaidika sana na biashara katika eneo la upande wa Kenya. Nashauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Maji pamoja na Taasisi za *TRA,* Uhamiaji, Polisi ambao wana ofisi pale mpakani zisaidiane kuondoa kero hii.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kwa kuona umuhimu wa kuunda Wizara hii mpya na pia kwa kuwateua viongozi wenye upeo wa juu kujenga muundo na msingi imara wa Wizara hii mpya. Mheshimiwa Waziri Andrew Chenge, Mheshimiwa Dr . Diodorus Buberwa Kamala, Naibu Waziri na Katibu Mkuu mahiri Ndugu Bendera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado lipo tatizo kubwa kwa Watanzania wengi kutojua mwelekeo na utendaji wa chombo kinachoongoza Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ili kutoa mwanya ningeshauri leo Mheshimiwa Waziri alieleze kwa ufupi Bunge hili na Taifa la Tanzania mambo yafuatayo:-

(1) Jinsi Bunge la Afrika Mashariki linavyofanya kazi na vikao vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi wanaona jinsi mikutano na vikao vya Bunge lao la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hata Baraza la Mapinduzi Zanzibar linavyofanya kazi. Sijawahi kuwasikia Watanzania wakizungumzia kuona katika vyombo vya habari kama *Television* au hata Redio kusikia Bunge la Afrika Mashariki likiendesha kwa uwazi mikutano na vikao vyake, iwapo inaendeshwa kimya kimya ni kwa nini sasa tusianzishe mpango wa uwazi kama ambavyo Watanzania wanaona na kusikia Mabunge yao ya Tanzania na Zanzibar? Kama halifanyiki nashauri mpango ufanyike na lianze mapema.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwakilishi wa muundo wa Bunge la Afrika Mashariki, idadi ya Wabunge ndani ya Bunge la Afrika Mashariki ni ndogo sana kutoa uwiano mzuri wa uwakilishi wa wana Afrika Mashariki. Ili kuliimarisha Bunge hilo nashauri yafuatayo:-

(i) Uwakilishi wa Kisekta. Zianzishwe sekta muhimu za kiutendaji za mambo ya kuanzia utekelezaji wa pamoja wa Jumuiya ya Ushuru wa Forodha, kama tulivyoainisha Ushuru wa Forodha, Mahakama za Rufaa za Afrika Mashariki na kadhalika.

Pamoja na kuwa watendaji wa kisekta kutoa ushauri kwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki bado uzito hautoshi. Ni vema kuwa na uwakilishi mzito zaidi wa kudumu ndani Bunge la Afrika Mashariki Kisekta ikibidi iwe hivyo kwa kuanzia.

(ii) Mabunge ya nchi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lianzishe siku maalum ya *agenda* ya maendeleo ya mikakati ya utekelezaji wa mambo muhimu ya Afrika Mashariki. Kwa njia hii wawakilishi wa wananchi yaani Wabunge kujua na kujadili kwa undani zaidi mambo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivi sasa Bunge linapewa taarifa tu lakini hakuna fursa za majadiliano. Haya ni mapungufu makubwa.

(iii) Kuunda vyombo vya pamoja na ushiriki wa pamoja kukabiliana na mambo muhimu yanayoendeshwa katika mikutano na Jumuiya mbalimbali kama *WTO, European Union* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunakusudia kuelekea kutekeleza muundo wa Shirikisho la Afrika Mashariki ni vema tuweke msimamo wa pamoja katika vyombo muhimu vya Jumuiya na Taasisi mbalimbali za Kimataifa kwa manufaa ya wana Afrika Mashariki wa leo na kesho.

(iv) Kuhusu kuunganishwa kwa barabara muhimu, mapendekezo ya kuboresha barabara muhimu za kuunganisha Afrika Mashariki ni muhimu sana kabla ya kukamilika kwa Shirikisho. Ni vema Mheshimiwa Waziri leo akatueleza juu ya mpango wa utekelezaji wa uboreshaji wa barabara hizo na kama fungu au bajeti ya kazi hiyo imepitishwa na fedha kutengwa kwa utekeleza kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti,baada ya ushauri huo naunga mkono hoja.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Wizara hii mpya kwa kufanikisha hotuba hii ambayo leo Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa hiari yake imeamua kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mara nyingine tena baada ya Jumuiya hii kuvunjika miaka ya nyuma. Tanzania imeundwa kutokana na nchi mbili yaani Tanganyika na Zanzibar ikiwa kama nchi ilikuwa imefungwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari mafanikio ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki yameanza kuonekana. Moja ya mafanikio hayo ni pamoja na kuwepo kwa Mkataba wa Uchunguzi wa Barabara *(Tripartite Agreement on Road Transport)* ambayo mkataba huo umesainiwa ili kuwa na mtandao wa barabara imara unaounganisha nchi zetu tatu yaani Kenya, Uganda na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa mtandao wa barabara jumla ya kilometa 15,273 na orodha ya barabara hizo umeonyesha kwenye ukurasa wa 21 na 22 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Katika mradi huu Zanzibar haina hata mradi mmoja wa barabara kwa maana nyingine ile azma ya Zanzibar kufaidika na mradi huu haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Zanzibar iweze kufaidika katika mtandao wa miundombinu kwa nini kusiwepo na utaratibu wa kuanzisha *Roro Ferries* kati ya Dar es Salaam - Zanzibar - Pemba hadi Mombasa pamoja na kuimarishwa kwa barabara kuu zinazounganisha bandari moja hadi nyingine Visiwani humo. Kwa mfano, barabara ya Mkokotoni - *Zanzibar Town* kwa upande wa Unguja na Mkoani, Wete kwa upande wa Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa Bandari Visiwani ni moja ya faida watakazonufaika wananchi wa Zanzibar kutokana na Jumuiya hii ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo kwa miradi kama hiyo kwa upande wa visiwani hivyo ni dhahiri kuwa Zanzibar watakuwa hawanufaiki sawasawa na Jumuiya hiyo japokuwa kutakuwa na faida nyinginezo zitakazotokana na Jumuiya hizo kwa mfano kuanzishwa kwa Mradi wa *East African Submarine Cable System (EUSSY).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iitetee Zanzibar vilivyo ili kuondosha manung'uniko kwa upande mmoja wa Jamhuri yetu wakati Jumuiya itakapokuwa kwenye *full swing.* Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona katika uchangiaji wetu wa jumla hapo ndiyo tumefikia mwisho. Sasa naomba kwa heshima na taadhima nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri aanze kujibu hoja na atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri mtoa hoja. Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki kwa kujibu baadhi ya hoja. Lakini kabla ya kufanya hivyo, nichukue nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Waziri, asubuhi ya leo alitoa hotuba nzuri na alitoa shukrani na pongezi kwa viongozi mbalimbali, nami niseme naungana naye mstari kwa mstari, neno kwa neno, koma kwa koma na nukta kwa nukta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuniteua katika nafasi hii. Naomba nimhakikishie kwamba nitajitahidi kadri ya uwezo wangu wote. Pale nitakapoteleza ajue labda maji yamemwagwa njiani na pale nitakapoanguka basi ajue nimesukumwa. Asisite kunishika mkono na kuninyanyua ili niendelee kutembea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge, Waziri wa Afrika Mashariki kwa kunilea katika Wizara hii, kwa kunifundisha Serikalini watu hufanya kazi namna gani na kwa kweli nazidi kujifunza sana kutoka kwake na msishangae siku moja mkisikia na mimi nakuwa Profesa wa Sheria kwa sababu niko na Kamusi ya Sheria ya nchi hii na kila siku najifunza. Kwa hiyo, siku moja mkisikia naitwa Profesa wa Sheria msishangae, mjue nitakuwa nimejifunza sana kwa Mheshimiwa Andrew Chenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Nkenge kwa jinsi walivyonichagua kwa kishindo mwaka 2000 na kura zile za mwaka 2000 zikasababisha niweze kupita bila kupingwa mwaka 2005.

Natambua wako wengi ambao wangependa kuwa Wabunge wa Jimbo la Nkenge na wana uwezo, lakini wameona ni vizuri niendelee. Nawaomba basi waendelee na moyo huo huo ili niweze kuendelea kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Nkenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Katibu Mkuu wa Wizara yetu, Ndugu Bendera, kwa kazi nzuri anayofanya na wasaidizi wake. Mwisho,

siyo kwa umuhimu bali ni kwa utaratibu, nimshukuru mke wangu kwa jinsi anavyonisaidia kuweza kutumikia wananchi wa Jimbo la Nkenge na kufanya shughuli zangu za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kujibu hoja mbalimbali zilizojitokeza. Mheshimiwa Paul Kimiti ametoa hoja nzuri na nyingi. Hatuwezi kuzijibu zote, lakini nyingine tutazijibu kwa maandishi. Hoja mojawapo amesema kwamba, ni lazima tuwe na mikakati ya kuwezesha nchi yetu ili tuweze kushiriki vizuri katika Afrika Mashariki na tusiwe na mawazo ya kufikiri kwamba sisi tuko nyuma na hatuwezi kushindana na Kenya na Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwa asilimia mia moja. Niseme tu kwamba Watanzania hatuna haja ya kuwa na wasiwasi kwamba hatuwezi kushindana kibiashara na Kenya wala na Uganda kwa sababu takwimu zilizopo zinaonyesha tunafanya vizuri. Tafiti mbalimbali zilizofanywa na Benki ya Dunia, zilizofanywa na *International Monetary Fund,* zilizofanywa na watafiti mbalimbali zinasema nini. Tafiti hizo ukiziangalia haraka haraka zinakuonyesha kati ya mwaka 1999 - 2002 uchumi wa Tanzania umekuwa ukikua kwa wastani wa asilimia 6.3, huku wa Kenya ukikua kwa asilimia 1.3 na wa Uganda ukikua kwa asilimia 3.8. Sasa hakuna haja ya kuwa na wasiwasi kwa mtu ambaye uchumi wake unakua kwa asilimia 1.3 wakati wa kwako unakua kwa asilimia 6.3. Unachotakiwa kufanya ni kuongeza jitihada zaidi ili walau uchumi wetu sasa ukue zaidi ya asilimia kumi na tuweze kwenda kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wapo ambao wamekuwa wakisema kwamba Kenya wana viwanda vingi. Lakini takwimu na tafiti zinaonyesha kwamba kwa Kenya viwanda vinachukua asilimia 15 ya Pato la Taifa, kwa Tanzania viwanda vinachangia asilimia 14 ya Pato la Taifa na kwa Uganda viwanda vinachangia asilimia 14 ya Pato la Taifa, kwa hiyo, tofauti ni asilimia moja. Kwa mikakati tuliyonayo, nina uhakika tutaweza kuchangia zaidi na viwanda vitakua zaidi kuliko hata wenzetu wa Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia haraka haraka tafiti zilizofanyika zinaonyesha kwamba mwenendo wa utendaji kazi katika mashirika mbalimbali Tanzania tunafanya vizuri. Utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia na kuchapishwa Kimataifa na unakubalika ni kwamba utendaji wa mashirika kati ya nchi 25 za chini ya Sahara, Tanzania mashirika yetu yanafanya vizuri zaidi. Tanzania ni ya tisa kati ya 25, lakini Kenya wao ni wa 21 kati ya 25 na Uganda ni wa 18 kati ya 25, lakini bado sisi tuna wasiwasi! Ukiangalia hata kwa mwenendo wa uchumi kwa ujumla wake ni kwamba kati ya nchi 25 sisi Tanzania ni wa tisa, Uganda ni wa 14 na Kenya ni wa 15. Lakini bado tunakuwa na wasiwasi na Kenya na Uganda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tangu tulipoingia kwenye ushuru wa forodha, mambo yameenda vizuri kama alivyoeleza Mheshimiwa wa Wizara yetu kwamba, mapato ya Tanzania kutokana na ushuru wa forodha yameongezeka kwa asilimia 52, lakini siyo hiyo tu, vile vile mapato kwa ujumla yameongezeka kwa asilimia nane. Siyo hiyo tu, mauzo yetu ndani ya Afrika Mashariki yameongezeka kwa asilimia

30. Pia siyo hiyo tu, manunuzi yameongezeka kwa asilimia 24. Siyo hiyo tu, ukiangalia vile vile sera zetu za Tanzania za Kupambana na Umaskini na Kukuza Uchumi ni bora kuliko nchi yoyote ndani ya Afrika Mashariki na nitaeleza kwa ufupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna MKUKUTA. MKUKUTA tulionao unakubalika Kimataifa na unafanya kazi nzuri kuliko mipango waliyonayo wenzetu. Nyote mnafahamu, kupitia Wizara ya Kilimo tuna mpango mkubwa ambao utatumia zaidi ya shilingi trilioni mbili ambazo tunazielekeza moja kwa moja kwenye kilimo maana ukikuza kilimo, unataka kukuza uchumi.

Pia, nyote mnafahamu tuna Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara tunaita MKUMBITA. Kwa mara ya kwanza haijawahi kutokea katika historia ya nchi hii, tunapeleka zaidi ya shilingi milioni 500 kila mkoa na mipango mingine ipo na nyote mnafahamu kwamba mtandao wetu hata wa barabara ni mzuri kuliko nchi yoyote ndani ya Afrika Mashariki. Ndiyo maana leo hii vyombo vya habari vimeeleza kwamba baadhi ya Wakenya wamekuja kushangaa barabara za Tanzania zikoje na tutawaelekeza ni namna gani tunafanya. Kwa hiyo, Watanzania tusiwe na wasiwasi na tusijione wanyonge kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya tutaweza kushindana vizuri ndani ya soko la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paul Kimiti ametoa hoja nyingine nzuri kwamba, ni vizuri Bunge la Afrika Mashariki likashirikiana na Bunge letu hili, ni kweli. Ukiangalia mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kifungu cha 65 kinaeleza kwamba: "Katibu wa Bunge la Afrika Mashariki anawajibika kuleta taarifa za mwenendo na mijadala mbalimbali ya Bunge la Afrika Mashariki." Niseme tu kwamba, tutalisimamia hilo ili tuweze kulitekeleza. Lakini vile vile Spika wa Bunge letu na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki wamekuwa wakishirikiana kwa karibu. Tunayo *East Africa Inter-Parliamentary Committee* na mambo mengine tutazidi kuyafanya ili tuzidi kuendelea zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwepo hoja ya kwamba, tuunde chombo kingine cha kusaidia kutekeleza masuala mbalimbali ya Afrika Mashariki. Niseme tu kwamba kwa hivi sasa ukiangalia mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kuna vyombo mbalimbali vinavyoanzishwa na hiyo *Treaty*. Kuna *Summit,* kuna *Council of Ministers,* kuna *Coordination Committee* ya Makatibu Wakuu, kuna *Sectoral Committees* na hivi sasa tunazo 17, kuna *Secretariat* yenyewe, lakini vile vile kuna Bunge la Afrika Mashariki na Mahakama. Hivi vyombo vyote kazi yake ni kuwezesha kusaidia Jumuiya ya Afrika Mashariki iende vizuri. Kwa hivi sasa hivi vyombo kwanza havijafanya kazi, kazi zilizopo ni kidogo, kwa hiyo, isingekuwa vizuri kwa sasa kuunda chombo kingine ingawa huko mbele ya safari wazo lake la kuunda chombo kingine tunaweza tukalitazama na kuona tunaweza kufanya namna gani. Lakini kwa sasa vyombo vilivyopo vinatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ya ajira imejitokeza na Mheshimiwa Paul Kimiti ameiongelea. Lakini niseme kwa ufupi tu kwamba kwa hivi sasa hatujaingia kwenye soko la pamoja. Kwa hiyo, sheria zetu zinazohusu masuala ya ajira, zilizopo

bado zinaendelea kufanya kazi na niwakumbushe tu kwamba hata Mheshimiwa Waziri anayehusika na masuala ya uhamiaji na vibali vya kutoa kazi alieleza hapa kwamba, wataweka msukumo kuhakikisha kwamba taratibu zilizopo zinafuatwa. Kwa hiyo, tutaendelea kuzifuata. Lakini tutakapoanza majadiliano ya kuingia kwenye *common market,* basi tutahakikisha kwamba Watanzania hatuwawekei mazingira mabaya ya kupoteza ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba pamoja na kufanya hayo ni vizuri tukaanza maandalizi ya kuweza kupambana na ushindani, siyo tu katika Afrika Mashariki, bali katika Afrika hata nje ya Afrika na ushahidi uliopo unaonyesha kwamba Watanzania wanafanya kazi nzuri sana wanapokuwa nje ya Tanzania. Tunafahamu kule Botswana, ukienda kwenye Vyuo Vikuu vya huko, Profesa anafahamu pale, Maprofesa wengi ni Watanzania na wanafanya kazi nzuri. Pia ukienda maeneo mengine unakuta Watanzania wengi. Kwa hiyo, tusije tukafikiri kwamba sisi Watanzania hatuwezi kushindana na wenzetu, uwezo upo, kinachotakiwa ni kujipanga vizuri ili tuweze kunufaika na hii Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu kwenda haraka haraka kuzipitia baadhi ya hoja. Kuna hoja ya kwamba tutumie vizuri fursa ya ushuru wa soko la pamoja. Ukiangalia watu ambao wametumia fursa ya soko la Afrika Mashariki, ukiangalia kwa haraka haraka utakuta kwamba waliochukua zile hati ili kuweza kufanya biashara ndani ya soko hilo ni makampuni 177. Lakini nilipochunguza zaidi nikagundua Tanzania tunayo makampuni zaidi ya 50,000 yaliyoandikishwa kufanya biashara. Kwa hiyo, kati ya makampuni 50,000 ambayo yana uwezo wa kufanya biashara Kenya na Uganda ni makampuni 177 tu ambayo yamefanya biashara hiyo. Kama walau makampuni 10,000 yangeweza kujiingiza kwenye biashara hii, maana yake tungeweza kufika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka Arusha ambao wametumia hiyo fursa ni makampuni matatu, Dar es Salaam 128, Iringa manne, Mara matatu, Morogoro sita, Kilimanjaro saba, Shinyanga matano, Tanga matano, Mwanza saba, Mtwara moja, Zanzibar mawili, Pemba moja, Kagera moja, Dodoma sitaki kusema, Singida sitaki kusema na mikoa mingine nakaa kimya ili nisionekane naonyesha kwamba hawachangamkii fursa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema ni kuwaomba wana Afrika Mashariki watumie fursa hizi. Ninachojifunza kutokana na takwimu hizi ni kwamba labda wapo wengine wanaofanya biashara na hatujawaweka kwenye takwimu zetu, lakini vile vile wako baadhi ya Watanzania wanaendelea kufanya biashara kupitia njia za panya bila kujua kwamba tumeshawaruhusu wafanyabiashara bila kulipa kodi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka ili niweze kumaliza. Mheshimiwa Herbert Mntangi, ametoa hoja nzuri kwamba tushirikiane na Bunge la Afrika Mashariki. Nimeshaeleza suala hili. Lakini vile vile ameuliza kwamba utekelezaji unaanza lini wa zile barabara tulizoeleza. Ninachosema ni kwamba Mheshimiwa Waziri wa

Miundombinu ndiye anatekeleza, sisi tunachofanya ni kuweka mikakati na kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha kujenga hizo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko tunashukuru kwa hoja yako. Umesema tuwe makini kuwapokea Rwanda na Burundi. Hoja yako ni nzuri na tutaizingatia kwamba ni lazima vigezo vifuatwe na kwa kweli vigezo vipo. Kuna kigezo cha utawala bora, kuna kigezo cha demokrasia na mambo mengine, yote hayo tutayatazama kabla ya kufikia uamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aloyce Kimaro hoja yake kwamba baadhi ya makampuni yanaingia mikataba kuzuia bidhaa zisiuzwe nchi nyingine ni nzuri, tumeipokea na tunaifanyia kazi na tutaifanyia kazi kwa ari mpya, nguvu mpya na kwa kasi mpya hatimaye uweze kupata jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho naweza kukuhakikishia hivi sasa ni kwamba kuna Muswada wa *Competition* ndani ya *East Africa,* utajadiliwa hivi karibuni na Bunge letu na ziko taratibu nyingine ambazo tunaweza kuzitumia kurekebisha hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, tunashukuru kwa hoja zako. Lakini ulisema kwa kuwa tumerudisha ushuru wa asilimia kumi kwa mafuta ghafi, basi hivyo hivyo tuzuie bidhaa zote zinazotoka Kenya zisiingie Tanzania, tuziwekee ushuru. Ile ya mafuta ghafi ni kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiit, tumefanya hivyo kwa ajili ya kulinda wazalishaji wetu wa mbegu wa ndani, lakini kwa mambo mengine lazima tuendelee kufanya biashara na ambacho nasema hapa ni kwamba huwezi ukafanya biashara ya kuuza tu, ukifanya biashara lazima uwe tayari kununua na lazima uwe tayari kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, ameleta hoja kwamba wapigakura wakewengi waliokuwa wanafanya kazi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hadi sasa baadhi yao hawajalipwa. Tunasema kwamba Wizara ya Fedha imesikia na sisi tumesikia tutawakumbusha ili waweze kulimalizia tatizo hilo kwa sababu mpaka sasa hivi wanalifanyia kazi. Kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Abbas Mtemvu, kwa kutetea wapigakura wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Richard Ndassa, hoja zake ni nyingi na nzito. Ameelezea kwamba kuhusu Rwanda tuwe makini, tutakuwa makini. Lakini vile vile akasema shilingi milioni 400 zilizotengwa kwa ajili ya kukusanya maoni ya Watanzania ni fedha kidogo, tunashukuru sana kwa kuliona hilo, lakini bajeti yetu ndivyo ilivyo ila tutawaomba kadri tunavyokwenda ili bajeti hii iweze kuongezeka kadri mambo yatakavyokuwa yanajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, kwa mchango wake mzuri alioutoa ndani ya Bunge hili. Tunamshukuru sana na amesema, Watanzania lazima tupende bidhaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakubali, tuwe na mikakati mbalimbali ya kuweza kuwawezesha Watanzania kushiriki Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Nami nakubali na ninasema naam, hiyo ndiyo kazi tuliyopewa kufanya. Tutaifanya siyo sisi peke yake, bali kwa kushirikiana vile vile na Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujibu hoja hizo ambazo tulikubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba ndizo niziongelee, basi nimalizie tena kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushuru sana. Naomba sasa nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri. Karibu mtoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa mara ya pili kwa kunipatia nafasi hii tena mchana huu ili niweze kufanya majumuisho kwa mchango ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge katika hoja hii ambayo iko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nakushukuru wewe na Mheshimiwa Job Ndugai, nilisahau kusema kitu kimoja tu kwamba ninyi wote Wenyeviti wawili kwa upande wangu ni watani zetu. Kwa hiyo, naamini kwamba ninyi kukalia nafasi hiyo ambayo Bunge hili limewapeni, ni heshima kubwa ambayo mmepewa na babu zenu Wasukuma. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii kwa maandishi na baadaye nitawatambua kama ilivyo kawaida Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii kwa kuongea humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Herbert James Mntangi na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Alhaji Ali, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa John Pombe Magufuli na mwisho kwa kutajwa lakini kwa umuhimu wa mchango ni Mheshimiwa Dr. Maua Daftari. *(Makofi)*

Waliochangia kwa kuongea humu Bungeni ni Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Dr.

Raphael Chegeni na mwisho na kwa umuhimu huo huo Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na moja kubwa la shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge katika michango yao waliyosema humu ndani, sote tumewasikia lakini wale waliotoa mchango wao kwa maandishi wametoa mchango mzuri katika maeneo mbalimbali ya mchakato wa Ushirikiano wetu wa Afrika Mashariki. Wametoa maangalizo, wametoa maoni, wametoa ushauri wa busara na wa hekima sana katika eneo hili muhimu, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja pia zimekuwa nyingi, nitajitahidi kwa kadri nitakavyoweza kuzijibu zote kama muda utaruhusu lakini pale ambapo kengele itanikuta kabla ya kumaliza itabidi nitoe ahadi kwamba kwa wale ambao hatutakuwa tumeweza kuwajibu hoja zao kwa utaratibu ule ule ambao tunatumia siku zote, tutawaandikia majibu ili waweze kuyapata mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru sana katika michango hii, mnatusaidia kuyasema ambayo sisi hatuwezi kuyasema. Mmesema suala la Bajeti, amelisemea vizuri pia Naibu Waziri. Lakini hicho ndicho tulichoweza kupata kwa sasa. Lakini naamini Serikali haitaweza kukubali ikwamishe shughuli zake muhimu kwa faida ya wananchi wa Tanzania ndani ya Afrika Mashariki kwa sababu ya kutoweza kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sentiment* ambazo nimezipata kutoka Wizara ya Fedha, kwa sababu tunajua zoezi ambalo tunataka kulianza tarehe 15 Septemba, 2006 ni zoezi kubwa. Hatuwezi kuwahadaa wananchi tukafika katika maeneo mengine lakini tusifike katika maeneo mengine. Tunataka tuhakikishe Watanzania wanapewa fursa ya kutoa maoni yao kwa ufanisi na ukamilifu na ili tuweze kufanya hivyo, tunahitaji tuwezeshwe vya kutosha. Naamini hilo litafanywa. Sasa ya baadaye tutayaone mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwepo tangu wakati wa mchango wa Wizara ya Biashara na Viwanda, huko nyuma katika Wizara nyingine na leo limeletwa hili la *COMESA* na *SADC*.

Mimi nataka niwe *technical*, Wizara yangu haishughuliki na masuala ya *COMESA* na *SADC,* lakini haimaanishi kwamba Wizara yangu hatuyafahamu hayo, maana yana mwingiliano haya. Itifaki ya Umoja wa Forodha inatamka wazi kabisa kwamba, lazima hizi jumuiya za kikanda kwa sababu ya kanuni za *WTO* na kanuni kwenye maeneo mengine kama *EU,* mazungumzo ya *EPA (Economic Partnership Agreement)* nchi ambayo ni mwanachama tayari katika umoja fulani wa forodha, hairuhusiwi kuwa mwanachama wa umoja mwingine wa forodha. Hiyo ndiyo misingi.

Ukitaka kuona mantiki yake, ni kwamba, wewe tumekubaliana pamoja kwamba tutakuwa na wigo wa pamoja kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi zetu kama wanachama wa umoja huo kama kwa Afrika Mashariki tumeweka *Common External Tariff* ya asilimia 25 ya ushuru wa forodha. Sasa wewe huwezi ukaenda ukapata maafikiano na

nchi nyingine ukataka kubomoa uwigo ambao tumeujenga kwa pamoja. Sasa changamoto ambayo unaiona kwa wengi ni kwamba, unataka kujaribu ikiwezekana ambavyo tunajua ni ngumu kweli kwa sababu ili muwe wote kwa pamoja, wale ambao mko *COMESA* na huku mko *EAC* wale ambao mko *SADC* na huku mko *EAC* unaweza usivunje kanuni hizo iwapo utahakikisha kabisa kwamba ile *Common External Tariff* mtakayoifikia hatimaye ilingane na ile ya kwako ya uanachama wako wa kwanza (*rules of origin),* ule uasili wa utambuzi wa bidhaa na wenyewe zifanane kama zile za uanachama wako wa kwanza, ule utaratibu wa *Customers Coding* na wenyewe ufanane. Hii ni kazi ngumu kweli kweli na ndiyo maana tunasema ni afadhali tukafuata kanuni hizo za *WTO.* Lakini tuseme kwa upande wa Tanzania ndani ya Jumuiya ya Afrika tujivunie ndugu zangu, sisi tumefikia Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki, *SADC* na *COMESA* hawajafikia na wako mbali kweli jamani.

Lingine, niwaambie ndugu zangu, kwa haya, kwa kadri mnavyokuwa wengi katika Jumuiya moja, inavutia sana kwa sababu mnapanua soko. Lakini kama hamjafikia hii *Common Customers Union,* mazungumzo ya kufikia *Common Customers Union* kwa sababu mko wengi, inakuwa kazi kweli kweli! Ndio maana ninaomba Bunge lako Tukufu lielewe kwamba sisi tuna kitu cha kujivunia na naamini kazi iliyoko mbele ya safari kwa upande wa wanachama wa *COMESA* na sisi Tanzania ambao tuko *SADC* tunajua ni kazi kweli kweli. Lakini lazima tuifanye.

Nimalizie eneo hili kwa kusema mawili. Kwa mujibu wa itifaki ya Umoja wa forodha ya Afrika Mashariki ni wajibu wetu kuleta muungano, hii *convergence* katika *economic arrangement* ambapo sisi ni wanachama. Ni wajibu wetu. Sasa Mikataba hii iko pale kuheshimiwa, tusiwe watu wa kwanza kuvunja mikataba ambayo sisi wenyewe tumeingia kwa hiari yetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme tu kwamba, namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, ndugu yangu, mdogo wangu; Mheshimiwa Dr. Kamala - Naibu Waziri wangu na wengine wote ambao wanaonyesha imani kwangu ni kweli nimekaa nimekuzwa na Serikali hii, nimesomeshwa na nchi hii. Mchango wangu mdogo ni huu wa kuweza kutoa ushauri pale ninapoweza.

Kwa hiyo, tunayoyafanya haya ni kwa faida ya nchi yetu kwa kadri ambavyo naweza. Sasa kwenye maeneo ambayo siyo ya kwangu, nasema nisingelipenda sana nirudi kuingia katika himaya za Mawaziri wengine. Lakini nalikumbuka moja na ndiyo maana huwa linauma sana. Mimi huwa sipendi kuficha ukweli.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kujioa *COMESA* hatukukurupuka tu. Wale ambao mnapenda kufuatilia magazeti ya miaka ya nyuma, taasisi za Sekta Binafsi ndiyo zilikuwa zinashinikiza Serikali kwamba hatunufaika na *COMESA,* tujiondoe. Leo ni Taasisi hizo hizo zinaigeukia Serikali zinasema Serikali inapoteza mapato mengi sana kwa kujitoa *COMESA*. Ndio maana lazima tuwe makini na waangalifu sana kwa masuala kama haya. *(Makofi)*

Sisi tunasema wamefanya ule utafiti kama alivyosema Mheshimiwa Karamagi, naomba sana wasiendelee kulalamika kama walivyofanya huko nyuma, walikwenda Wizara ya Viwanda na Biashara, wakawasilisha hoja yao ikaiva, Waziri mwenye dhamana na Wizara hiyo wakati huo akapata nguvu ya kwenda kwenye Baraza la Mawaziri, kujenga hoja na ikakubalika hoja hiyo. Kwa hiyo, tunaomba wafanye hivyo hivyo kama wanaona sasa ipo sababu ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Zanzibar katika mchakato mzima huu wa Afrika Mashariki, nianze labda kwa kurudi nyuma kidogo. Hoja hii imechangiwa na Wabunge wengi sana, nikianzia na rafiki yangu Mwanasheria mzuri, Mheshimiwa Abubakar Bakary ndiyo amesema kwa niaba ya Upinzani, hoja hiyo ameisemea vizuri tu, lakini pia na baadhi ya Wabunge waliochangia kwa maandishi na wenyewe waligusia hoja hiyo.

Lakini narudi nyuma kidogo kwa sababu Mheshimiwa Riziki Omar Juma wakati anatoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusiana na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, aliligusia pia suala hili, lakini alileta katika sura ambayo siku ile mimi lilinistua kidogo. Nataka nimnukuu kidogo yale ambayo katika *statement* yake nanukuu: "Jumuiya ya Afrika Mashariki inafanya maamuzi yanayoiathiri Zanzibar. Mfano dhahiri ni kuhusu kodi ya forodha ambayo siyo ya Muungano, lakini Serikali ya Muungano ikajadiliana na Kenya na Uganda kuhusu Umoja wa Forodha bila kujali kuwa Zanzibar inapaswa kuwa mshiriki mkuu. Je, haya tunayafanya makusudi?" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hili, napenda nisaidie, maana anayetoa kauli mara nyingi ni kutokufahamu. Katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, mambo ya Muungano yameainishwa katika *item* ya 10, inasema hivi: "Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya forodha."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano, sasa sio vizuri tukaanza kupindisha ukweli. Kwa hiyo, ushuru wa forodha ni suala la Muungano na ndiyo maana tumelichukulia katika sura hiyo, kwamba tunatambua kabisa kwamba ni suala la Muungano.

Lakini pia tunatambua Tanzania ni tofauti sana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kenya na Uganda, kwa sababu sisi ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hiyo ni tofauti kubwa. Kusema kweli mimi nakubaliana kabisa na hoja za Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar, Mheshimiwa Abubakar Bakary kwamba Zanzibar kwa mambo ambayo siyo ya Muungano ina mamlaka kamili. Hilo halina ubishi kabisa, Zanzibar ina mamlaka kamili kwa masuala ambayo siyo ya Muungano kwa Zanzibar na hili lazima tuendelee kuliheshimu, maana tusipofanya hivyo, tutawachanganya wananchi. *(Makofi)*

Lakini napenda niseme tu, hapa tulipofikia katika mtangamano wa nchi zetu tatu, ni kwamba, tunatekeleza mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tumeshavuka hatua ya kupata maoni ya wananchi kuhusiana na *whether* Tanzania iingie katika Jumuiya hiyo ya Afrika Mashariki. Tumeshavuka huko.

Wananchi walipewa fursa ya kutoa maoni kati ya mwezi Mei, 1998 mpaka mwezi Aprili, 1999 mwaka mzima. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati ule anasimamia *port folio* hii aliifanya kazi hii kweli kweli! Amekuja Bungeni kuelezea kila hatua tuliyokuwa tumefikia, mfumo unaopendekezwa na kwa nini unapendekezwa. Hivyo, alikwenda kwenye Baraza la Wawakilishi, akajieleza na akarudi tena hapa akatueleza na wananchi walio wengi wa Kenya, Uganda na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakasema tuingie, huko ni kwema, huko ni salama. Katika dunia ya leo hatuwezi tukakaa kama Kisiwa. Lakini tunatoa maangalizo na tutaendelea kutoa maangalizo katika hoja ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachosema, Zanzibar haiwezi ikaingia yenyewe kama mwanachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkataba wenyewe, yaani *treaty* ambayo kwetu ndiyo sheria, inatambua, inawataja, Ibara ya tatu ya Katiba yetu, maana hii ni Katiba, labda tuibadilishe na utaratibu uliowekwa, inasema: "*Members of the Community in this treaty.*" Wanachama wa Jumuiya ya Afrika kwa mujibu wa Mkataba huu ambao wataitwa *partner states, shall be The United Republic of Tanzania, The Republic of Kenya and The Republic of Uganda and any other country granted membership to be Community under this article.* Kwa hiyo, hata dhana ya wanachama shiriki au shirikishi, *(associate membership)* na yenyewe lazima uwe ni nchi ambayo inatambulika kimataifa kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

Sasa mimi nisingelipenda hili tulikuze sana, lakini mimi nirudi katika hoja kubwa ambayo ndiyo ya msingi ambayo nasema Zanzibar lazima iendelee kupewa hadhi yake katika kuamua masuala ambayo yamo katika mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa suala la msingi hapa, Serikali zetu mbili zimeweka utaratibu upi ambao una hakikisha kwamba haya ambayo siyo ya masuala ya Muungano, kweli Zanzibar inashiriki kikamilifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ambao uliopo kama ilivyo katika Miungano mingine katika Dunia hii, maana ni nchi huru zimeungana au zimekubali kushirikiana, zitakuwa zimeweka utaratibu wa namna ya kushirikiana kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi na Serikali ya Muungano wa Tanzania, ambayo na yenyewe inasimamia masuala ambayo siyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania Bara. Utaratibu tuliojiwekea ni mashauriano.

Sasa katika hili la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kabla ya vikao vyote, kwanza kuna Mawaziri mahususi ambao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imewateua kwa shughuli hii, tena ni Mawaziri imara kweli kweli. Naupongeza uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi katika kuteua timu hiyo na mchango wao mpaka sasa katika Mikutano yetu inakuwa mizuri. Lakini Mikutano hiyo inakuwa mizuri zaidi inapoboreshwa na ushiriki wa Watalaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda vizuri na sijawahi kuletewa malalamiko na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwamba hapa imewaburuza. Kama alivyosema Dr. Kamala na utaratibu huu ambao haujaleta matatizo, ningeliomba sana tusiutumie kukwamisha shughuli za kutupeleka mbele kwa sababu kwanza muda hatuna. Dunia haiwezi ikasubiri kwa sababu eti Watanzania bado mnatafakari mambo yenu.

Tunachoomba ni kwamba pale ambapo tatizo linaonekana ni la msingi tunakutana mara moja. Watalaam wanashauri Serikali zetu hizi kwamba hii ndiyo njia muafaka ya kutufikisha kule tunakotaka kwenda. Lakini ya kusema kwamba hatujawa tayari, oh, wenzetu wamegundua mafuta na gesi kule Uganda; mimi nawatakia mema na sisi tunajua siku moja *inshallah* tutayapata. Lakini Watanzania tusianze kugombana kwa kitu ambacho hatujakipata. *(Makofi)*

Mimi naendelea kuishauri Serikali na Serikali zetu kwamba juhudi za kutafuta mafuta ambayo tunajua dalili ni nzuri, lazima ziendelee na ziendelezwe kwa nguvu zote, tukaribishe makampuni makubwa yenye uwezo, yenye teknolojia, yaje yaendeleze kazi hii kama wanavyofanya Uganda na Kenya. Lakini la msingi ndiyo tukubaliane tukishayapata ule mgao unakuwaje kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi? Hiyo hoja ina mantiki. Lakini tukianza kugombana kwa kitu ambacho hatuna, hata watu watashangaa ninyi Watanzania mkoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lingine nadhani Dr. Haji Mwita Haji huwa anakuwa makini sana. Mimi michango yake huwa naipenda sana. Leo nadhani ameghafilika tu, nadhani ulimi uliteleza, yawezekana mimi sikumwelewa au sikumpata vizuri. Alisema kwamba katika shirikisho lililovunjika, kwa sababu hatujawahi kuwa na shirikisho katika Afrika Mashariki, Mwalimu alijitahidi sana kuchelewesha uhuru wa Tanganyika ili kuwasubiri wenzetu wa Zanzibar, Kenya na Uganda ili tuweze kwenda pamoja katika shirikisho hili.

Nikiunganisha hapa hapa na yale ambayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani, yawezekana pia mimi siyo mwana historia mzuri, huwa napenda tu kuyasoma haya na kuyaelewa na mengine nimefunzwa, nawashukuru sana Marehemu Jamal, Mzee Msuya, Rais Mwai Kibaki, Balozi Lusinde, Marehemu Bomani, hawa ndiyo wametulea sisi tukiwa vijana sana. Mimi nimeanza Shule, nimemaliza Chuo Kikuu, kazi yangu ya kwanza ilikuwa ni masuala ya Jumuiya ile ya kwanza ya Afrika Mashariki kabla ya kwenda Marekani kusoma. Nimerudi nimekuta imeshazikwa.

Lakini lazima tuelewe historia na ndiyo maana sipendi kuamini ndugu yangu, rafiki yangu, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji hakumaanisha hiyo. Lakini tukiangalia zile tarehe zenyewe hapa, simjibu yeye, lakini najibu zile hoja nzuri za Kambi ya Upinzani. Zanzibar imepata uhuru wake kutoka kwa Wakoloni (Waingereza) tarehe 13 Desemba, mwaka 1963.

Sasa kipindi hicho kwa sababu wale ambao walikuwa wanachama wa chombo cha wakati ule ambacho kilikuwa kinajaribu kutuunganisha kilikuwa kinaitwa *The East*

*African Common Services Agreement,* maana ilikuwa ni mikataba mnasaini. Ni kweli Mwingereza alikuwa amesaini kwa niaba ya *Sultanate* ya Zanzibar. Uhuru wa kuwaondoa Wakoloni umekuja tarehe hiyo. Maana ya *succession,* ni kwamba unarithi na mikataba ile ambayo yule aliyekuwepo alikuwa ameirithi. Kwa Tanganyika, tulifanya hivyo, isipokuwa kwa mikataba miwili tu *Nile Waters Agreement* na mikataba ya Belbes kwa upande wa *Port* ya Dar es Salaam na Kigoma ni miwili ambayo tuliikataa, tukasema hatuitambui, lakini tuko tayari kuanza mazungumzo na wahusika.

Tulipoanza kuwauliza Waingereza na Wabelgiji, wakatuambia bwana nchi hizo zimejitawala, nendeni mkaongee na Misri, nendeni mkaongee na Sudan, nendeni mkaongee na Zaire, nendeni mkaongee na Ruanda na Burundi. Lakini kwa hali ya kwetu, Zanzibar sura yake ndiyo hiyo sasa, Januari 12 mwaka 1964 kipindi kifupi sana baada ya kumfukuza Mkoloni/Mwingereza, Mapinduzi halali ya Zanzibar yakatokea.

Mwaka 1964 tumo katika *East African Common Services* na tarehe 26 Aprili 1964, Muungano. Kwa hiyo, unaona kwa kile kipindi kifupi, sidhani kama yaliweza yakafanyika mengi ambavyo yanasemwa na Waheshimiwa Wabunge. Lakini hii ndiyo historia ambayo mimi naifahamu, naamini na ninyi mkienda kuisoma mtaikuta ipo tu. Sasa mimi nadhani tusiwe watumwa wa Historia. Kuna yale ambayo tunapaswa tuyafanye, lakini tuyafanye kwa misingi ya sheria ya kimataifa. Kama ni hoja nzuri, mimi nasema tusikilize hoja hiyo na tuielewe na tuone namna ya kushirikiana. *(Makofi)*

Nadhani nafasi ya Zanzibar mimi nasema kwa kipindi ambacho nitabahatika kuwa katika *position* hii ya Afrika Mashariki nitahakikisha kwamba kweli Zanzibar kwa mambo ambayo sio ya Muungano, tunakwenda vizuri na pale ambapo tunabidi kuhitaji muda wa kutosha ndani yetu sisi wenyewe ndani ya Muungano, kabla ya kwenda kuwaona wenzetu wa Kenya na Uganda tutawaomba wenzetu wa Kenya na Uganda watuelewe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi, lakini nisahihishe moja ambalo ni kosa langu, kwa sababu nilisahau kuwatambua watu muhimu sana. Maana usipomtambua Mwenyekiti au Mjumbe wa Mwenyekiti aliyetumwa kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje ambayo ndio imeyapitia haya maombi ya pesa hizi, nimetolewa taarifa, mimi nitakuwa sina wadhila na wala sina shukrani, sistahili kuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimtambue Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, kama miongoni mwa wale waliochangia. Pia, hapa hapa nimtambue rafiki yangu Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa eneo hili. Samahani sana ndugu zangu, nilighafilika, lakini nashukuru wamenisahihisha mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kwa kifupi faida. Jamani lazima nikubali, na ni hoja ya Waheshimiwa Wabunge wengi. Serikali, nyinyi watu wa *East Africa Community,* wananchi wa Tanzania na tunadhani hivyo hivyo kwa Kenya na Uganda hawajaielewa sana Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo tumeanza kuijenga. Ndiyo hoja inasemwa. Somo hili linahitaji kueleweka kwa wananchi ili waweze kuwaungeni mkono.

Kwa sababu kama mtu hajalielewa somo hata ukienda kumwomba kitu itakuwa ni kumwonea.

Mimi ndugu zangu nakubaliana kabisa na hili na juzi kwenye Kikao cha Mawaziri pale Arusha cha mashauriano haya na bahati nzuri tumepata Katibu Mkuu mpya, naye ana mawazo mazuri sana kwenye eneo hili. Lakini nianze kushukuru sana Bunge la Afrika ya Mashariki kwenye eneo hili. Wamefanya kazi nzuri sana ya kuhamasisha wananchi ili waielewe na kuiunga mkono Jumuiya yetu. Tunawashukuru sana kwa kazi hiyo. Tunaomba waendelee hivyo hivyo, wale ambao mmoja mimi nawaombeni mtakaporejea katika Jimbo lenu, *inshallah* Mwenyezi Mungu asikie dua zenu mrejeshwe. Wale mnaotaka kuingia na wenyewe nawaombeeni dua zenu *inshallah* Bunge liwakubali. Lakini lengo ni kwamba nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani mbele yetu huko, mimi naona dhoruba. Sasa ni vizuri tukajiandaa. Hawa tunaowapeleka katika chombo hicho cha Bunge la Afrika Masharika lazima wafanane na hali halisi hii ambayo tuna kesi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombeni sana kupitia kwako, Bunge lako Tukufu, hili suala tuliangalie kwa makini sana. Tusipofanya hivyo, tutajikuta mijadala ya mle ndani ya Bunge hilo, nashukuru kwa ridhaa ya Rais, mimi kwa wadhifa huu pia ni Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Kwa hiyo, kote kuwili, Mheshimiwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki alinitania akaniambia, hivi wewe unapeperusha bendera ngapi kwenye gari lako? Nikamwambia mimi najua moja tu, ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Hapana, lazima uweke na ya Bunge la Afrika Mashariki.
Sasa nikajiuliza, nikiweka ya Bunge la Afrika Mashariki, niweke na ya Serikali, niweke na bendera ya Jamhuri ya Muungano, sasa utakuwa na bendera tatu kwenye gari moja! *(Kicheko/Makofi)*

Na nikienda Jimboni, naweka na ya *CCM.* Lakini ndiyo hali ambayo najikuta nayo mimi. Lakini nawashukuruni sana kwa sababu ni sehemu ya changamoto ambayo lazima tuifanye ili kuhakikisha kwamba tunahakikisha Tanzania inanufaika na uanachama wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tujipange vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Msambya, suala la elimu Mheshimiwa Msambya, alinisahihisha akasema, yeye anaamini changamoto kubwa siyo ile ya tofauti ya maendeleo kati ya nchi zetu tatu. Mimi bado na-*stick* kwa kusema kwamba, ndivyo hotuba yangu inavyosema. Kwa sababu tusipokuza uchumi, ndugu zangu hata kama tusingelitaka kujiunga na Jumuiya yoyote, Tanzania itaendelea kuwa soko la bidhaa za kutoka nchi nyingine. Hilo lazima tulielewe. Hili ni ukweli usiopingika . Mimi hoja hiyo na mimi nimeisemea katika maneno tofauti. Maana nikasema pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kuandaa Watanzania kwa kuwawezesha, lakini ipo haja kubwa sana ya kuwekeza zaidi katika elimu.

Maana elimu bora, na mimi sisemi siyo elimu tu, jamani. Tunataka mwanafunzi wa Tanzania au anayemaliza iwe ni *Form Four, Form Six*, hasa Chuo Kikuu. Maana

dunia ya leo nawaambieni siyo ya *Form Four* na *Form Six,* ningelipenda tuendelee kuwekeza, tupanue. Najua wote hatutaweza kwenda Vyuo Vikuu, lakini kwa kadri iwezekanavyo, wale ambao wana sifa za kwenda Vyuo Vikuu, tuhakikishe wanakwenda. Tuwekeze kwa sababu elimu bora, lazima elimu bora inayomjenga mwanafunzi wa Tanzania anayemaliza kwamba anaweza akashindana, siyo Tanzania pekee na siyo ndani ya *East Africa* peke yake, lakini pia nje ya Afrika. Mimi ndiyo dhana yangu ya mtu aliyeelimika. Naishukuru sana nchi hii, Serikali hii Watanzania mmenisomesha, nimekwenda Harvard. Harvard huendi tu hapo hapo Chuo Kikuu cha Harvard. Nawashukuruni, nimesomeshwa na nchi hii.

Lakini ningependa wengi wasome kwenye Vyuo jamani. Mimi nasema tunaweza kuwa maskini, lakini siyo maskini wa akili. Tunayamudu haya na imedhihirika hivyo na tujiamini tu. Mimi ningelipenda elimu bora iwe kweli ni msingi wa kuweza kuyakabili haya ambayo yako mbele yetu kwa sababu wananchi katika Tanzania na katika Afrika Mashariki, watafaidika na hili tunalotaka kulijenga iwapo watakuwa na afya njema, watakuwa na elimu bora, watakuwa na ujuzi, watakuwa na sifa na uwezo wa kufanya kazi.

Kwa hiyo, mimi siko mbali sana na Mheshimiwa Msambya kwa hilo. Faida ziko nyingi katika maeneo haya. Mimi nimeainisha kwa upande wa Jumuiya, yale ambayo tumeyafanya. Kuna faida za mtu mmoja mmoja. Sasa hivi wafanyabiashara ingawa bado tuna kero nyingi sana katika baadhi ya sehemu za mipakani kule. Malalamiko tunayapokea mengi tu. Lakini zipo fursa za mtu mmoja mmoja za kutaka kwenda upande wa pili wa mpaka na kurudi kufanya shughuli zake. Tupunguze hayo mahangaiko. Lakini lipo hili kubwa ambalo tunalisemea sisi la ushirikiano wa kikanda ambao unawezesha watu na nchi kuhimili vizuri zaidi nguvu za kiuchumi katika dunia ya leo ya utandawazi.

Soko kubwa zaidi lina uwezo zaidi kuhimili misukosuko ya uchumi wa dunia hii. Pia, mnapokuwa soko kubwa, mnapokuwa wamoja, mnaongeza kauli na uwezo katika majadiliano ya kimataifa. Hasa nchi ndogo na maskini zinapounganisha nguvu kwa pamoja na rasilimali, zinapokuwa na msimamo mmoja zinapata uzito mkubwa wa kisiasa kuliko ambapo kila nchi ikisimama kivyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ushirikiano wa kikanda unasaidia kujenga uwezo wa kutumia fursa ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki na kwa nje ndani ya utandawazi. Kwa sababu mnapata uwezo wa kutengeneza miundombinu iliyo bora kwa maana ya barabara, bandari, umeme, simu, reli na kadhalika, pamoja na kuwekeza kwenye kuboresha nguvu kazi kwa mafunzo ya ufundi na ujuzi, elimu ya juu na utafiti, matumizi ya teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, kwa Kampuni za Kitanzania ambazo hazina uzoefu wa ushindani wa kimataifa, kama nilivyosema asubuhi katika hotuba yangu, zinapata fursa ya kushindana kwenye ngazi hii ya kwetu, uwanja wa kwetu huu wa nyumbani kabla sasa ya kwenda kushindana kimataifa. Ndiyo maana ya dhana hii. Kwa hiyo, tuitumie vizuri sana nafasi hii.

La tatu, ushirikiano wa Kikanda unasaidia kutuhimiza sisi wenyewe kama wanachama, masuala muhimu sana ya utamaduni wenye faida kama vile sera nzuri za kukuza uchumi na fedha, Masuala ya utawala bora, utawala wa sheria, kwa sababu tunaona mahali ambapo kuna utawala bora katika nchi hiyo na kasi ya maendeleo inakuwa ni nzuri. Tukiwa pamoja, tutasaidia sana katika kudhibiti uhalifu unaovuka mipaka. Maana anayefanya uhalifu hapa Tanzania akidhani anakimbilia Kenya au Uganda, mnakuwa na mtandao wa pamoja wa kuweza kujua na kumnasa mara moja, kuliko kama unafanya wewe peke yako. Nimeona niyasemee tu hayo, lakini yapo mengi kwenye upande wa utalii, Mheshimiwa Diallo aliyasema siku ile. Yapo mengi, tutayasikia.

Labda kabla sijafika hapo, Mheshimiwa Msambya ametoa *point* nzuri sana. Alinitahadharisha kwamba hiyo ramani ambayo iko katika ukurasa wa kwanza katika hotuba yangu, sio ramani ambayo inaonesha mipaka sahihi kama tunavyoifahamu sisi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kwanza niliombe radhi Bunge lako na pili niwaombe radhi Watanzania kwa hili. Lakini niwahakikishie mimi kama Mwanasheria Mkuu Mstaafu wa nchi hii, ambaye nimeyasimamia hayo, nafahamu fika kwamba mpaka wa Tanzania, mpaka kati yetu na nchi ya Malawi uko katikati ya Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maombi ya Rwanda na Burundi, nimesikia hoja hizo, lakini nawashukuru kila mtu jamani. Mwenyezi Mungu ametupatia kila mtu akili zake. Ndiyo Waswahili wanasema nywele ni dawa. Kila mtu ana akili zake. Nawashukuru kwa michango yenu. Wale mnaosema mnawaleta wa nini hawa? Wale ambao wanasema ndiyo, mimi nasema lazima twende kidogo kama viongozi wa nchi hii, tulione suala hili katika upana kidogo. Lakini nianze na moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema katika hotuba yangu, nchi hizi zimewasilisha maombi yake rasmi ya kutaka kujiunga na sisi. Nilitegemea Waheshimiwa Wabunge tungeshangilia, kwa sababu jumuiya hii inaanza kuonekana na wenzetu kwamba ina mvuto. Kwa nini watu waombe kama kitu siyo kizuri? *(Makofi)*

Lakini niseme, nimerudia tena kwenye hotuba yangu kwamba mkataba wa Umoja wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, unaweka utaratibu, kanuni na vigezo ambavyo anayeomba lazima afuzu. Asipofuzu, basi. Unasema kuna kuomba na kupata na kuna kuomba na kutokupata na hili chaguo, *treaty* iko *very clear.* Maana hawa watakuja kwa njia ya *acquisition.* Maana wameshavuka, tumesha-*ractify,* imeanza kutumika. Kwa hiyo, hakuna njia nyingine. Watakuja kwa njia hii ya *acquisition.* Sasa wana chaguo.

Ninavyolifahamu mimi, *unless* ni tatu kama mwanachama kamili, *full member* au kama huna hiyo, unakuja kama mwanachama mshiriki, kwa maana niliyoieleza kwa upande wa Zanzibar, lazima uwe ni nchi ambayo inatambulika kwa mujibu wa sheria za

kimataifa. Kama hili unaliona, tena ni vigumu kwako, *treaty* inakwambia unaweza ukashiriki katika baadhi ya miradi na programu ambayo Jumuiya ya Afrika Mashariki inatekeleza. Wewe utachagua na sisi tutakupima kwa maeneo hayo.

Lakini vigezo hivyo, wale ambao mtapata nafasi, wale ambao mna mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Ibara ya 3 (iii) paragrafu ndogo (a) - (f) zinaainisha yale masharti, utayakuta mengi ni utawala bora, utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu na kuhakikisha kwamba panakuwa na *Social Economic Policy Convergency.* Yaani sera zetu kwa masuala ya kiuchumi na kijamii yafike mahali kama tunashabihiana. Haiwezekani ukajenga jumuiya ambayo mko *far apart.* Kwa hiyo, ni la msingi sana hili. Lakini maombi haya bado yanafanyiwa kazi.

Mimi nakubaliana na wasiwasi unaotolewa. Hapa kweli yapo matatizo. Ni kweli sio vizuri matatizo ya vita na vurugu hizo kama zipo katika maeneo, baadhi ya maeneo ya maziwa makuu yakahamishwa hapa. Hakuna anayependa kitu cha namna hiyo. Lakini tuliangalie *on the opposite side* kwa sababu kumalizika kwa vurugu na vita hivyo katika ukanda huu wa Ziwa, eneo la Maziwa Makuu ni kwa faida yetu Watanzania. Maana ndiyo tume-*dare the grunt* ya vurugu za kule. Wanazalishwa wakimbizi huko sisi ndiyo tunapokea.

Lakini kama alivyofanya Marehemu, Mheshimiwa Baba wa Taifa, ambaye amesimamia mpaka Mwenyezi Mungu amemwita, suala hili kwa sababu aliliona kwamba *there is no solution* kwa hawa, isipokuwa kuhakikisha kwamba amani ndani ya nchi hizi inapatikana na sisi kama viongozi wa Taifa hili la Tanzania ambao tumebahatika, sasa ni vizuri tukaendeleza moto huu wa kusema hawa lazima tuhakikishe kwamba wanayoyafanya nyumbani kwao tuwasaidie kuyamaliza. Lakini ufunguo wa kuyamaliza matatizo yao wanao wao wenyewe. Sisi ni wa kusaidia tu. *(Makofi)*

Mimi ningelipenda na Serikali na sisi Serikali za Afrika Mashariki zinataka kuona amani katika maeneo hayo kwa sababu tukishapata amani, ndiyo tunaweza sasa tukaungana, tukapata soko tena kubwa la watu wengine wengi, tukasaidiana katika kupambana na umaskini kuwaletea watu wengi maendeleo, watu wa nchi zetu tano. Lakini huwezi ukaleta maendeleo katika hali ya vurugu na vita.

Nashukuru sana Rwanda wanaendelea vizuri sana. Tunawaombea amani ambayo imepatikana nchini Rwanda iendelee kudumu na kudumishwa. Tunaombea hivyo hivyo ndugu zetu wa nchi ya Burundi. Lakini lazima tukubali Rwanda na Burundi ni nchi jirani na *Treaty* kwenye hiyo ibara ya tatu moja ya vigezo ni hiyo *Geographical Proximity* ule ukaribu.

Kwa hiyo, kijiografia, tuko karibu sana. Lakini pia kiutamaduni na mila na desturi zetu, mimi nimetembelea mara nyingi sana Burundi na Rwanda, ukiwaona wale wananchi, huwa najiuliza rafiki yangu Mheshimiwa Msambya, yaani ni wa pande wa Tanzania huku! Nikimwangalia rafiki yangu Naibu Waziri wa Kazi, *features* nyingine zinafanana kabisa! Lakini kubwa ambalo nataka kulisema, ukiangalia mila, desturi na utamaduni, yaani unafanana kweli jamani.

Sasa mimi ningelipenda hawa kama tukikubali kwamba ni ndugu zetu, hata nyumbani kwetu mimi wapo wakorofi, nyumbani kwangu katika familia yangu wapo wakorofi. Lakini mtu akiwa mkorofi ambaye ni ndugu yako, haikufanyi wewe ukasema wewe siyo ndugu kuanzia leo. Unatakiwa umsaidie pale ambapo umeona amejikwaa, unamwambia tunakurudisha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi mtazamo wetu ni kuwaona hawa kama ndugu, tusaidiane katika haya, tuweze kuvuka. Nimetumia muda mrefu sana katika hayo maeneo mawili kwa sababu ndiyo *thrust* kubwa ya hoja hii na sisi ndani ya Afrika Mashariki tunataka kujenga matumaini. Lakini lipo hili la soko la pamoja la *Federation.*

Ndugu zangu nimesema katika hotuba yangu kwamba, ndiyo tunaanza maandalizi ya mchakato wa kwenda kwenye soko la pamoja. Nimetoa tahadhari tu. Ardhi na ajira mimi nasema ardhi tukijipanga vizuri wala siyo suala la kututisha kwamba watakuja kuchukua ardhi. Wanaokuja kuwekeza kutoka Kenya au Uganda, mimi nasema ruksa. Wakijenga hosteli ruksa. Watu wanapata ajira na wenyewe wanakipata kipato kilichowaleta hapa.

Lakini wakitaka kuondoka, ile hoteli kwani wataibeba mgongoni? Hoteli itabaki hapa. Lakini kuipata ardhi Tanzania kuna utaratibu wake. Mgeni hawezi akaja Tanzania *unless* tunafanya ule ujanja ujanja maana Watanzania na sisi tuna tatizo hili, tunalea matatizo, mgeni anapitia mgongoni mwa Mtanzania. Mtanzania anapewa tu kibakshishi, ile anakuwa *front.* Unakuta kiwanja kimeandikwa kwa jina la Chenge, lakini ukiangalia yule ambaye yuko pale ni tofauti.

Sasa haya ni matatizo yetu. Tusiseme kwamba sheria haipo, sheria ipo, inakataa. Nina imani hata tukifika kwenye shirikisho suala la ardhi, yatakuwepo masuala ambayo ni ya Muungano na masuala ambayo hayatakuwa ya shirikisho na ardhi, maana ni eneo *sensitive,* tunataka sisi tuliangalie kwa jicho la upendo sana kwamba litaendelea kukaa na sisi *close to our heart.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirikisho hili tunaloliongelea siyo la kutoka juu na ndiyo maana Viongozi wetu Wakuu wa nchi tatu wakasema jamani tumepata maoni, Kamati ya Wataalam ambayo Mheshimiwa Rais Kikwete wakati akiwa Waziri wa *Foreign Affairs* alikuja tena Bungeni, siku mbili tulipewa semina ya kuzungumzia ripoti hiyo, siku mbili, mliongea vizuri na Serikali ikachukua *summary* nzuri sana ikampelekea Rais na ndiyo ni sehemu ya *marching instructions* ambazo mimi nimepewa na Mheshimiwa Rais kwenye eneo hili.

Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na kwa Watanzania, nataka tuwahakikishie kwamba tutakuwa makini sana na kwa sababu tumeingia mle kwa hiari, nchi huru, tutajitahidi twende kwa haraka, lakini pale ambapo tunahitaji maandalizi mazuri, tutawaambia wenzetu jamani tunahitaji muda kidogo hapa. Naamini wenzetu wa Kenya na wenyewe watatuelewa.

Waheshimiwa Wabunge, lakini kubwa tunalolisema, *process* kama mlivyotuambia, nimefurahi sana leo, hakuna Mbunge aliyesimama humu akasema kwamba Shirikisho hili hatulitaki. Wote wanakubali tufike. *(Makofi)*

Hoja ya Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, ni lini tufike huko na njia ya kufika huko. Sasa ni muhimu sana hatua ambazo zimo ndani ya *Treaty* maana *tripple* tunaanza na *Common Custom Union* ambayo tunaitekeleza sasa. Nimeeleza vizuri asubuhi ninavyoamini mimi kwamba, hiyo ndiyo iwe kama kigezo chetu. Tukitekeleza vizuri hiyo, inatupa matumaini ya kwenda katika hatua inayofuata na vile vile kwenye *Common Market,* Soko la Pamoja tukitekeleza vizuri haya masuala ni ya kuaminiana.

Kuna rafiki yangu mmoja ameniletea ki-*note* akasema nimekuelewa. Lakini bado sijakuelewa. Nataka nikubaliane naye kwamba haya ni masuala ya kuaminiana katika kila hatua. Ni kama wewe rafiki yako unamkaribisha kuja nyumbani kwako mnataka kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 97 – WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**

Kifungu cha 1001 – *Administration and General*... ... ... ... Sh. 1,075,709,300/=

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nazungumzia *vote* 97 *programu* ya 10 *sub -vote* 1001 kifungu kidogo 250100 mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hoja, nashukuru sana alinisahihisha kutokana na kauli ya kwamba nilitamka kwamba kuvunjika kwa lililokuwa shirikisho la Afrika Mashariki wakati tulikuwa bado hatukufikia kwenye shirikisho.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sahihisho hilo ambalo kwa kweli ilikuwa imekusudia kuwa iliyokuwa ni Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Sasa nilipokuwa nachangia hoja, nilikuwa na lengo au mpaka sasa hivi na nia ya kutahadharisha kwamba, taratibu au mwenendo ambao ulipelekea Jumuiya ile ya Afrika Mashariki na sio shirikisho kama nilivyotamka hapo awali, tusije tukarejea yale matatizo

au matayarisho ambayo yalisababisha mpaka ikavunjika hiyo Jumuiya iliyopita. Kwa hiyo, naomba nisahihishe hiyo kauli yangu kwamba, sikukusudia kwamba ni shirikisho, lakini nilikusudia Jumuiya. Naamini wazi kwamba Mheshimiwa Waziri yuko makini sana na nina hakika kwamba shughuli zote zinazohusiana na shirikisho hili tunalolielekea kufuatana na Jumuiya yetu hii ya Afrika Mashariki, atafanya vizuri na naunga mkono tena kwa asilimia zote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nafikiri hiyo sio hoja ya kujibiwa na Mheshimiwa Waziri, naona Dr. alikuwa anaweka msisitizo na amekubali kwamba Mheshimiwa Waziri ana uwezo wa kuyafanya hayo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nimepokea majibu ya Mheshimiwa Waziri, *vote 97* programu 10 *sub-vote* 1001 *sub-vote* tena 250100 - Mshahara wa Waziri. Suala ninalotaka kuzungumzia ni la kisera. Kuna mambo matatu ambayo napenda Waziri anifafanulie zaidi. Namshukuru kwa ufafanuzi mwingine ambao alikuwa ameutoa na hasa hasa kuhusiana na suala la uanachama wa Rwanda na Burundi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, namshukuru sana.

Cha kwanza ambacho nilikuwa napenda nifahamishwe zaidi na nilikieleza katika *point* zangu akijibu Mheshimiwa Waziri, niilisema suala la kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya *Customs Management Act* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kifungu cha 112(2), kinasema kwamba *preferential treatment* zote ambazo *member countries* zinazitoa kwa mfano Tanzania inayotoa kwa *SADC* na Kenya na Uganda inatoa kwa *COMESA*, inapaswa kwisha itakapofika tarehe 31 Desemba, 2006. Kwa hiyo walitoa miaka miwili ya *UA*. Lakini mpaka sasa hakuna utaratibu wowote unaofanyika kwa ajili ya hiyo *preferential treatment* kuweza kuondolewa.

Kwa hiyo, nilikuwa nimeshauri kwamba aidha tuka-*amend* hii *bill*, tu-*amend* hii *act customs management act* au tuhakikishe kwamba tunaondoa hizo *preferential treatments.* Nilikuwa naomba Waziri anipatie jibu katika hilo.

La pili, kuanzia mwaka 2004, Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wabunge wa *ER* waliwasilisha katika Bunge la *ER* Muswada wa sheria ambao unaitwa *joint trade negotiations bill*, ambao ulitaka nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinapokwenda kufanya majadiliano ya kibiashara na nchi nyingine, zifanywe kama *block*, kwa maana ya kwamba Balozi zetu za Geneva na Brussels ziweze kufanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na *negotiation power* kubwa zaidi. Lakini na bahati nzuri kwamba wewe mwenyewe ulikuwa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali kipindi kile, *Sector Committee* ya Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliuchukua huu Muswada na ukaukataa na sasa hivi kuna kesi kuhusiana na suala hili, katika Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Sasa bahati nzuri amekuwa Waziri wa Wizara hii. Je, atatoa ushirikiano kwa Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhakikisha kwamba sheria hii inapita ili kuweza kuweka nguvu yetu ya kujadiliana kibiashara na mataifa mengine?

La mwisho, nilizungumza hapa kwa mujibu wa mapendekezo ya Kamati ya *WACO* kuhusiana na *frustrating* ya shirikisho la Afrika Mashariki. Inatakiwa Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakae Arusha. Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Wizara yake nzima bado wako Dar es Salaam, ni lini wanakwenda kukaa Arusha?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, kwa maelezo yake. Kama nilivyosema wakati nahitimisha hoja yangu ni mtu makini na tutaendelea kusaidiana mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya maswali au ufafanuzi ambao Mheshimiwa Zitto Kabwe ameomba, kwanza nimshukuru, alinileteа ki-*note*, nimeghafilika tu kwa sababu ya muda na mambo ni mengi na ningependa tu niseme yafuatayo:-

Nianze na hili la ripoti ya *WACO.* Ni kweli mapendekezo hayo yanasema hivyo, lakini ripoti ya *WACO*, yeye alitumwa na Viongozi Wakuu wa nchi zetu tatu na wenzake, kwenda kufanya kwa mujibu wa hadidu za rejea walizopewa na kwa maana hiyo, waliwasilisha ripoti yao wakawa wamekamilisha kazi. Sasa ripoti hiyo wanayoimiliki ni hawa Viongozi Wakuu wa nchi zetu tatu. Wao wamemaliza kazi zao na ni kweli nasema, moja ya pendekezo ni hilo, Mawaziri wanaoshughulika na masuala haya wakae Arusha. Uamuzi wa Viongozi wetu Wakuu wa nchi tatu kwa suala hili ni kwamba kwa sasa Mawaziri hawa waendelee kukaa katika Miji Mikuu ya nchi zao, hadi hapo uamuzi utakaoachukuliwa na Viongozi wetu hao baadaye. Mantiki unaiona, kwanza mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, hilo la *federation* na nafasi hii, unaona ziko hatua mbali kidogo. Mawaziri hawa wametajwa, kwa sababu hata kabla ya kuteua Mawaziri mahsusi, walikuwepo Mawaziri. Mheshimiwa Rais wetu wa sasa ameifanya kazi hii na Mawaziri wa *Foreign Affairs* ndio ilikuwa kazi yao. Lakini kubwa ambalo tunalisema ni kwamba, shughuli hizi tunazifanya kwenye Vikao rasmi Arusha. Wakati ukiwadia, tukiona kwamba sasa wakati umewadia na kazi ipo ya kutosha ya kuweza kufuatilia shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa karibu, naamini Viongozi wetu Wakuu watatuelekeza iwe hivyo.

La pili, ni kweli kuna kesi hiyo inayosubiri uamuzi mbele ya Mahakama ya Afrika Mashiriki inayohusu uamuzi wa *Legal and Judicial Sector Council* kuhusiana na *joint negotiation bill*. Mimi nisingependa sana niliendeleze hilo kwa sababu ya misingi ile ile ya kisheria, kwamba kwa kanuni zetu, nitakayoyasema haya, nisingependa niwe *quoted* kwa sababu nilikuwa sehemu ya ule uamuzi nikiwa kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, mimi ningelipenda niliachie hapo, lakini shabaha ya Muswada huo, hakuna anayeweza akaipinga. Lakini kuna hoja za msingi ambazo zilikuwa *raised* kuhusiana na utaratibu. Nadhani ndizo hizo tunataka zipate uamuzi, maelekezo ya Mahakama ya haki ya Afrika Mashariki.

La tatu, ni kuhusiana na kifungu cha 112, kifungu kidogo cha kwanza cha (a) kikisomwa na kifungu kidogo cha pili cha sheria ya usimamizi ya ushuru wa forodha ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Kabwe ni kweli kabisa. Ndiyo sheria inavyosema na ni sheria ambayo imepitishwa na Bunge la Afrika Mashariki, ni sheria ambayo inatufunga sisi kama nchi wanachama na lazima tuheshimu. Lakini suala hili limekuwa na mjadala katika Vikao rasmi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu tunaangalia wanachama wetu kama wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Jumuiya nyingine za kimataifa, kama *WTO* ambayo sisi ni wanachama na tulikuwa tunaliona kwamba labda suala hili tulifanye lijikite na *commitments* za nchi zetu tatu katika uanachama wetu huo.

Nadhani huo ndio mwelekeo na tutakapopata maridhiano ndani ya nchi zetu tatu, itabidi kifungu hiki cha sheria ambacho ni sahihi kabisa kama alivyokisoma Mheshimiwa Zitto, itabidi sasa tukirekebishe ili kiendane na mtazamo huo ambao nimeueleza.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niko kwenye *program 10 sub-vote* 1001, *sub-vote* 250100, ningependa kupata ufafanuzi kwenye kitabu cha Waziri ukurasa wa 28, ningenukuu tu baadhi ya mistari, "Hivyo itabidi tupate muda wa kutosha kujiandaa na masuala haya ya ardhi na ajira na tunawaomba wenzetu wa Kenya na Uganda watuelewe. Waziri alipokuwa akijibu hoja za Wabunge ni ruksa Mkenya kupata ardhi Tanzania, sasa inapingana na maelezo yake katika ukurasa wa 28. Sasa napenda kupata ufafanuzi, hivi ardhi iko katika ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki? Kwa sababu naona ni vigumu sana Mtanzania kupata ardhi Kenya. Mimi niko mpakani tunapakana na Kenya.

Suala la pili, ningependa kuulizia mpaka wa Tanzania na Kenya, karibu wananchi wote walioko mpakani ni wafugaji pande zote, nikianzia Longido; Longido tunapakana na Kenya, Ngorongoro wanapakana, Tarime wanapakana, Serengeti wanapakana, Loria wanapakana na Kenya, Uganda, Karagwe, Misenyi, kwa Naibu Waziri na Karagwe. Wilaya zote nilizotaja ni Wilaya za wafugaji. Kwa hiyo, wanapakana pande zote, wafugaji wa upande wa Kenya na wafugaji wa upande wa Tanzania, kadhalika Uganda na Tanzania.

Sasa wenzetu wa Kenya kwa sababu Kenya ndio wanafahamu zaidi, wameweka utaratibu mzuri sana wa wafugaji kufanya biashara. Sasa Tanzania huku hatuna utaratibu. Wafanyabishara wanatumia njia za panya. Hivi nashindwa kuelewa kama wananchi wa nchi yako, umejiunga na Afrika Mashariki, lakini wananchi walioko mpakani hawajui kabisa wala hawajui kitu kinachoitwa Afrika Mashariki, biashara inayofanyika katika nchi zote mbili, lakini upande mwingine wanafahamu na wanafaidi mifugo ya Watanzania. Sasa nataka kujua kama ufugaji haupo katika *East Africa Community.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer, naomba sasa uende kwenye swali lako maana dakika tano zimekwisha sasa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Ndio nataka nipate maelezo, wananchi hawa wote walioko mpakani ambao ni wafugaji, hawajahesabiwa au hawana utaratibu katika biashara hii ya Afrika Mashariki?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimjibu Mheshimiwa Michael Laizer, Mbunge wa Lungido, maswali au nimpe ufafanuzi alioutaja katika maeneo mawili kama ifuatavyo:-

Lile la ardhi yawezekana Mheshimiwa Mbunge hakunipata vizuri, maana nilichosema ni kwamba, ardhi Tanzania inasimamiwa na Sheria na tukasema kwa mujibu wa Sheria hiyo, mgeni kama anataka kuja, amependa ardhi ya Tanzania, hawezi akaipata ng'o. Nikaeleza kwamba, yapo matatizo ambayo tunayasababisha sisi wenyewe. Lakini kama Mkenya anakuja Tanzania kama mwekezaji mwingine, amepitia taratibu zote, nilitoa mfano kwamba, kama anataka kuwekeza katika kujenga hoteli, hiyo nikasema ruksa. Kwa sababu atakuwa amefuzu vigezo vyote vya kumwezesha kuwekeza hapa na sisi angalau tunufaike. Akiamua kuuza hisa zake kwa mtu mwingine, nilisema jengo lile hatalibeba mgongoni na kuondoka nalo kwenda kokote au kurudi nalo Kenya, litabaki hapa hapa.

Nikaendelea kusema hivi, niwaondoe wasiwasi Watanzania, hata katika hatua inayokuja, hata kule mbali iwapo ishara itafika kwenye shirikisho, ni kwamba eneo hili tutakuwa makini kuhakikisha kwamba halitakuwa sehemu ya mambo ambayo yatakuwa ni ya shirikisho. Tunataka shirikisho libaki na yale masuala muhimu tu.

Hiyo ndiyo ninavyoiona mimi, lakini kubwa zaidi, tusiogope kwa sababu na sisi Watanzania haipendezi kuwa tunasema ardhi. Ardhi hiyo, tungependa tutumie misingi ya kisasa ya utumiaji wa ardhi hiyo iwe na faida kwako. Haiwezekani unaiangalia tu, unasema hiyo ni ardhi yangu sawa, lakini unanufaika nayo vipi? Tungependa sasa kama unataka kulima, kweli lima ya kisasa, tuwe wasasa katika kilimo chetu, tuwe wasasa katika kufuga, tuwe wasasa katika uvuvi. Yote hii ndio tunasema itatuwezesha sisi Watanzania kujikwamua kwanza kupambana na umaskini, lakini kuweza pia kuhimili ushindani huu. Mimi nadhani tukienda hivyo, hakuna linaloharibika kwa suala zima la ardhi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amenijibu moja, lingine hajanijibu.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana. Kwa upande wa mifugo, soko la mifugo amelisemea sio leo tu. Nakumbuka moja kwenye Kamati alianza yeye Mheshimiwa Lekule, halafu Mheshimia Cheyo akaingia, nikasimama hapa nikatoa maelezo, nataka nirudie tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hivi, sasa hivi nchi zetu tatu tunakamilisha taratibu za kulinda afya ya wanyama, afya ya binadamu na mimea, ambayo tunaita *sun trap* na fito, *sun trap measure* kwa sababu ni muhimu sana kama tunataka tuifanye kazi hii kwa uhakika na ndio maana nikasema tupeni muda tu kwa sababu suala hili hatungelipenda tuone Watanzania mnapeleka biashara kule, halafu mnarushwa kwa sababu ujanja unaotumika upande fulani wa mpaka ni kwamba fedha unayolipwa kwa mifugo ambayo umeuza kule hawakulipi wewe, analipwa wakala. Iwapo mambo

yatakuaharibikia, lazima utakimbilia upate msaada wa Ubalozi wetu au na Serikali yake. Sasa haya tunataka tuanze kuyawahi mapema.

Lakini pili, tunataka tuwe na utaratibu ambao utahakikisha kwamba Serikali inapata mapato yake ya kodi na watu wasitumie ujanja huo wa kupeleka kuvusha mali bila kulipia kodi stahili kwa mapato ambayo wanayapata. Hiyo ndio dhana ambayo tunayo na sio kwamba tunakataa Watanzania wasifanye biashara hiyo muhimu. Mheshimiwa Lekule, kama yuko jirani pale, najua uwezo wake ni mzuri tu pamoja na wananchi wa Jimbo lake kuweza kuwafanya.

Lakini nasema, tuwahamasishe wananchi wetu kwenye maeneo yetu ya wafugaji. Tusifanye hii biashara ya kuswaga mifugo kwa miguu au kulundika kwenye Fuso, unasema basi nimepata soko, lazima ifuate utaratibu wa sheria. Sheria yetu *veterinary*, kama ilivyo sheria ya Kenya inakutaka uwe na kibali kwa sababu tunataka tuhakikishe kwamba hutuharibii soko letu kwa kupeleka mifugo au wanyama ambao wana magonjwa katika nchi ya Jumuiya wanachama wa Afrika Mashariki.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba ufafanuzi zaidi. Waziri amesema tunataka kuwalinda wafanyabiashara wetu wasirushwe. Nadhani wafanyabiashara wanaokwenda Kenya ni wengi sana, wanakwenda nadhani hata hao wafugaji ambao hujawawekea utaratibu, bado wanakwenda, asilimia 60 ya mifugo inayouzwa Kenya ni mifugo ya Watanzania. Kwa hiyo, sijui ni ugonjwa gani. Anasema tulinde ugonjwa usipelekwe Kenya au usiletwe Tanzania kwa sababu bado mifugo inakwenda Kenya. Ningependa tu kuomba ufafanuzi: Hivi kwanini Serikali isiweke utaratibu tu waende kama wanavyokwenda? Lakini kwa utaratibu huu na Serikali yetu ifaidike, sio kwamba mifugo hawaendi na wafanyabiashara ambao hawaendi Kenya au hawana utaratibu ni wa mifugo tu, wengine wanakwenda, hujawalinda hao ili wasirushwe? Ni wafugaji tu ndio ana hofu kwamba watarushwa?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, utaratibu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, kwa mujibu wa kanuni 21, 1 mpaka 6, Mbunge anaruhusiwa kusimama mara mbili tu kwa ajili ya kuomba ufafanuzi. Mara ya tatu ni kutoa Shilingi. Kwa hiyo, ninadhani kuhusu kwa mwongozo wako, Mheshimiwa Waziri hapaswi kujibu swali Mheshimiwa. Aidha, anatoa Shilingi au hatoi Shilingi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona Mheshimiwa Zitto hakuzingatia jinsi tulivyokuwa tunaendesha Kikao hiki. Kwa sababu mara ya pili ambayo Mheshimiwa Mbunge amesimama, alikuwa anakumbusha swali lake la pili ambalo lilikuwa halijajibiwa. Hivyo akataka swali hilo lijibiwe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zitto, nafikiri hakuna kanuni ama utaratibu uliovunjwa. Kama angekuwa amesimama kwa hoja mpya, kwa maana hiyo, tusingeweza kumruhusu.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimjibu tu rafiki yangu Mheshimiwa Laizer kwa swali lake kwamba, Serikali haina nia ya kuwazuia Watanzania wanaotaka kufanya biashara ya mifugo kupeleka katika soko hili. Ndio maana tumeanzisha Umoja huu wa Forodha ambao tunautekeleza sasa hivi. Lengo lake ndio hilo kuwa na soko pana ambapo wananchi wetu wataweza kunufaika, hususan katika mifugo na mazao ya mifugo. Lakini iwapo anaamini kwamba kuna Mtanzania ambaye ana kibali sahihi kutoka kwa ma-*vet officers* wetu na amepata soko na ana kibali cha upande wa pili wa mpaka, naye ana-*permit* ya kule, basi tungelipenda tupate hiyo, maana ni sehemu ya zile tunazozita vizigiti visivyo vya kodi *(non tariff barriers)* na tuna utaratibu wa kuweza kuyashughulikia matatizo kama hayo.

Lakini mimi nilikuwa naelezea ambalo linawahusu Watanzania wengi wenye mifugo. Hatutaki kuharibu soko letu na jina la nchi yetu, kwa sababu tu eti mwananchi amepata soko pale. Waziri wa Mifugo alilieleza vizuri sana wakati anawasilisha na ndio maana nikaomba sana. Sisi kazi yetu kama Serikali ni kuharakisha hizi taratibu zikamilike mapema, tuwatangizie Watanzania wote wanaopenda kutumia fursa hii waweze kufanya hivyo.

Mimi hiyo ndio rai naitoa na nitahakikisha kweli tusukumane ndani ya vyombo hivi husika, tuweze angalau suala hili tukalifanya kuwa ni la historia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1002 - *Finance and Accounts*... .Sh. 108,794,900/=

Kifungu cha 1003 - *Policy and Planning*... ... Sh.5,206,081,600/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1004 - *Trade, Finance and Investment* ... ... ... ... ... ... Sh.178,355,500/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru fungu hilo *subvote* 1004 kifungu kidogo 260100 najikita pale kwenye *Communication* na *information*.

Nilipozungumza kwa mdomo na kwa maandishi, nilizungumzia kuhusu mwongozo au *guide lines* zilizoandaliwa na *East African Committee Secretariat*

kuongoza *development projects* au *investments* kwenye maeneo ya mpaka katika nchi zetu za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nilisema, hizi ni muhimu kwa sababu ziliandaliwa miaka miwili au mitatu iliyopita na zinatutaka kwa mfano, mradi ule magadi ulizozungumzwa na Wizara ya Viwanda jana, juzi au ujenzi wa barabara kutoka Mgumo, kupitia Loliondo kuja Mto wa Mbu, kwa utaratibu ule unatutaka *EIA* ihusishe *very closely issue* zote mbili zinazohusika kwa sababu ni *resource* zilizo mpakani.

Sasa nilichotaka kupatiwa ufafanuzi ni kuwa: Je, tumeridhia *guide lines* hizo na kwamba sasa ni lazima zitumike au bado hazijaridhiwa? Kwa hiyo, tunaweza kuendelea kufanya *EIA* ya *developments* kwenye maeneo ya mpaka bila kuwahusisha majirani?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulipata mchango mzuri wa Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, kama ilivyo kawaida yake. Kwenye eneo hilo niseme tu kwamba, ni kweli zile *guide lines* za *impact assessment* za kwenye maeneo ya mipakani zilijadiliwa na zikakubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua inayofuata ni kuanza ule mchakato wa kupata idhini ya Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki, yaani *The Council of the Ministers* kwenye suala hilo na nadhani ni miongoni mwa *protocols* ambazo zinasubiri kuwasilisha kwa sababu ile *protocol* nyingine ambayo unaikumbuka wewe kama mwana mazingira ambayo *the Protocol on the Environment National Resources* ilisainiwa katika Mkutano uliopita wa Baraza la Mawaziri iliyofanyika Mjini Arusha mwezi Aprili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nasema, kwa hii ambayo ndiyo nasema ni muhimu sana kwa hali ya sasa, nataka niseme bado haijafika na ikishapata idhini hiyo, lazima tufuate sasa *formalities* za kisheria za kuja humu Bungeni, kwa sababu ni itifaki ambayo itakuwa sehemu ya mkataba wa kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ipate ridhaa ya Bunge hili kwa maana ya *ratification*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1005 - *Economic and Social Infrastructure*... ... ... Sh.511,769,500/=
Kifungu cha 1006 - *Political, Defence and Security*... ... ... … Sh.76,546,200/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa mwaka wa Fedha

2006/2007 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa heshima na taadhima, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Naibu Waziri wake na timu nzima ya wataalam wa Wizara yao, kwa kuweza kupitishiwa Bajeti yao ya Fedha na hivyo tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa shughuli zao kwa mwaka huu. *(Makofi)*

Ninaomba niseme tu kwamba, nimewasiliana sana na Mheshimiwa Seif Khatib na masuala ya lugha hayana matatizo tena. Kabla sijaahirisha Bunge naomba nitangaze yafuatayo:-

Tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, anasema anaomba niwatangazie Wenyeviti wa Mkoa ya Tanzania Bara, wakachukue bahasha zenye majina ya waliopangwa kwenye Mikoa yao. Kwa kuwa orodha ni kubwa, tumegawa kimkoa ili Waheshimiwa Wabunge wapate kuondoka hapa Bungeni wakiwa na orodha hiyo mikononi mwao.

Waheshimiwa Wenyeviti wa Mikoa, Makabrasha hayo, yanapatikana *Documentation Room* ya Bunge. Kwa hiyo, kila Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge ya Mkoa akachukue kwa niaba ya Wabunge wenzake ili mambo hayo yaende vizuri.

Pia, Waheshimiwa Wabunge, kuna Mheshimiwa amepoteza ufunguo wake wa gari. Tunaomba sana ahakikishe kwamba anaupata, asije akashindwa kurudi nyumbani leo na akalala hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine. Kwa ruhusa ya Mheshimiwa Spika, ameniomba niwatangazie kwamba, tarehe 14 jioni tutakuwa na sherehe maalum kwa ajili ya Wabunge wote. Sherehe hiyo itakuwa na maudhui mawili makubwa.

Kwanza, ni kumuaga Mheshimiwa Spika, aliyestaafu madaraka yake, Mzee wetu Pius Msekwa, lakini pili itakuwa ni sherehe ya kupongezana na kupeana pole kwa safari hii ndefu ya Bunge la Bajeti la kwanza katika Serikali hii ya Awamu ya Nne.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli hiyo itaambana na mambo mbalimbali. Kamati inayoandaa sherehe hiyo, imeshafanya kazi kubwa na ya kutosha na tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuhudhurie wote kwa umoja wetu.

Lakini pia kutakuwa pia na masuala ya zawadi mbalimbali za hapa na pale. Kwa hiyo, ingekuwa vizuri uwepo ili zawadi yako uichukue wewe mwenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndio matangazo ambayo yako kwenye meza yangu kwa jioni hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya, ninaomba sasa niahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.09 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 10 Agosti, 2006 saa Tatu Asubuhi)*